

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tisa - Tarehe 29 Aprili, 2005**

*(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Mfuko wa Fedha za Barabara kwa Mwaka 2002/2003 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Roads Fund Board for the Year 2002/2003*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa Mwaka Ullioishia tarehe 30 Juni, 2004 (*The Annual Report and Accounts of Tanzania Communications Regulatory Authority for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2004*).

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Makumbusho ya Taifa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 (*The Annual Report and Accounts of the National Museum of Tanzania for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2004*).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali ya Mwaka 2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi ya Mwaka 2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira ya Mwaka 2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:** Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje ya Mwaka 2004.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya Mwaka 2004.

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 116

### **Kufutwa kwa Tume ya Utangazaji**

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika taaluma ya mawasiliano ya umma kuna utenganisho kati ya vyombo vinavyotumiwa (*tools*) na maudhui yanayobebwa na vyombo hivyo hususan redio, televisheni, magazeti na kadhalika na kwa kuwa Taifa lolote lile lazima litathmini wakati wote aina ya maudhui ya vyombo vya habari kama chakula cha fikra cha mtu kila siku kielimu, kiuchumi na kijamii na kwa kuwa kila jamii hujitahidi kulinda utamaduni wake usiathiriwe na maudhui potofu ya vyombo vya habari:-

- (a) Je, kwa nini Serikali iliamua kuifuta Tume ya Utangazaji iliyokuwa ikifanya kazi nzuri ya kusimamia utengamano wa maudhui ya vyombo vya habari?
- (b) Je, kazi ya kufuatalia ubora na athari za maudhui ya vyombo vya habari sasa inafanywa na chombo gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Tume ya Utangazaji haikufutwa bali iliunganishwa na Tume ya Mawasiliano hapo Novemba 1, 2003 na kuundwa chombo kilicho bora zaidi kijulikanacho kama Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (*Tanzania Communications Regulatory Authority - TCRA*).

Kuunganishwa kwa Tume ya Utangazaji na Tume ya Mawasiliano kumetokana na mabadiliko katika teknolojia ambayo yamesababisha muunganiko wa huduma mbalimbali za utangazaji na mawasiliano (*Covergence of Broadcasting and Telecommunications into Broadcasting Services*).

Matokeo yake ni kwamba hivi sasa unaweza kupata huduma za simu, takwimu, redio na televisheni kuititia miundombinu ambayo hapo awali ilitumika kwa kutoa huduma moja tu. Vile vile hivi sasa unaweza kupata matangazo ya radio na televisheni kwa njia ya *internet*. Kutokana na mabadiliko hayo, tofauti zilizokuwepo awali zimepotea na kwa hiyo taasisi zilizokuwa zinadhibiti utangazaji na mawasiliano zililazimika kwenda sambamba na mabadiliko hayo ya teknolojia.

(b) Kazi ya kufuutilia ubora wa maudhui ya vyombo vyatangazaji uliokwa unafanywa na Tume ya Utangazaji ya vyombo vyatangazaji umeimarishwa kwa kuwa na chombo kinachoitwa Kamati ya Maudhui (*Content Committee*). Kamati sheria iliyounda Mamlaka ya udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) kifungu 25 na kifungu 26 cha sheria hiyo Na. 12 ya mwaka 2003 inatoa Mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya utangazaji kuunda Kamati ya Maudhui kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Bodi ya *TCRA*.

Kazi ya Kamati hiyo ni kudhibiti ubora wa vipindi vinavyorushwa na vituo vyote vyatangazaji nchini. Ubora huo ni pamoja na kuzingatia utamaduni wa Watanzania ili usiathiriwe na maudhui potofu ndani na nje ya nchi. Kamati ya Maudhui imeshaundwa.

Na. 117

### **Ubomoaji wa Vibanda vya *Marching Guys* katika Miji**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya majukumu ya Serikali yoyote ni kuwapatia raia wake ajira, na kwa mazingira ya sasa ni kuweka sera ambayo itaweka mazingira mazuri ya kukuza sekta binafsi na kujajiri kwa lengo la kuongeza uchumi wa nchi, na kwa kuwa wafanya biashara ndogo ndogo maarufu kama *Marching guys* wameamua kujajiri kwa kufuata masoko yaliyopo lakini wanapata bughudha mbalimbali; ikiwemo ya kubomolewa kwa vibanda vyao vyatangazaji:-

(a) Je, Serikali inatoa maelekezo gani juu ya ubomoaji wa vibanda vya muda vyatangazaji ya wafanya biashara mbali na jukumu lake la kuwapatia ajira na je, imefanya utafiti ili kujua ni hasara ya kiasi gani imetokana na ubomoaji wa vibanda hivyo pamoja na kuharibu mitaji na hasara za kiuchumi kwa Taifa na hususan kwa Manispaa husika?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuboresha mazingira hayo ambayo mnunuzi na muuzaji wanavutwa kufanya biashara kwa kuyahalalisha kisheria, ili Manispaa ziweze kuongeza mapato yake na kujenga sehemu za kufanya biashara kwa kuzingatia mandhari nzuri ya kuhifadhi mazingira na majengo ya muda ambayo yaweza kuhamishwa?

(c) Je, Serikali haioni ubomoaji huo wa vibanda vya biashara unakiuka azma nzima ya kupunguza umaskini na kusababisha ongezeko la uhalifu na wizi wa kutumia silaha na mauaji ya raia wema, hali ambayo pia inachangiwa na kutowawezesha wananchi kuboresha na kukuza sekta ya kilimo vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abu Kiwanga,

Mbunge wa Jimbo la Kilombero, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ubomoaji wa vibanda vya muda vya wafanya biashara hufanywa na Halmashauri husika, Serikali imeziagiza Halmashauri zote kutenga maeneo ya kufanya biashara ndogo, yawe ya muda au ya kudumu, kwa nia ya kuwapatia ajira wafanya biashara ndogondogo. Mara kwa mara wafanya biashara ndogo hawayatumii maeneo yaliyotengwa na Halmashauri badala yake hufanya shughuli zao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

Kwa hiyo, Halmashauri hulazimika kuwahamisha wafanya biashara hawa kwa hiari au kwa nguvu. Ofisi yangu haijafanya utafiti wa hasara za kiuchumi kwa Taifa kutokana na mazoezi haya yanavyoendeshwa. Napenda kusisitiza tena kwa Halmahauri zote kutenga maeneo kwa ajili ya wafanya biashara ndogo ndogo.

Vile vile katika wafanya biashara ndogo wanaagizwa kufanya biashara zao katika maeneo yaliyotengwa. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuzipongeza Halmashauri za Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke, Moshi, Iringa, Mbeya Dodoma na Tanga kwa kutenga maeneo yanayotumika kikamilifu na wafanya biashara hao kama nilivyofafanua wakati ninajibu swali Na. 100 la Mheshimiwa Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Jimbo la Kwela tarehe 11/2/2005.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishazielekeza Halmashauri zote kutenga maeneo ya kufanya biashara ndogo ndogo na kuyaboresha kwa kuweka huduma zote muhimu kama vyoo, maji, umeme ili yavutie na kuhalalishwa kisheria. Halmashauri zinaendelea kuzingatia maelekezo haya kama mifano michache nilioitoa katika sehemu ya (a) ya jibu la swali hili.

(c) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wafanya biashara ndogo ndogo una lengo la kuwawezesha wnanchi hao kufanya shughuli zao kwa kuzingatia sheria na taratibu na hivyo kuwawezesha kupambana na umaskini ipasavyo. Pale ambapo wafanya biashara ndogondogo hufanya biashara zaokatika maeneo yasiyoruhusiwa, Halmashauri huwaagiza wafanya biashara hao kubomoa na kuhama kwa hiari yao. Wengi wanahama isipokuwa wachache ambao wanakiuka taratibu za Halmashauri. Kwa sasa Ofisi yangu haijapata taarifa za kushuka kwa sekta ya kilimo na ongezeko la uhalifu wa silaha unaosababishwa na ubomoaji vibanda vya wafanya biashara ndogo.

Na. 118

#### **Vituo vya Afya Kyela**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kyela inazo Tarafa mbili za Unyakyusa na Ntebela ambazo zimegawanyika katika Kata 15, na kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002 Wilaya hiyo ina wakazi 174,000.

(a) Je, kwa mujibu wa sera za Afya za Serikali; wananchi 174,000 wanaokaa katika Kata 15 wanastahili kuhudumiwa na Vituo vya Afya vingapi?

(b) Je, isingekuwa jambo la busara kwa Serikali kusikiliza kilio cha wananchi wa Kyela katika Tarafa ya Unyakyusa kujenga kituo cha Afya katika mji mdogo wa Kasumulu ili kuhudumia maelfu ya wakazi wa mji mdogo wa Kasumulu pamoja na vijiji vya jirani vya Njusi, Isaki, Lubale, Kilasilo na Ibanda?

(c) Kwa kuwa, hii ni mara ya pili Mbunge wa Kyela anaiomba Serikali kujenga Kituo cha Afya katika Tarafa ya Unyakyusa bila mafanikio. Je, Serikali imelichukuliaje ombi hilo, kana kwamba sio jukumu lake na inawaambia nini wananchi wa Kyela?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Livingstone Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera na Miongozo ya Wizara ya Afya, Zahanati inahudumia watu wapatao 6,000 hadi 10,000, Kituo cha Afya kinahudumia watu 50,000 wakati Hospitali ya Wilaya inahudumia watu 200,000. Kwa kigezo cha idadi ya watu 174,000 Wilaya ya Kyela inastahili vituo vya Afya vitatu (3). Hata hivyo wakati mwagine kigezo hiki cha idadi ya watu huenda pamoja na vigezo vingine vya hali ya kijigrafia kama vile umbali, kutopitika kwa eneo kwa sababu ya milima, mito, ziwa, misitu na kadhalika. Kwa sasa Wilaya ya Kyela ina Kituo kimoja tu cha Afya kilichoko katika Mji Mdogo wa Ipinda Kata ya Ipinda yenye wakati 16,756.

(b) Serikali siku zote inasikiliza vilio vya wananchi wake ikiwa ni pamoja na wa Kyela-Tarafa ya Unyakyusa. Wakati nikijibu swali Na. 375 la Mheshimiwa Mbunge tarehe 4/8/2004 kuhusu ujenzi wa Vituo vya Afya kwa Wilaya ya Kyela nilieleza wazi kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela inao mpango wa kujenga Kituo cha Afya katika Kijiji cha Njusi mpakani mwa Tanzania na Malawi katika Tarafa ya Unyakyusa.

Wakati huo Mheshimiwa Mbunge alikuwa anaomba Serikali iigeuze Zahanati ya Kilasilo iliyoko katika Kata ya Ikolo Tarafa ya Unyakusa ili iwe Kituo cha Afya badala ya kujenga Kituo kipyra cha Afya katika kijiji cha Njusi. Nilimshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri yake ili wafanye maamuzi kwa pamoja juu ya wapi wanataka kujenga kituo hicho cha Afya kati ya Njusi na Kilasilo. Leo Mheshimiwa Mbunge anaomba Kituo cha Afya sasa kijengwe katika Mji Mdogo wa Kasumulu badala ya Kijiji cha Njusi na Kilasilo vyote ambavyo viko katika Tarafa hiyo hiyo ya Unyakyusa ili kituo hicho kiweze kuhudumia vijiji vya jirani vya Njusi, Isaki, Lubale, na

Ibanda.Kijiji cha Njusi, na Mji Mdogo wa Kasumulu vyote viko katika Tarafa moja ya Unyakyusa. Walioamua kuwa kituo cha Afya kijengwe katika kijiji cha Njusi ni Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na siyo Serikali Kuu. Hivyo ninaendelea kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri yake kutatua suala hili la mahali panapostahili kujengwa Kituo hicho cha Afya. Baada ya uamuhi huo Wadau wote hususan Wizara ya Afya, wananchi na wahisani wengine washirikishwe katika hatua zote za maandalizi ili kuharakisha utekelezaji wa ujenzi wa kituo hicho.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali yetu katika harakati zake za kupeleka madaraka kwa wananchi imeliweka wazi suala la namna ya kupata miradi ya maendeleo. Miradi yote ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ya ujenzi wa kujenga Zahanati na Vituo vya Afya inapaswa kuibuliwa na wananchi kupitia Serikali zao za vijiji kwa kuangalia fursa na vikwazo vyao. Baadaye wataandaa mpango wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na kupeleka maombi kwenye Halmashauri zao ili waweze kupewa taratibu za sekta inayohusika, utaalamu pamoja na kuombewa kibali. Jukumu la Seriali ni kuhakikisha kwamba taratibu zimefuatwa na kutoa fedha iwapo mradi huo upo kwenye Bajeti ya Halmshauri.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Nataka tu nipate wasiwasi kwa maendeleo ya kujenga hicho kituo cha Afya huko Kyela kwa sababu Jimbo la Mikumi tumeshajenga Zahanati zaidi ya sita. Kuna utata kati ya TAMISEMI na UTUMISHI na Wizara ya Afya watumishi hawapo. Je, lini watatatua tatizo hilo ili mimi nipate watumishi hao? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, umeanza kwa wasi wasi juu ya Kituo cha Afya cha Kyela, sasa sikuwa na hakika kama ulitaka kisijengwe au hapana. Lakini nimeelewa hoja yako ya upungufu wa watumishi katika sekta ya Afya. Na naomba nirudie maelezo ambayo tumekuwa tukiyatoa siku zote kwamba sekta hii ni kweli inakabiliwa na upungufu wa watumishi na juhudi za Serikali zipo na nyinyi Waheshimiwa Wabunge mnaona kila kukicha kuna jitihada zinafanyika kuzidi kuimarisha sekta hiyo kwa kuwapatia watumishi zaidi. Tutaendeleza jududi hizo kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unapatikana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee jibu la ziada kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri (TAMISEMI) kwamba kwanza naomba niwapongeze wananchi kwa kujenga zahanati na vituo vya afya vingi nchini ili kukabiliana na matatizo ya afya ya wananchi wetu. Pili, Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba afya ya wananchi ni muhimu sana UTUMISHI imeacha kutoa kibali kwa watumishi wa Afya ili Wizara ya Afya yenyewe kila inapopata wahitimu wa ngazi mbalimbali wa Afya wawe wanapelekwa moja kwa moja kwenye sehemu za kazi. (*Makofi*)

### **Mahitaji ya Umeme Jimbo la Ukonga**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI (K.n.y. MHE. DR. MAKONGORO M. MAHANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swalı langu hapo tarehe 115/11/2002 kuhusu usambazaji wa umeme Jimboni Ukonga, iliahidi kuwa maeneo ambayo umeme haujafikishwa na wananchi bado wanatumia vibatari kama yale ya Mongo la Ndege, Ulongoni, Bangulo, Chanika, Mvuti, Msongola, baadhi ya maeneo ya Kitunda, Kinyerezi na Kipunguni kwamba yatafanyiwa utafiti ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kuanzia wakati huo na kwa kuwa, maeneo hayo yote sasa sio vijiji tena bali ni mitaa ndani ya Manispaa ya Ilala yanayozidi kupimwa viwanja na watu wengi wanahamia kwenye maeneo hayo ambayo yanakua kwa kasi kubwa:-

- (a) Licha ya umuhimu wa umeme kwa maendeleo ya wananchi. Je, Serikali inafahamu kwamba, kutokana na wananchi wengi kuhamia kwenye maeneo hayo na kutokana na kutokuwepo kwa umeme, majambazi na wezi wanatumia nafasi hiyo ya kutokuwepo umeme kwenye maeneo hayo na kufanya uhalifu na maficho yao na kufanya wimbi kubwa la uhalifu katika maeneo hayo ambayo sasa yanatisha?
- (b) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya uhakika ya kusambaza umeme kwenye maeneo hayo haraka iwezekanavyo bila kujali tathmini ya kibashara ya *TANESCO* kama ilivyofanyika vijijini kote Tanzania ambako umeme umeperekwa bila hata *TANESCO* kupata faida?

### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalı la msingi la Mheshimiwa Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali iliahidi maeneo ambayo umeme haujafikishwa kwenye Manispaa ya Ilala ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja yangefanyiwa utafiti ndani ya mwaka moja. Serikali ikishirikiana na *TANESCO* imeyafanya utafiti maeneo yote aliyoyataya Mheshimiwa Mbunge pamoja na mengine mengi katika Manispaa ya Ilala ili kujua idadi maombi ya wateja, idadi ya wateja wa uhakika na makadirio ya gharama za kuwaunganishia. Baada ya zoezi hilo, Serikali ikishirikiana na *TANESCO* ilianza kuandaa mikakati ya kuwapatia umeme wateja hao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali inafahamu fika ya kwamba kutokana na kutokuwepo umeme hasa maeneo ya kando kando ya manispaa kama alivyoyataya Mheshimiwa Mbunge kunaweza kusababisha majambazi na wezi kutumia nafasi hiyo ya kutokuwepo kwa umeme kwenye maeneo kama hayo kufanya uhalifu. Ndio maana ni pamoja na sababu zingine za kuleta maendeleo Serikali inafanya kila juhudii kuhakikisha

kuwa maeneo hayo yanapatiwa umeme. Serikali na *TANESCO* wameandaa mkakati wa kusambaza umeme kwenye maeneo hayo kuitia mradi wa kuunganisha jumla ya wateja 100,000 kwa mwaka (100,000 project) nchini kote, mijini na vijijini ambapo tayari huduma ya umeme wa *TANESCO* upo. Hadi sasa hatua na matayarisho ya kuwaunganishia wateja wapya 45,000 wa mwanzo zinaendelea. Zoezi hili litaanza baada ya vifaa kwa ajili ya utekelezaji kuletwa na wazabuni kuajiriwa. Zabuni tayari zilishatangazwa na zitarudishwa mwishoni mwa mwaka huu na vifaa vinategemewa kuanza kuwasili mwanzoni mwa mwezi ujao na kazi inategemewa kuaanza kutekelezwa Juni, 2005. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo aliyoyataja yatajumuishwa katika mradi huu.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Kwa kuwa inaonyesha muda mrefu umepita toka ahadi hii itolewe. Na natambua anasema mwezi Juni vifaa hivi vitakuwa vimepatikana na kwa kuwa pia katika Jimbo la Siha Naibu Waziri alifika na kuona eneo hili na kuna tatizo pia la vifaa, atatuthibitishia hapa kwamba tutapata vifaa hivyo mapema iwezekanavyo kabla ya mwezi Oktoba ili kazi hiyo iwe imekamilika? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu vifaa nya mradi wa umeme kwenye Jimbo la Ukonga ama nilivyoeleza awali napenda nichukue nafasi hii kurejea majibu yangu kwamba vifaa hivi vinatarajiwa kufika mwezi wa tano na kazi kuanza mwezi wa sita. Ni matarajio yetu kwamba kutokana na mipango thabiti iliyopangwa hivi sasa kwamba kazi hii itafanyika. Napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Siha kwa ujumla kwa mapokezi makubwa walionipa wakati tulipotembelea Jimbo la Siha. Na napenda nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Siha kwamba ile miradi ambayo tulipitia na kuona kule na kuzungumza na wenzetu wa *TANESCO* kwamba waneifanyia kazi na kwa uhakika kazi hiyo tayari imeashaanza na miradi ile itatekelezwa.

**SPIKA:** Swali la msingi lilihusu jumbo la umeme la Ukonga, sasa majimbo mengine yalete maswali yao pamoja na jumbo la Kisarawe. Lakini Mheshimiwa Jangu, heshima kwa Mwenyekiti uliza swali.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri kwa kuwa anafahamu maeneo ya Chanika, Mvuti, Msongola yako yamepakana kabisa na maeneo ya Kitanga, Msimbu na Homboza kule Kisarawe. Kwa nini utafiti uliofanywa haukuhusisha maeneo haya ambako hawa majambazi wanawenza wakajificha tena. Je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba sehemu hizi zinapata umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati najibu swali nilikuwa nazungumzia utafiti mahsusuli uliofanywa kwa mujibu wa maombi ya Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ukonga. Napenda nimthibitishie kwamba Serikali inatilia maanani sana maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na nataka nimwahidi kwamba tutayafanyia kazi kama ambavyo ameyataja yeze mwenyewe.

**Rushwa Michezoni**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kupambana na rushwa michezoni Serikali iliandaa warsha kwa wadau 61 wa Kanda ya Mashariki iliyofanyika Morogoro ili kujadili sababu na mianya ya rushwa:-

- (a) Je, ni kitu gani kinasababisha rushwa michezoni?
- (b) Je, wapo watuhumiwa waliokamatwa kwa kula rushwa michezoni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI) (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir, Mbunge wa Nungwi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, zinazosababisha rushwa sehemu yoyote hazitofautiani na zile za michezoni. Rushwa ni rushwa huwezi kutenganisha rushwa michezoni na rushwa ya sehemu nyingine.
- (b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa rushwa inamhusisha mtoaji na mpokeaji imekuwa vigumu kuwanasa wahusika, hadi pale wadau wote watakapotoa ushirikiano wa kupambana na tatizo hili kwa kuwafichua. Kwa hiyo, sina orodha ya watu waliothumiwa kukamatwa kwa kula rushwa michezoni kwa hivi sasa.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBERI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kinachoendelea sasa katika michezo ni uzalendo na ubinafsi ambao unatawala katika michezo. Je, kwa hili Mheshimiwa Waziri atalizungumziaje? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (k.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngwali kama ifuatavyo:-

Vyama vyote vya michezo vina wenywewe. Uko uongozi ulioundwa na vyama husika na yako mabaraza yanayosimamia mwenendo wa utendaji wa vyama hivyo. Kwa hiyo, wanachama wa vyama hivi wasiruhusu huo ubinafsi ukatawala katika vyama vyao vya michezo.

### Ajira kwa Wataalam wa Kigeni

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa bado nchi yetu hajajitosheleza kwa wataalamu wa nyanja mbalimbali na kwa kuwa inabidi tupate wataalamu wa kigeni kuja hapa nchini kufanya kazi.

- (a) Je, Serikali imepata maombi mangapi ya vibali vya ajira kwa wataalamu wa kigeni kati ya mwaka 2000/2001 hadi 2004/2005?
- (b) Je, ni nyanja gani kwa kiasi gani zinaongoza kwa kuingiza wataalamu wengi wa kigeni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, swali lake lenye sehemu (a) na (b) na kama ifuatavyo:-

- (a) Kati ya mwaka 2000/2001 hadi mwaka wa 2004/2005 Serikali imepokea maombi ya vibali vya ajira kwa wataalam wa kigeni kama ifuatavyo:-
  - (i) Julai 2000 mpaka Juni, 2001 ni maombi 2,955;
  - (ii) Julai 2001 mpaka Juni 2002 ni maombi 2,327;
  - (iii) Julai 2002 mpaka Juni 2003 ni maombi 2,725;
  - (iv) Julai 2003 mpaka Juni, 2004 ni maombi 1,989;
  - (v) Julai 2004 mpaka Septemba, 2004 ni maombi 432.
- (b) Mheshimiwa Spika, jumla ya maombi yote kati ya Julai 2000/2001 mpaka Septemba, 2004 ni 10,428. Nyanja zinazoongoza kwa kuingiza wataalam wengi wa kigeni nchini na kwa kiasi gani ni kama ifuatavyo:-
  - (i) Sekta ya Madini (*Mining Services*) ni 30%;
  - (ii) Sekta ya Ujenzi (*Construction*) ni 25%;
  - (iii) Sekta ya Biashara na Utalii (*Commerce and Tourism*) ni 20%;
  - (iv) Sekta ya Uzalishaji Viwandani (*Manufacture*) ni 18%;
  - (v) Huduma za Jamii (*Social Services*) ni 7%.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, katika nyanja hizi alizozitaja Mheshimiwa Waziri jitihada gani zinafanywa kujua kwamba hakuna Mtanzania ambaye ana sifa katika nyanja hizo. Na kwa nini Makampuni ya kigeni yanaajiri wahudumu katika Ofisi zao? Anasema vipi juu ya hili? (*Makofî*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza Mheshimiwa Mwaga, kama ifuatavyo:-

Serikali hairuhusu tu kienyeji kuingiza hawa wafanyakazi kutoka nje. Na haya ni maombi tu nimesema siyo kwamba wote ndiyo walioingia walioomba kazi. Uko utaratibu ambao umewekwa kisheria wa namna ya kuruhusu wafanyakazi wa kigeni kufanya kazi katika sekta mbalimbali. Sekta ya madini kwa mujibu wa sera na sheria inayo sheria yake na sekta nyingine inayo sheria yake. Kila mara tunataka kila mwajiri amepewa nafasi kadhaa chache ambazo anaweza akaajiri watu wa nje. Lakini nyingine zote Watanzania wajazwe. Isipokuwa tu pale ambapo Mtanzania hayupo wa kuweza kujaza nafasi ile ndiyo hawa wageni wanaweza wakaruhusiwa.

Kwa hiyo, kwa taarifa nilizonazo katika sekta nyingi, sijui kama kweli hao wafanyakazi wa aina anayosema Professa Mwaga wapo. Na kama wapo inawezekana kwa sababu hii nchi ni kubwa na inawezekana pia kwani wengine wanakuja kinyemela kwa njia za panya. Tushirikiane wote kuwaondoa hawa watu wote ambao wanakuja kuchukua kazi ambazo hawastahili. Kazi ambazo zingestahili kufanya na Watanzania. (*Makofsi*)

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya nyongeza aliyotoa Mheshimiwa Waziri, ningeomba kuititia Bunge hili atufahamishe kwamba hivi sasa imedhibitika na wala siyo siri kwamba kuna kazi za kawaida kabisa zinazofanywa na wageni. Kama vile hoteli hata kupika maandazi hata chapati, kuuza maua zinafanywa na wageni. Je, Mheshimiwa Waziri atalizungumziaje suala hilo na hawa watu wanapitia wapi na wanapata vibali gani? (*Makofsi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare kama ifuatavyo:-

Narudia kusema Serikali haiingizi tu kiholela wageni kufanya kazi katika nchi hii ziko taratibu. Kila mtu anayetaka kuingiza wageni katika nafasi ambazo zimeruhusiwa kwa mujibu wa mkataba wake, anatakiwa kutoa matangazo kwanza ndani ya nchi mara tatu ili ithibitike mara ya kwanza asipopata mwombaji mwenye sifa zinazotakiwa arudie mara ya pili na ya tatu. Na vielelezo hivyo vya magazeti na *application* letters za wale walioomba lazima zifkishwe Wizara ya Kazi ili kuhakikisha kwamba kweli amejitahidi na ameshindwa kupata watu wenye sifa.

Ziko baadhi ya hoteli hapa Tanzania kwa sifa za kigeni huwa zinaitwa migahawa *restaurant*. Lakini zina sifa kubwa ni migahawa ambayo *investment* ni kubwa. Wapo watu wanatangaza aina fulani ya wapishi wa aina fulani ya chakula ambacho Watanzania hawakusomea. Ni kweli kwani mimi nimewahi kuona *restaurant* moja wametangaza na walikuja na mifano. Huyo mwenye restaurant anapika chakula cha aina ya Malaysian. Aina ya chakula anachopika yeche ni konono na vyura. Anao wateja wake wanakuja na

meli za kutoka maeneo hayo ya Asia na chakula hicho wanatoa *order* kabla hawajafika Tanzania. Watanzania wameshindwa kabisa kujifunza namna ya kutengeneza chakula cha aina hii. (*Kicheko*)

Sasa huu ni mgahawa na sheria inamtaka *investment* yake iwe zaidi ya dola laki tatu. Amewekeza ndani ya Tanzania zaidi ya dola laki tatu kuanzisha ule migahawa lakini *speciality* yake ni kupika hivyo vyura na Mtanzania hayupo unafanyaje? Nafikiri Watanzania tujifunze zaidi ili tuweze kupata ajira katika sekta mbalimbali. (*Makofî*)

Na. 122

### **Miradi Mingi ya Kitaifa Isiyokamilika**

#### **MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko au maelezo gani juu ya miradi mingi ya kitaifa ambayo imeachwa bila kukamilika chini ya Wizara mbalimbali kama vile ujenzi wa majengo?
- (b) Je, miradi hiyo ni mingapi na ina thamani gani?

#### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, swali lake lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi inaratibu miradi mingi ya ujenzi ikiwa ni pamoja na kuwateua wataalam, kuandaa usanifu, kusimamia na kuhakiki malipo ya ujenzi husika mpaka unapokamilika.

Kwa upande wa majengo, miradi mingi ya Serikali inasimamiwa na kuratibiwa na Wakala wa Majengo kwa kufuata taratibu zote zilizoainishwa katika Sheria ya Manunuzi *Procurement Act No. 3 of 2001*. Utekelezaji na maendeleo ya miradi hii hutegemea upatikanaji wa fedha kwenye Wizara, Idara na Taasisi zenyé miradi husika. Kwa miradi ambayo fedha imetolewa na Serikali kuititia Wizara ya Ujenzi, Wakala unaiendesha kwa ufanisi mkubwa. Aidha, inatuwia vigumu kutoa takwimu sahihi kwa miradi ambayo haikukamilika kwa sababu miradi mingi ya namna hiyo imekuwa ikisimamiwa na kuratibiwa na Wizara, Taasisi au Idara ambazo miradi husika inawahu.

Ili kuinusuru Serikali kutokana na hasara inayotokana na mapungufu kama yaliyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge katika swali lake, Wizara yangu inatoa wito kwa maafisa wa Wizara nyingine ambao fani zao ni tofauti na zile za ujenzi na ambao wanasmamia masuala ya majengo yaliyoko katika Wizara zao waanze sasa kushirikiana na wataalam wa Wizara yangu kuanzia hatua za awali hadi hatua za mwisho za miradi husika. Miradi mingi ya ujenzi inayosimamiwa na Wakala wa Majengo imekamilika na kukabidhiwa kwa watumiaji. Aidha Wizara ya Ujenzi kuititia Wakala wa Majengo, inafanya juhudhi ya kuelimisha Wizara pamoja na Idara zake ili watumike wataalam

waliopo Wizara ya Ujenzi kwa kupata ushauri bora na hatimaye kupata Usimamizi mzuri wa miradi.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(1) Pamoja na majibu yaliyojitokeza ambayo naona yanatoa taarifa ya kutosha. Ningombu tu nifahamu kwamba; kwa vile swali la msingi limezungumzia miradi mbalimbali. Kuna ujenzi wa *control tower* katika uwanja wa ndege Mwanza ambao mradi umekaa muda mrefu sana. Pia kuna ujenzi wa kituo cha polisi Nyakato nao una muda mrefu sana. Wizara inasemaje namna ya kuratibu miradi hiyo?

(2) Kwa vile swali linazungumzia miradi mbalimbali na Wizara mbalimbali kwamba tumekuwa tukipewa ahadi mbalimbali hapa ndani ya Bunge, na hasa ningependa nipate maelezo kwamba sasa katika miradi ya umwagiliaji ambayo iko Mbarika ambayo ni ya muda mrefu sana. Kila siku tunaambiwa kwamba itafanya kazi mpaka leo hatujaona matokeo. Miradi ya Ramadi pia nayo hatuona matokeo. Je, hii Wizara inasemaje? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, kama ifuatavyo:-

Katika jibu langu la awali nilijibu kwamba ipo miradi ambayo inasimamiwa na wizara na Taasisi husika na hiyo miradi haisimamiwi na Wizara ya Ujenzi. Nilisema itakuwa vigumu kutoa takwimu sahihi kwa miradi hiyo ipi imekamilika na ipi bado. Na bahati nzuri ametoa mfano yeche mwenyewe kwa kuuliza swali kwa nini ujenzi wa *Control Tower* Mwanza haujakamilika, Kituo cha Polisi Nyakato? Hii miradi haisimamiwi na Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, hatuwezi kutoa taarifa hii ni miradi ya Serikali inayosimamiwa na Wizara na Idara husika. Kwa hiyo, wao ndiyo wanawenza kutoa taarifa hiyo. Hali kadhalika na miradi ya umwagiliaji, hii inaweza kutolewa taarifa na Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge bado namwomba akubaliane na mimi kwamba ile miradi ambayo Wizara ya Ujenzi inasimamia, ndio Wizara ya Ujenzi inaweza ikatoa takwimu sahihi. (*Makofi*)

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa, Wizara ya Ujenzi sasa imejiingiza kindakindaki katika kujenga nyumba za kuishi. Sasa swali langu ni kwamba je, itatusaidiaje wananchi wanaoishi *Ilala Quarter* katika Kata ya Mchikichini pamoja na *Quarter* za Magomeni katika kuboresha nyumba zile ili nao waishi katika nyumba bora kama vile Serikali inavyokusudia? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Ujenzi haijaingia kindakindaki kwenye kujenga nyumba. Wizara ya Ujenzi inawafikiria jinsi gani wafanyakazi wa Serikali nao wanaweza kuwa na hali bora baada ya kustaafuli. Kwa hiyo, inajitahidi kuwajengea nyumba wafanyakazi wa Serikali. Nyumba nyingine kwa mfano za *Ilala quarter*; na *quarter* zingine zile ziko chini ya *National Housing*. *National Housing* lazima tuseme kweli hapa inajitahidi kweli kujenga nyumba sana zaidi kuliko Wizara ya Ujenzi na kila mahali. Kwa hiyo, mimi nina hakika *National Housing* ina mpango kabambe kabisa juu kuongeza na kubomoa hizi za *Ilala quarters* najua nyingine zilibolewa pale na yakajengwa maghorofa. Najua baadaye wataziboresha hizo nyumba za *Ilala quarter* na *quarter* zingine. Lakini wananchi naomba waelewe kwamba Wizara ya Ujenzi inajitahidi kujenga nyumba kuwasaidia wafanyakazi wa Serikali baada ya kustaafuli kwao wawe na hali nzuri ya maisha. (*Makofii*)

Na. 123

### **Barabara ya Mikumi - Handeni**

#### **MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA aliuliza:-**

Je, ni lini barabara ya kutoka Mikumi - Kilosa - Dumila hadi Handeni, itafanyiwa upembuzi yakinifu na kuanza kutengenezwa?

#### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilitenga jumla ya Shilingi za Kitanzania 202.5 milioni kupitia Bajeti ya mwaka wa fedha 2004/2005 kwa ajili ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu. Zabuni za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hiyo ya upembuzi yakinifu zilitangazwa na Wakala wa Barabara *TANROADS* Mkao wa Morogoro na zitarudishwa tarehe 20 Mei, 2005. Mkataba wa Usanifu unatarajiwa kusainiwa mapema mwezi Julai na kazi ya usanifu itaanza mwezi wa Agosti, 2005 kwa lengo la kukamilishwa mwezi Machi, 2006. Matokeao ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu yataiwezesha Wizara yangu kutenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina na hatimaye ujenzi wa barabara husika kwa kiwango cha lami kuanza kutegemea uwezo wa Serikali.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Serikali ya awamu ya tatu ndiyo yenye jeuri nzuri na nia njema ya kujenga miundombinu ya barabara, barabara za lami hatimaye hata hii barabara ya Kilosa - Mikumi imewekewa Bajeti hiyo.

(1) Je, sasa watafanya hima kwa Bajeti hii inayokuja izungumzwe kabisa kwa sababu usanifu ndio unakuwa mwezi wa nane?

(2) Wanasemaje kuhusu shule zile zilizokuwa karibu na barabara? Maana zinahatarisha kwani ziko karibu na barabara wanawenza wakawatuma watu wa *TANROADS* wakawapimie ili wale waendelee na ujenzi kwenye mashule na zahanati?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christopher Semanini Wegga, kama ifuatavyo:-

Katika jibu langu nilisema wazi kwamba usanifu utaanza mwezi Agosti, na kukamilika mwezi Machi, 2006. Kwa hiyo Kiserikali na kibajeti Bajeti sahihi yakuiwekea pesa barabara hii ni Bajeti ya mwaka 2006/2007. (*Makofî*)

Je, nyumba, zahanati na shule zilizokuwepo barabarani bila ya kufanya usanifu hautajua barabara inaishia wapi, inapitia wapi? Kwa hiyo kuamua sasa hivi *TANROADS* wawapimie wananchi hawa waendelee kujenga mashule, itakuwa ni kuwapotosha. Kwa sababu inawezekana kabisa usanifu ukasema barabara sasa ipite hapa. Na hapo *TANROADS* itakuwa imekwishaidhinisha.

Mimi ninaomba kwa kuwa wamekwishastahimili kwa muda mrefu sana wastahimili kwa muda huu mfupi utakaokuja ili tuwe na usahihi wananchi wanajenga wapi nyumba zao, zahanati na shule tusije tukapata hasara kwa kubomolewa.

Na. 124

### **Matumizi ya Mbolea ya Chumvichumvi na Uzalishaji wa Mbegu ya Mahindi na Mpunga**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA (k.n.y MHE. DR. LAWRENCE GAMA** aliuliza:-

(a) Je, tangu tupate uhuru tumekuwa tukitumia mbolea za chumvichumvi za kupandia na kukuzia kiasi gani kila mwaka kufikia mwaka 2003/2004, na ni nchi gani Kusini mwa jangwa la Sahara inatumia mbolea hizo zaidi?

(b) Je, ni vituo gani vyta utafiti hapa Tanzania vinazalisha mbegu za mahindi na mpunga na kwa kiasi gani na je, zinazotosheleza mahitaji ya Tanzania?

### **WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba niunganishe vipindi hivi badala ya kujibu kila mwaka maana itakuwa refu sana.

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka wa 1961 na 1970 nchi ilitumia wastani wa tani 30,000 tu za mbolea. Na hii ilitumiwa zaidi na wakulima wakubwa siyo wakulima wadogo wadogo. Kati ya mwaka 1971 na 1981 tulitumia kiasi cha tani 87,000. Ongezeko kubwa la matumizi ya mbolea lilitokana na kuanzishwa kwa kiwanda cha mbolea cha Tanga katika mwaka 1972 ambacho kilikuwa na uwezo wa kuzalisha tani 105,000 za mbolea kwa mwaka. Ililitokana pia na uhimizaji wa matumizi ya mbolea uliyofanywa na chama na Serikali kupitia kwenye miradi kama Azimio la Mlale lililokuwa kule Mkoani Ruvuma.

Kati ya mwaka wa 1982 na 1992, matumizi ya mbolea yaliongezeka kufikia tani 111,575.8 na Ongezeko hili lilitokana na Serikali kutoa ruzuku kwa mbolea. Kati ya mwaka wa 1993 na 2002/2003, matumizi ya mbolea yalishuka hadi tani 82,408 na kushuka huku kulitokana na kuondolewa kwa ruzuku kwenye.

Kati ya mwaka wa 2003/2004 tulipata tena ongezeko la matumizi ya mbolea kufikia tani 92,568 na ongezeko hili lilitokana na Serikali kurudishwa kwa ruzuku kwenye mbolea.

Mheshimiwa Spika, tumatumia mbolea kidogo sana kwa hekta kiasi cha kilo 6 - 7 za virutubisho kwa hekta, ikilinganishwa na wastani wa kilo 21 kwa nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara na 51 kwa Afrika ya Kusini ambayo ndio inaongoza katika eneo hili kwa matumizi makubwa ya mbolea.

(b) Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mbegu unafanywa katika hatua kuu tatu.

(1) Hatua ya kwanza ni ile ya kuzalisha mbegu mama ama inajulikana kama mbegu ile ilizalishwa na watafiti.

(2) Ni kupeleka mbegu hii kwenye mashamba ya uzalishaji ili kuzalisha mbegu ya msingi.

(3) Ni kuizalisha hii mbegu ya msingi kwa wingi ili kupata *certified seed*.

Sasa ili kutokana na utaratibu huo, Vituo vya utafiti vinavyozalisha mbegu ya mahindi ni Ilonga, Seliani na Uyole. Uyole huzalisha pia mbegu chotara na mbegu ya mtama uzalishwa KATRIN na Dakawa.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya Taifa ya mbegu ni makubwa ni tani 9,000 za mahindi na 7,000 za mpunga. Na uzalishaji wetu ni mdogo ni tani 182 za mbegu ya mahindi na tani 168.5 za mbegu ya mtama. Pengo linalotokea linajazwa na uagizaji wa mbegu kutoka nje na matumizi ya mbegu za wakulima wenyewe. Serikali sasa hivi iko mbioni kukamilisha maandalizi wa wakala wa mbegu atakayechukua nafasi ya *tan* seeds ili kuhakikisha kwamba mbegu za kutosha zinazalishwa kukidhi mahitaji ya wakulima.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuwa, tathmini ya udongo yaani *soil analysis* ni huduma ya msingi kabisa katika kuboresha kilimo chetu. Na kwa kuwa huduma hii ilikuwa inatolewa siku za nyuma na sasa hivi haipo katika maeneo mengine hasa Mkao wa Ruvuma. Je, Serikali itakuwa tayari kufufua huduma ya msingi kwa lengo la kuepuka matumizi mabaya ya mbolea?
- (b) Wakati wa utawala wa kikoloni na kufikia hadi miaka ya sabini palikuwepo kituo cha kuzalisha mbegu ya mahindi aina ya *Songea Selected*. Je, Serikali itakuwa tayari kufufua kituo hiki ili kuweza kuongeza uzalishaji wa mbolea hapo badala ya kutegemea kuagiza kutoka nje?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ngwatura kama ifuatavyo:-

Kwanza huu utaratibu wa soil *analysis* unaendelea na kituo chetu cha Ilonga ndicho kinachofanya kazi hii ya kufanya uchunguzi wa udongo na kuonyesha nini kilichopo katika udongo huo na kupendekeza matumizi ya mbolea. Kwa hiyo, ni kazi inayoendelea na wala hajawahi kusimama. Katika baadhi ya mikoa kwa mfano; Mkao wa Iringa, hii wakati ule ilikuwa inaitwa *ECC* sasa *European Union* walifanya uchambuzi wa Mkao wote eneo kwa eneo na kuna makapu makubwa kabisa yanayoonesha hali ya udongo kila mahali katika Mkao ule. Ilifanyika vile vile kwa hii *Uhuru Corridor*. Lakini hayo matabu yamefungiwa *store* hakuna mtu anayeyasoma. Naomba sana tafadhali mkayachukue hayo matabu myasome maana yataonyesha ni nini tunachoweza kufanya na udongo. Tulikuwa na mbegu nzuri sana ya Songea ilikuwa inaitwa *Songea Selected*. Lakini mbegu hii ilishikwa na ugonjwa wa ukungu kiasi kwamba haingeweza tena kulimwa. Kituo chetu cha Uyole kimezalisha mbegu nyingine badala ya *Songea Selected* ambayo ina sifa bora kuliko *Songea Selected*. Na ninaomba kule Ruvuma mtumie mbegu hii badala ya ile ya kwenu ya zamani ambayo sasa hivi haifai.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni vitabu siyo matabu. (*Kicheko*)

**MHE. HALIMENSHI K.R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu lake la msingi, kuna tatizo moja kubwa ambalo mwaka jana tulipitisha Bajeti kwa nchi nzima kuweza kupata mbolea ya ruzuku. Sasa hii mbolea mpaka sasa katika baadhi ya Mikoa ukizingatia na Mkao wa Kigoma ambao unahitaji mbolea hiyo kwa wingi hata wale mawakala hawana fununu licha ya kuwa wana hela za kutosha kuweza kupata mbolea hiyo ya ruzuku. Sasa kama sisi tunahitaji kuanzia mwezi wa Tano, mvua ni mwezi wa Saba na wa Nane na kuendelea. Je, mbolea hiyo inafika wakati gani au hatumo kabisa? Tupate jibu hata sisi.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeamua kwamba mbolea ya ruzuku itasambazwa nchi nzima na Mkoa wa Kigoma ni mmoja wa Mkoa ambayo unapewa umuhimu wa juu kabisa. Kwa sababu kila mwaka wanapata mvua za kutosha. Sasa kama hii mbolea hajafika ya kutosha na Mheshimiwa Mayonga alishaniona juu ya suala hili, nitakwenda kufuatilia kuhakikisha kwamba inafika. Naomba tu viongozi wa Mkoa wahakikishe kwamba wanasimamia usambazaji wa mbolea hiyo vizuri ili ifike wa wakulima kama inayokusudiwa. Hii mbolea inasambazwa sasa kwa hiyo itawahi msimu wako unaoanza sasa na kuendelea. Ahsante.

#### Na. 125

#### **Kupanda kwa Bei ya *Sulphur* na *Bayfidan***

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na upungufu mkubwa wa dawa ya *sulphur* na *Bayfidan* kwa wakulima wa zao la korosho wa Mikoa ya Lindi na Mtwara; na kwa kuwa upungufu huo umesababisha bei ya pembejeo hizo kupanda hasa *sulphur* hadi kufikia zaidi ya shilingi 20,000 kwa mfuko wa kilo 25 badala ya bei ya kawaida ya shilingi 9,000/= na shilingi 10,000/= na kwa kuwa; wakulima wengi wa korosho wakiwemo wa Wilaya ya Liwale hawawezi kumudu bei hizo.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza makali ya bei za pembejeo hizo kwa wakulima wa korosho nchini?
- (b) Je, ni kampuni ngapi na za akina nani zimepewa kibali cha kuagiza pembejeo hizo na kwa kiasi gani?
- (c) Je, dawa hizo yaani *sulphur* na *Bayfidan* zina madhara gani kwa wakulima wa zao la korosho?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Kuanzia mwezi wa Mei, 2005 Serikali itaanza kutoa ruzuku kwa baadhi ya madawa ya kupulizia korosho, hususan yale yasiyokuwa na madhara makubwa kwa mazingira. Chini ya mpango huu, Serikali itafidia gharama za kusafirisha madawa hayo kwa asilimia 100 hadi kwenye vituo vikuu vya kupokelea madawa hayo ambayo ni Dar es Salaam, Lindi, Tunduru, Mtwara na Tanga. Aidha, Serikali itafidia asilimia 50 ya madawa hayo.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya mpango huu, Serikali itafuatilia kwa karibu uagizaji na usambazaji wa madawa ya korosho ili kuhakikisha kwamba yanapatikana

kwa wingi na kwa kutoa ruzuku kuhakikisha kwamba mkulima anayapata kwa bei nafuu.

(b) Biashara ya dawa za korosho inafanywa na sekta ya watu binafsi. Serikali haitoi vibali, wala haipangi kiasi cha madawa kitakachoagizwa. Wafanyabiashara huagiza madawa kulingana na uwezo wao wa kifedha na kwa kuzingatia mahitaji ya aina ya dawa inayohusika katika soko. Hata hivyo, Serikali inasimamia ubora wa madawa na pembejeo nyingine za kilimo zinazoingizwa humu nchini.

Mheshimiwa Spika, Makampuni yanayoagiza madawa ya korosho ni *Abbas Export, Mukpar, Bytrade, Twiga Chemicals* na *Syngenta*. Hadi Aprili, 2005, Makampuni hayo kwa pamoja yalikuwa yameagiza nchini tani 2,700 za *sulphur* na lita 4,800 za *Bayfidan*

(c) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa madawa ya *Sulphur* na *Bayfidan* hayajathibitika kuwa na madhara kwa wakulima wa korosho. Madawa haya yanaweza tu kuwa na madhara kama yaktumiwa vibaya kwa kuwa madawa yote hasa ya kilimo ni sumu.

Uchunguzi uliofanywa na watafiti wa udongo unaonyesha kwamba *sulphur* inaongeza tindikali kwenye udongo inapokuwa imedondoka kwenye udogo kwa wingi. Kwa hiyo, *Bayfidan* haina matatizo hayo. Kwa hiyo, tunapendekeza kutumiwa zaidi kwa madawa yasiyokuwa na madhara kwa mazingira na madawa hayo ndiyo yatakayopewa ruzuku.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kujuu Serikali imechukua hatua gani kuwasaidia wakulima wa korosho hasa wa eneo la Liwale ambako mimi ndio Mbunge wao kuona matatizo yaliyojitokeza mwaka jana ya majani ya korosho kuwa mekundu hatimaye kukauka, imetatuliwa namna gani.

Pili pia kutokana na bei kubwa kwa mwaka jana ya pembejeo hiyo wananchi au baadhi ya wakulima waliamua kutumia ngao kwa ajili ya kuua mbu, Serikali inatamko gani kuhusu matumizi hayo.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, hili la majani kubadilika rangi na kuwa mekundu nalisikia mara ya kwanza, tutaagiza kituo chetu cha Naliendele kilifanyie utafiti na tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi kuweza kutoa maelezo sahihi hapa Bungeni baada ya utafiti huo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana ni kweli bei za madawa ya kupulizia korosho zilipanda sana na ilitokana na ukweli kwamba kulikuwepo dawa kidogo sana nchi na aliyekuwa nayo ni msambazaji mmoja kwa hiyo akachukua nafasi ile akapandisha sana bei ya madawa. Kutokana na matatizo ya mwaka jana Serikali imefuatilia kwa karibu sana uingizaji wa madawa nchi mwaka huu na tunatarajia kwamba yatakuwepo madawa

ya kutosha na hakutakuwepo sababu ya kutumia ngao badala ya madawa haya hiyo ngao endeleeni kutumia kuwafukuza mbu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona wakulima wa korosho wote wamesimama, sasa wakulima wa korosho Mkoa wa Pwani Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, wakulima wa korosho Mkoa wa Mtwara Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu la msingi alieleza vituo ambavyo vitapelekwa hizi dawa za kupulizia korosho. Lakini hakutaja mkoa wa Pwani amba ni wakulima, kataja Dar es Salaam tu hakutaja Pwani.

Je, Mkoa wa Pwani haistahili na yeze kuwa na kituo chake.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani upo karibu sana na Dar es Salaam, na wakati mmoja Dar es Salaam ndio ilikuwa makao makuu ya eneo lote lile ikiitwa *Eastern Province* na madawa haya yanaingilia Dar es Salaam kwa hiyo naomba mkoa wa Pwani tuchukulie pale Dar es Salaam. Kwa sababu hakuna eneo lolote ambalo tunaweza kuweka kituo Pwani kikawa karibu na wananchi kuliko Dar es Salaam.

Kwa hiyo, naomba mkoa wa Pwani na Mkoa wa Dar es Salaam waendelee kushirikiana kama walivoyozoea na dawa wachukulie Dar es Salaam.

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametamka kwamba kuna ruzuku ya asilimia 50 ya *Sulphur* na wewe Mheshimiwa Spika ni shahidi hapa, amesema hapa hapa. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa tamko gani kwa wakulima wa korosho kufaidika na ruzuku hii ya kupungua kwa bei ya *sulphur* mwaka huu? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri rafiki yangu Mheshimiwa Namkulala hakunisikia vizuri. Tumesema Serikali itafidia gharama za usafirishaji kwa asilimia 100, itafidia asilimia 50 ya bei kwa madawa yale ambayo hayana madhara makubwa kwa mazingira. Kwa bahati mbaya sana *sulphur* ina madhara makubwa kwa mazingira, kwa sababu inaongezeka tindikali kwenye udogo. Sasa naomba tukubaliane na utaratibu huo.

Na. 126

#### **Kusomesha Watoto Yatima na Wale Ambao Wazazi Hawana Uwezo**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kuwasomesha kwa kiwango cha elimu ya Sekondari Watoto yatima au wale ambao

wazazi wao hawakuwa na uwezo na Wilaya ya Muheza ilipata nafasi 47 na kwa kuwa, elimu ya Sekondari ni miaka 4 mpaka miaka 6 kwa watakaoishia kidato cha sita:-

- (a) Je, Serikali imepanga mkakati gani wa kuendelea kuwalipia wanafunzi hao kwa muda wote wa miaka minne hadi sita?
- (b) Je, wale wanafunzi 47 wa Wilaya ya Muheza waliolipiwa mwaka uliopita wameshalipiwa ada na mahitaji yao kwa mwaka huu wa pili, 2004/2005?
- (c) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kupitisha fedha za wanafunzi hao katika mifuko ya Elimu ya Wilaya hiyo ili kuwezesha usimamizi wa karibu?

#### **WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mkakati wa kugharimia elimu ya wanafunzi hao hadi watakapohitimu kidato cha nne na cha sita kwa wale watakaoendelea hadi kidato cha sita. Hivi sasa kuna jumla ya wanafunzi wa aina hiyo 23,587 ambaa wako kwenye shule za sekondari za Serikali katika vidato vya kwanza hadi cha tatu. Kati ya hao 12,000 ni wa kidato cha kwanza ambaa fedha zao zimelipwa kutokana na MMES na 11,587 wa kidato cha pili na kidato cha tatu, ambaa fedha zao zimetengwa kwenye fungu la Bajeti ya Wizara.
- (b) Wilaya ya Muheza inao wanafunzi 109 wa kidato cha kwanza, 61 cha pili na 47 wa kidato cha tatu, ambaa jumla yao ni 217. Wanafunzi hao wote wamekwisha kulipiwa kwa mwaka huu wa 2004/2005.
- (c) Mheshimiwa Spika, hadi sasa fedha hizi hulipwa kwenye akaunti za shule husika na Wakuu wa shule wanawajibika kuona kuwa watoto hao wanapewa huduma zinazostahili. Utaratibu wa kupitisha fedha kwenye akaunti za shule, unatumika pia katika kupeleka fedha kwenye shule hizo kwa ajili ya uendeshaji wa shule na shughuli nyinginezo. Wizara yangu tangu utaratibu huo uanzze kutumika haijapata taarifa ya matatizo makubwa ya usimamiaji wa fedha zinzaotumwa kwenye shule moja kwa moja, ambayo yanalazimisha kuchukua hatua za kutuma fedha kwa kuhusisha Mfuko wa Elimu wa Wilaya kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoatoa, lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza kwa kuwa sasa ada katika shule za Sekondari za Serikali imepungua. Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa ipo haja ya kuongeza idadi ya wanafunzi kwa kutumia kiwango kile kile kilichokuwa kimapagwa?

Pili, je, Serikali ina mpango gani sasa wakuwafikiria watoto yatima ambao wamekutwa na uyatima wao wakiwa wanasoma katika Taasisi mbalimbali za dini na au katika shule zisizokuwa za Serikali ili nao waweze kulipiwa ada?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kwa kuwa ada imepungua je, tunaweza kuongeza idadi ya wanafunzi. Jibu ni kwamba inawezakana kwa sababu tunatumia ile Bajeti kama tulivyopewa, na kama bajeti itaruhusu tuweze kuwalipia wanafunzi wengi zaidi hatutasita kufanya hivyo.

La pili kuhusu watoto yatima ambao wanasoma katika Taasisi mbalimbali ama shule ambazo sio za Serikali. Kusema kweli utaratibu wa sasa chanzo chake ni wale waliofaulu mtihani wa darasa la saba kwenda sekondari. Hicho ndio chanzo tunataka kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatumika kuwalipia wanafunzi ambao kweli watapata manufaa, baadhi ya wanafunzi walio katika shule ambazo sio za Serikali huwa ni wanafunzi ambao hawakufaulu ule mtihani wa darasa la saba na tunakuwa na mashaka juu ya uwezo wao. Huu ndio utaratibu tunaoutumia kwa hivi sasa endapo hapo baadaye tunaona kuna haja ya kubadili, lazima uamuzi huu uendane na uamuzi wa kuhakikisha kwamba wanafunzi hao wanaokwenda katika shule hizo ni wale waliofaulu mtihani wa darasa la saba na sio vinginevyo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa huduma hii ya kusomesha wanafunzi yatima ama wazazi wasio kuwa na uwezo imegawanyika katika makundi mawili, yaani wanafunzi wanaosomeshwa na Serikali na wanafunzi wanaosomeshwa na Halmashauri za miji wilaya ama Manispaa na kwa kuwa kuna Halmashauri ambazo zina uwezo mdogo kipesa na kufanya wanafunzi wanaosomeshwa na Halmashauri kutopata huduma zinazostahili.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hili ili wanafunzi wote walingane kwa huduma zinazostahili.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli kwamba mgawanyiko huo upo kwamba wako wanafunzi ambao wanaosomeshwa wanafunzi wanatoka familia zisizo na uwezo. Wapo wanaosomeshwa kwa ruzuku ya kutoka Serikali Kuu na wako wanaosomeshwa kwa ruzuku kutoka kwenye Halmashauri na ni kweli. Kwa hiyo, kama Halmashauri haina uwezo mkubwa itashindwa kutekeleza jukumu hilo kulinganisha na zile Halmashauri zilizo na uwezo mkubwa.

Lakini jambo hili ni ufundi wa kuandaa Bajeti, kwa sababu kila Halmashauri ikishaanda Bajeti yake yale maeneo ambayo inapungukiwa, inaruhusiwa kuomba ruzuku na kujenga hoja ya Halmashauri yenyewe kupewa ruzuku kutoka Serikali kuu. Kwa hiyo, zile Halmashauri ambazo wanajikuta hawana uwezo, lakini wanalo tatizo kubwa la watoto wanao toka familia zisizo na uwezo wa kifedha, basi ni wajibu wao kuhakikisha wanaomba ruzuku wanajenga hoja na kuomba ruzuku ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo kutoka Serikali Kuu.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimwa Spika, ahsante sana kwa kuniona lakini swali langu limeshajibiwa katika sehemu ya pili ya jibu la Mheshimiwa Waziri.

**SPIKA:** Ni vizuri sana kwa hiyo tunaendelea na maswali yanayofuata.

Na. 127

### **Tatizo la Walimu na Umeme - Sekondari ya Mipa**

**MHE. PAUL MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa shule ya Sekondari ya Mipa iliyokoa katika Kata ya Seke-Bugoro Tarafa ya Mondo ina tatizo la upungufu wa walimu na upatikanaji wa umeme:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua matatizo hayo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua tatizo la shule ya sekondari ya Mipa iliyoko Kata ya Seke-Bugoro, Tarafa ya Mondo Wilayani Kishapu. Shule hiyo ina walimu saba badala ya walimu 12 wanaohitajika. Kwa hiyo inao upungufu wa walimu wanne wa Masomo ya Hisabati, Fizikia, Biolojia na Kemia. Katika mwaka wa 2004/2005 Serikali imepanga kuajiri walimu wapya 1,500. Pengo la walimu lililopo katika shule hiyo inatarajiwa kupungua baada ya zoezi la kuajiri walimu hao litakapo kamilika. Aidha MMES 2004-2009 tunalo lengo la kuhakikisha kuwa shule zote za Sekondari nchini zina kuwa na walimu wa kutosha ifikapo 2009, kwa sababu mpango una *component* maalum ya mafunzo ya walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la umeme, kwa kuwa shule hiyo iko mbali na uliko umeme wa *Grid* ya Taifa, ufumbuzi wa tatizo hili ni ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya, Shirika la *TANESCO* na Serikali. Kwa vile ni tatizo linalohitaji fedha nyingi, litaendelea kupatiwa ufumbuzi kwa kadri uwezo utakavyokuwepo, ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kupata vyanzo vingine vya umeme kama vile kutumia nguvu za juu, hasa kwa shule za vijijini zikiwemo za Wilaya ya Kishapu.

**MHE. PAUL N. MAKOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini katika maelezo yake amesema kwamba uwezekano wa kupeleka umeme katika eneo hili ni gharama kubwa kwa sababu ya umbali wenyewe. Lakini akajaribu kusaidia kueleza kwamba pangeliwezekana vile vite kupelekwa umeme wa *Solar*.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akasaidiaje kupeleka umeme wa *solar* katika eneo hili la shule ili tatizo la umeme liweze kuondoka katika shule hii na liweze kutoa msaada mkubwa kwa wanafunzi, anaweza akasaidiaje?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nitasaidiaje kupeleka umeme wa *Solar*, hili namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane tu kutafuta ufumbuzi hapa nilipo sina majibu ya kujua ni gharama zifi tunaweza kuzitumia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Makolo tushirikiane tutafute ushauri wa kitaalam itagharimu kiasi gani na endapo tutaona inawezakana kuingiza katika Bajeti basi tutachukua hatua inayohitajika.

**SPIKA:** Kwa kuwa Serikali ni moja namwomba Naibu Waziri wa Nishati na Madini, asaidie kujibu hilo.

**NAIBU WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni naomba niongeze tu kwenye majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumepitisha Muswada hapa wa Umeme, Taasisi ya Umeme Vijijini na mfuko wa umeme vijijini, na moja ya madhumuni makuu ya mfuko ule ni kufanya umeme iwe ni sekta mtambuka katika maeneo ya elimu, mawasiliano katika kukuza uchumi, biashara na kadhalika na maeneo ya shule moja wapo ambayo yatapewa kipao mbele katika mradi ule.

Lakini pia napenda niunge na Mheshimiwa Waziri wa Elimu alivyosema kwamba, pengine la kufanya hapa ni kutafuta wakati tunasubiri utaratibu huo. Ni kutafuta miradi ambayo vyazo vyake ni vingine, Mheshimiwa Waziri pale ametaja umeme wa juu kama alivyotaja Mheshimiwa Makolo lakini pia kuna uzalishaji wa umeme wa kutumia *biogas* na kule kwa Mheshimiwa Makolo, hii *biogas* ipo nyingi. Kwa hiyo, nadhani tukishirikiana kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Elimu tunaweza tukapata ufumbuzi wa haraka zaidi, *biogas* ya wanyama na pia hata ya binadamu ipo nyingi.

Na. 128

### **Kushuka kwa Thamani ya Shilingi Kunavyomnufaisha Mkulima**

**MHE. DR. ZAINAB AMIR GAMA** aliuliza:-

Kuna msemo usemao kuwa kushuka kwa thamani ya shilingi kunamnufaisha mkulima.

Kama msemo huo ni kweli. Je, mkulima huyo ananufaikaje na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania maana yake ni kuongezeka kwa kiwango cha shilingi ya Tanzania kinachohitajika kubadilisha au kununua kiasi hicho hicho cha fedha za kigeni. Kwa mfano thamani ya shilingi inakuwa imeshuka iwapo Dola moja ya Marekani iliyokuwa inanunuliwa kwa shilingi 1,000, sasa itanunuliwa kwa zaidi ya hiyo shilingi 1,000. Sababu zinazosababisha kushuka kwa thamani ya shilingi ni uhaba wa dola unaotokana na uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nchi za nje ambao ni mkubwa zaidi kuliko mauzo yetu ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa thamani ya shilingi kunamnufaisha mkulima kwa njia zifuatazo:-

(i) Kama mkulima, mathalani, alikuwa anapata sh. 1,000 kwa kilo moja ya kahawa, baada ya kushuka kwa thamani ya shilingi tuseme kwa asilimia 10% atapata shs.1,100 kwa kilo endapo bei ya zao hilo itaendelea kuwa dola moja kwa kilo.

(ii) Soko la mazao ya kilimo nchi za nje litapanuka, kufuatana na mazao hayo kukabili ushindani wa bei katika soko la dunia; kwani mfanyakishara nchi za nje aliyekuwa akiagiza bidhaa kutoka Tanzania zenye thamani ya sh. 1,000 sawa na dola moja, sasa atawezu kuagiza bidhaa zile zile kwa asilimi 10% pungufu ya dola moja.

(iii) Soko la ndani la bidhaa za biashara yaani litapanuka vilevile, kwani gharama za uagizaji wa bidhaa kama hizo kutoka nje zitaongezeka. Kwa mfano, mwagizaji aliyekuwa akitumia shilingi 1,000 kupata dola moja ya kuagiza bidhaa nchi za nje, sasa itambidi kutoa shilingi 1,100 kuipata hiyo dola. Hivyo atashawishika kununua bidhaa kama hiyo izalishwayo nchini.

(iv) Kwa mkulima ambaye hapo awali alilenga kuuza kwenye soko la ndani, atashawishika kuanza kuzalisha kwa ajili ya soko la nje ili kuongeza pato lake. Hali hiyo ikitokea, mauzo ya taifa nchi za nje yataongezeka; ununuzi nchi za nje utapungua, na ununzi wa bidhaa zetu wenyewe utaongezeka. Mkulima atafaidika zaidi akizalisha zaidi kwa kuuza nje zaidi.

(v) Pato la mkulima kutockana na kupungua kwa thamani ya shilingi litaongezeka hata kama bei na gharama kwa mkulima ya mali ghafi na pembejeo itaongezeka, kwa sababu gharama ya vitu hivyo ni sehemu ndogo katika jumla ya gharama za uzalishaji. Gharama kubwa zaidi ni juhudhi ya mkulima mwenyewe.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Waziri kwa kunijibu kitaalam. Nina swalii moja la nyongeza, kwa kuwa *raw material* nyingi mbole, kutengeneza majembe *raw material* zinatoka nje au vitu vinatoka nje kwa kununua kwa bei ya dola, *tractor* kwa bei ya dola. Sasa hivi mafuta yamepanda bei na kusababisha mkulima alime kwa tractor zaidi, kwa pesa zaidi kuliko mwazo kwa sababu dola imepanda na wakati mazao yanapozidi kuwa mengi mkulima mazao yake huwa yanapungua bei.

**SPIKA:** sasa swalii.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Je, Waziri haoni ndio maana miaka hadi mwaka mkulima anakuwa maskini anafikia hatua hata hawezu kujimudu yeye na watoto wake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye lakini narudia tena *point* yangu ya namba tano nimesema hivi pato la mkulima kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi itaongezeka hata kama bei na gharama kwa mkulima ya malighafi na pembejeo itaongezeka kwa sababu gharama ya vitu hivyo ni sehemu katika jumla ya gharama ya uzalishaji. Gharama kubwa zaidi ni juhudhi ya mkulima mwenyewe.

Na. 129

#### **Mkataba wa *The East African Customs Union***

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na inategemea kuridhia mkataba wa *East African Customs Union* na kwa kuwa wafanyabiashara wadogo wadogo mpakani katika Wilaya ya Mwanga bado wanansumbuliwa sana na vyombo vya dola kwa kudaiwa malipo mbalimbali bila kupewa risiti:-

- (a) Je, wafanyabiashara wadogo wadogo mpakani wanawajibika kulipa kwa nani na kiasi gani kama wanapeleka kuuza Kenya mazao ya kilimo ya thamani isiyozidi shilingi 50,000/= au wanapoingiza nchini kutoka Kenya bidhaa za kawaada yaani *Consumer Goods* zisizozidi shilingi 50,000/=?
- (b) Je, ni lini Serikali itawaelimisha watendaji wake wa wilaya za mpakani kuwa biashara ya mipakani sio ulangazi bali ni nyenzo muhimu ya kuondoa umaskini?
- (c) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa Watanzania wa mipakani wanafaidika na soko la Kenya na Uganda kwa kuwaondolea vikwazo vya ndani?

## **NAIBU WAZIRI WA FEDHA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliridhia mkataba wa *East African Customs Union* mwezi Desemba, 2004 na kuanza kutumika rasmi mwezi Januari, 2005. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki sasa zinatoza na kutumia viwango sawa vya ushuru kwa bidhaa zinazoingia kutoka nje.

Kwa bidhaa za ndani ya Afrika Mashariki, bidhaa kutoka Kenya zinatozwa ushuru usiozidi asilimia tano mwaka huu, nne mwakani na kuendelea kupunguka kwa asilimia moja moja hadi sifuri baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, bidhaa kutoka Tanzania kwenda Kenya hazitozwi ushuru wowote kuanzia Januari mwaka huu 2005, bali ni lazima ziwe na leseni ya kuzisafirisha ni *export licence* inayotolewa na Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, lenye sehemu (a), (b), na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bidhaa ndogo ndogo zinazouzwa au kununuliwa na wananchi wa mipakani kwenye masoko ya kienyeji ya mipakani hazitozwi ushuru wowote, kwa mujibu wa hotuba yangu Bungeni ya mwaka 2002/2003 na kwa mwenendo wa sasa wa umoja wa forodha katika Afrika Mashariki.

Watu hawa, wakiwemo wakulima wanaobadilishana vyakula kwenye masoko ya pande zote mbili, wana uhuru wa kufanya hivyo na wasibugudhiwe na mtu yejote kwa madai yoyote isipokuwa kama kuna tuhuma za wizi kwa msako wa polisi. Mazao ya biashara ya kilimo, kama vile kahawa, ndiyo yanayo takiwa kufuata taratibu za kisheria za zao husika. Serikali kuitia Wizara ya Viwanda na Biashara, inaandaa utaratibu wa kuwawezesha wasafirishaji wakubwa wanaotumia malori, gari moshi, ndege au meli kupata leseni husika kwa urahisi na huko huko Mikoani.

Natoa onyo kwa watendaji wa Mikoani, Wilayani na Tarafa, Kata na Vijiji kote nchini, wakiwemo mgambo wa vijijini, wasiwanyanyase wananchi wanapo badilishana bidhaa ndogo kwa msingi wa ujirani mwema na kwa kujipatia riziki zao.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake nzuri, lakini kwa kuwa vyombo vyetu vya dola vimetapaka nchi nzima na kwa yakini vinawasumbua sana wafanyabiashara wadogo wadogo wanaochukua bidhaa za kilimo na bidhaa zingine

ndogo ndogo kutoka Tanzania kwenda kwenye magilio nchini Kenya, na wanao nunua vikanga vidogo vidogo na vitu vidogo vya matumizi ya nyumbani kuleta na wanawatoza fedha bila hata kuwapa stakabadhi ya Serikali.

Je, Serikali ipo tayari kutoa tamko kupiga marufuku vyombo vyote vya dola vinavyokaa mipakani na kuwatoza wananchi fedha bila kutoa stakabadhi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, si sheria kuwatoza fedha wananchi wakiwa wafanyabiashara, wakulima bila ya stakabadhi, ni kosa. Serikali italichukulia hatua jambo hilo. Itaangalia kwa undani aina gani ya biashara ambayo haina ushuru lakini pale inapolazimika kuna biashara zina ushuru na inategemea itatokea wapi. Tumesema hapa inayotokea Kenya kwa sasa tuko kwenye 5% mwisho itakuwa sifuri sisi kinachokwenda kule hakuna kitu. Kama wanafuata utaratibu, kwa mujibu wa makubaliano yetu ya *East African Common Custom Union* hakutakuwa na tatizo na hilo la kutoza ushuru bila stakabadhi ni kosa na tutajaribu kama tuwezavyo tulikomeshe.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Kabla hatujaendelea, ningewarudisha nyuma kidogo, katika *Order Paper* ya leo kulikuwa na taarifa za kuwasilisha mezani na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi hakuwahi kuiwasilisha na makusudio yetu ni kwamba taarifa hizi za Kamati zikishawasilishwa mezani zinafanyiwa kazi na Serikali moja kwa moja. Kwa hiyo, ili na hii nayo iweze kufanyiwa kazi na Serikali, ningemwomba Mwenyekiti sasa aiwasilishe mezani.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Kamati ya Ardhi na Kilimo ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**SPIKA:** Sasa tunaendelea na matangazo ya leo kwanza ni vikao vya Kamati. Kikao cha Kamati ya Hesabu za Serikali, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Profesa David Mwakyusa, anaomba wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*) wakutane leo tarehe 29 Aprili, 2005 saa tano asubuhi kwenye chumba Na. 231.

Kikao kingine kimeitishwa na Katibu Msaidizi, Kamati ya Wabunge Wanawake wa CCM, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote wa CCM wahudhurie kikao kifupi kesho Jumamosi tarehe 30 Aprili, 2005 mara baada ya semina itakayofanyika hapa ndani ya ukumbi wa Bunge na kikao kitafanyika hapa hapa ndani ya ukumbi wa Bunge. (*Makofî*)

Mwisho wa matangazo, ziko taarifa chache nyingine. Kulilizwa swali wakati wa mkutano huu kuhusu Taarifa ya Mheshimiwa Kwaangw' iliyoangalia madai mbalimbali

ya Walimu na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tuliahidi kwamba Waheshimiwa Wabunge mtapewa nakala za taarifa hiyo. Sasa imeshawasilishwa kwa Katibu wa Bunge na Katibu wa Bunge ameziweka nakala za taarifa hii katika visanduku vya barua za Wabunge kule tunakochukulia barua zetu za kawaida kwenye *pigeon hale*.

Taarifa nyingine ni kwamba ratiba ya leo tutamaliza majadiliano ya jumla saa saba na saa kumi na moja kamili Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa hotuba ya kufunga rasmi Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge hili.

Tumeshagawa ratiba ya shughuli zetu za mkutano ujao tukianza na Kamati za Kudumu za Bunge. Baada ya kuona kwamba uelewa wa Waheshimiwa Wabunge unapatikana kutokana na semina tunazowapangia sasa tumepanga kwamba kabla Kamati hazijakaa kujadili Bajeti ijayo, kutakuwa na semina ya Wabunge wote kuelewa maudhui ya Bajeti na misingi iliyotumika katika kuiandaa. Ratiba inasema Kamati zitaanza kazi Dar es Salaam tarehe 23/5/2005, Jumatatu ndio siku ya kwanza ya Kamati. Tutaachia hiyo siku ya kwanza Waheshimiwa Wabunge wajipange vizuri kwenye Kamati zao lakini siku inayofuata tarehe 24/5/2005 ndio itakuwa semina ya Waheshimiwa Wabunge wote kuhusu Bajeti kule kule Dar es Salaam, twende tukijua hivyo.

Napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho tuna tafrija ya kumuaga aliyekuwa Katibu wa Bunge hili, Mheshimiwa Kipenka Msemembo Mussa, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kituo chake cha kazi sasa ni Arusha, lakini tumeshampelekea usafiri wa gari ili aje tuweze kumuaga rasmi kesho katika taratibu zetu za kawaida. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, kadi zitakuwa kwenye *pigeon hall* lakini Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa katika halfa ya kumuaga aliyekuwa Katibu wetu wa Bunge na kumkaribisha Katibu wetu wa sasa wa Bunge, katika viwanja vyetu vya burudani. Ni kesho, Jumamosi tarehe 29 Aprili, 2005 saa moja jioni.

Katika mstari huo huo wa kuaga wafanyakazi wetu wa Bunge, kuna mfanyakazi mwingine ambaye hatutamfanya tafrija ya kuaga kwa sababu ya ngazi yake ya utumishi, lakini ningependa nimfanyie kitendo kidogo cha kumuaga rasmi hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Namwita Ndugu Abdallah Gora, *Sergeant Art-arms*, uje mbele hapa usimame uwaangalie Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

(*Hapa Ndugu Abdallah Gora, alifika na Kusimama Mbele ya Waheshimiwa Wabunge*)

**SPIKA:** Ndugu Abdallah Gora ametufanya kazi nzuri sana, ndani ya ukumbi huu kwa kuongoza misafara ya Spika kuingia na kutoka Bungeni na sasa amefikia umri wa kisheria wa kustaafu.....

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah, aongezewe muda.

**SPIKA:** Kwa hiyo, *gwaride...*

**WABUNGE FULANI:** Aongezewe muda, kwa mkataba ... (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Spika amesikia, tutalipeleka wazo hilo mbele ya Tume ya Huduma za Bunge. (*Makofi/Vigelegele*)

Lakini kwa sasa hivi ile siwa atakayoibeba leo kumtoa Spika baada ya Bunge kufungwa kama haitatokea mambo mengine kama yanavyoombwa sasa hivi, itakuwa ndio *gwaride* lake la mwisho. (*Makofi*)

Ndugu Abdallah Gora unaweza kurudi mahali pako pa kazi. (*Vigelegele/Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Kwa mkataba, atarudi.

**SPIKA:** Tunaendelea na *Order Paper*, Katibu endelea!

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

**Muswada wa Sheria Kuhusu Utaratibu wa Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa wa Mwaka 2005 (The National Leader Funeral Bill, 2005)**

(*Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa mara ya Kwanza*)

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **AZIMIO**

**Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika ((African Energy Commission))**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liridhie makubaliano ya kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika (*African Energy Commission, AFREC*).

Mheshimiwa Spika, mnamo mwezi Aprili, 2001 Mawaziri wa Nishati wa Afrika walikutana nchini Algeria kutafakari maendeleo ya nishati katika nchi za Afrika. Katika kikao hicho, Azimio la kuundwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika (*African Energy Commission*) lilipitishwa.

Kuanzishwa kwa Tume hiyo kunafuutilia maamuzi yaliyofikiwa mwaka 1995 huko Accra, Ghana ambapo ilisisitizwa kuwa maendeleo ya kijamii ni lazima yaambatane na matumizi ya nishati endelevu.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa Tume hiyo ni kuunganisha nguvu za nchi wanachama katika kuendeleza sekta ya nishati za nchi husika na kuhakikisha kuwa nishati inakuwa kichocheo kikubwa katika kuleta maendeleo ya kijamii kwa wananchi wake na kuendeleza ubora wa maisha kwa kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nishati ya Afrika imeanzishwa kwa kufuata misingi muhimu ifuatayo:-

- (a) Kuendeleza matumizi ya nishati ili kusaidia kukua kwa uchumi na maendeleo ya jamii, kupunguza umaskini na kuongeza ubora wa maisha kwa nchi wanachama;
- (b) Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi wanachama katika kuendeleza vyanzo vyta nishati na kuitangaza miradi ya nchi wanachama;
- (c) Kuhamasisha uendelezaji na utumiaji endelevu wa nishati na kutunza mazingira;
- (d) Kutangaza maeneo ya utafiti na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika sekta ya nishati;
- (e) Kuhakikisha nishati inayotolewa kwa nchi wanachama inatosheleza mahitaji, ni ya kuaminika, salama na ya bei nafuu;
- (f) Kuhakikisha kila mwanachama anachangia gharama za uendeshaji wa Tume ya Nishati ya Afrika kwa misingi ya utawala bora na uwazi; na
- (g) Kuhamasisha ipasavyo biashara na misaada ya kifundi katika sekta ya nishati. Aidha, vipengele muhimu vyta makubaliano haya kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

Sura ya Kwanza, inatoa maelezo juu ya maeneo ya jumla ikiwa ni pamoja na maana ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika mkataba, kanuni, kazi na muundo wa Tume.

Sura ya Pili, inaelezea utawala ikiwa ni pamoja na madaraka na majukumu ya Bodi ya kiufundi na Sekretariati ya Tume, pamoja na vikao vyake vyta kawa. Pia imeeleza kazi, taratibu na sheria za Bodi ya Sekretarieti.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Tatu, inaeleza upatikanaji wa mali, rasilimali na ukaguzi wake. Rasilimali hizo zitajumuisha:-

- Michango ya mwaka ya nchi wanachama;
- Michango maalum kutoka nchi wanachama;
- Gawio/faida yoyote kutokana na kazi zitakazofanywa na Tume;
- Zawadi na michango mingine; na
- Vyanzo vingine kama itakavyokubaliwa na bodi.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Nne, inaeleza mambo mengineyo na utaratibu utakaotumika na nchi wanachama ikiwa ni pamoja na kufanya mabadiliko mbalimbali kama vile kujitua uanachama, lugha itakayotumika mahusiano na jumuia nyingine za kiuchumi na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuridhiwa, Tume ya Nishati ya Afrika itakuwa na majukumu yafuatayo:-

- (i) Kuhamasisha uendelezaji na utumiaji endelevu wa nishati ya kisasa;
- (ii) Kutangaza maeneo ya utafiti kwa lengo la kuyaendeleza;
- (iii) Kuhakikisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika sekta ya nishati, ili kusaidia kukua kwa uchumi na maendeleo ya jamii, kupunguza umaskini na kuongeza ubora wa maisha kwa nchi wanachama;
- (iv) Kuhakikisha kuwa nishati inayotolewa na nchi wanachama inatosheleza mahitaji, ni ya kuaminika, ni salama na ni ya bei nafuu;
- (v) Kuhamasisha ipasavyo biashara na misaada ya kifundi katika sekta ya nishati mionganoni mwa nchi wanachama;
- (vi) Kutunga na kusimamia sera na mipango madhubuti ya kuendeleza nishati ya kisasa katika Afrika; na
- (vii) Kushauri namna ya kujenga uwezo katika sekta ya nishati na kutoa mafunzo ya kiufundi katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, iwapo Tume hii itaridhiwa itakuwa ikiendeshwa kwa michango ya nchi wanachama ambapo kila nchi itakuwa ikichangia kiasi ambacho kitapendekezwa na kukubaliwa na wanachama wote watakaoridhia Azimio hili. Kwa upande mwagine Tume itawasiliana na Mashirika ya Kimataifa kama *UNIDO*, *UNESCO*, *UNEP*, *UNDESA* na Shirika la Nishati la Kimataifa ili kupata misaada ya kiufundi na kifedha.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingi ya nishati vilivyopo Afrika ambavyo havijaendelezwa vinafanya nishati isitumike kikamilifu katika kuleta mendeleo ya wananchi katika nchi za Afrika. Mfano, *Nile Basin Initiatives*, *Inger Dam-Congo*, *Stigler's Gorge - Tanzania*, na kadhalika. Hivyo katika kikao chake cha 37, Umoja wa Afrika uliona umuhimu wa kuyatangaza maeneo husika ili kuhamasisha teknolojia ya kisasa katika sekta ya nishati na hatimaye kuhakikisha kwamba nishati inayotolewa na nchi wanachama inatosheleza mahitaji.

Mheshimiwa Spika, *AFREC* itakuwa ni moja ya vitengo vinavyoundwa na Jumuiya ya Afrika. Kitengo hiki kitakuwa na wanachama kutoka katika kila nchi iliyo

katika Jumuiya ya Afrika. Ili kuhakikisha kuwa inatekeleza majukumu yake ipasavyo, chombo hiki kitakuwa na Bodi ya kiufundi pamoja na Sekretarieti ya Tume.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa yaliyomo kwenye makubaliano ya kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika, utaanza mara baada ya nchi wanachama kuridhia makubaliano haya. Nchi wanachama ziliombwa kuridhia makubaliano hayo tangu mwaka 2001 hadi sasa nchi zilizokwishardhia ni saba ambazo ni Algeria, Comoro, Misri, Libya, Msumbiji, Rwanda na Senegal. Makubaliano yalifikiwa kwamba mara baada ya nchi 15 kuridhia na kusaini mkataba huo basi chombo hiki kitaanza kazi.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya nchi yetu kuridhia makubaliano haya ni kwamba:-

(i) Kwa ushirikiano na nchi wanachama tutaweza kuweka mipango endelevu ya kuendeleza nishati na hatimaye kukuza sekta mbalimbali za jamii na za uchumi ambazo zinategemea sana kuwepo kwa nishati ya uhakika na ya bei nafuu.

(ii) Kuleta mabadiliko katika maeneo ya vijiji katika upatikanaji wa nishati hasa katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, pendekeso linalowasilishwa ili Bunge liridhie kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika *AFREC* ni kama ifuatavyo:-

KWA KUWA katika kikao chake cha 37 kilichofanyika Lusaka, Zambia Julai, 2001, Umoja wa Afrika ulipitisha kwa kauli moja Azimio la kuundwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika;

NA KWA KUWA makubaliano hayo yana lengo la kuendeleza matumizi ya nishati ili kusaidia kukua kwa uchumi na maendeleo ya jamii, kupunguza umaskini na kuongeza ubora wa maisha kwa nchi wanachama;

NA KWA KUWA nia ya wanachama wa Afrika ni kuimarisha ushirikiano baina ya nchi wanachama katika kuendeleza vyanzo vya nishati na kuitangaza miradi ya nchi wanachama;

NA KWA KUWA nchi wanachama zinatambua umuhimu wa kuhamasisha uendelezaji na utumiaji endelevu wa nishati na utunzaji wa mazingira;

NA KWA KUWA nia ya nchi wanachama wa Afrika ni kutangaza maeneo ya utafiti na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika sekta ya nishati ili kuhakikisha nishati inayotolewa na nchi hizo inatosheleza mahitaji ni ya kuaminika, salama na ya bei nafuu;

NA KWA KUWA utaratibu wa uanachama utakuwa ni kwa kila mwanachama kuchangia gharama ipasavyo katika utekelezaji wa makubaliano kwa msingi wa utawala bora na uwazi;

NA KWA KUWA matokeo ya kuridhiwa kwa makubaliano haya ni kuhamasisha ipasavyo biashara na misaada ya kiufundi katika sekta ya nishati;

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya makubaliano haya na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(A) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Bunge hili sasa katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa linaazimia Kuridhia Makubaliano ya Kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (*African Energy Commission*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. SALOME J. MBATIA - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, ninaomba na mimi niungane na Wabunge wenzangu kutoa salaamu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Balozi Ahmed Diria pamoja na familia ya Balozi Paul Bomani kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika yaani *African Energy Commission (AFREC)* kwa mujibu wa Kanuni ya 43(5)(b) ya Kanuni za Bunge, toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji na Biashara inaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini iliyowasilishwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na kuliomba Bunge lako Tukufu kuridhia Azimio hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaafiki hoja hiyo kwa misingi ifuatayo:-

(i) Nchi yetu inavyo vyanzo vingi vya nishati ambavyo havijaendeleza au kutumika kikamilifu kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa Serikali. Kwa mfano maporomoko ya *Stigler's Gorge*, gesi ya asilia ya Songosongo na *Mnazi Bay* na makaa ya mawe Kiwira na Liganga huko Ludewa. Hivyo kuridhia Azimio hili kutaifanya nchi yetu kufaidika na mikopo ya pamoja ya kuiendeleza vyanzo hivyo. (*Makofi*)

(ii) Baadhi ya miradi ya nishati ni mikubwa mno kwa nchi moja kuiendeleza na kwa wakati huu hata kuiendesha kwa faida kwa mfano *Stigler's Gorge*. Kutokana na kuundwa kwa Kamati ya Nishati ya Afrika itawezekana kuiendeleza miradi hiyo na kuunganisha mifumo ya nishati hiyo kwa nchi wanachama na hivyo kuleta faida kwa wanachama.

(iii) Kutokana na uwezekano wa nchi zote wanachama kuunganishwa katika mfumo mmoja wa nishati, kuundwa kwa Tume hii kutatuhakikishia nishati wakati wote.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kukushukuru kwa fursa hii uliyonipa ili niweze kutoa maoni haya. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Dr. Ibrahim Msabaha na wataalam alioongozana nao kwenye Kamati yetu ambao waliweza kutoa ufanuzi mbalimbali kuhusiana na Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa William Shellukindo, kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni haya kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge, wajumbe wenzangu wa Kamati kwa michango yao iliyowezesha kuleta maoni haya. Nao ni Mheshimiwa William Shellukindo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Margaret Bwana, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ismail Ivvatta na Mheshimiwa Stephen Kazi.

Wengine ni Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Khamis Aboud, Mheshimiwa Freeman Mboge, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Ali Mussa, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Sumri Mohammed, Mheshimiwa Mohammed Ali Said, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwanga na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka , kwa maandalizi mazuri ya Kamati na Ndugu Aggrey Nzowa kwa kuhudumia Kamati yetu vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika sekta hii, lakini sio mionganoni mwa wale waliofukuzwa jana, Mheshimiwa Isaac Cheyo. (*Kicheko*)

**MHE. ISAAC M. CHEYO - MSEMADI WA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, natumaini yale yaliyotokea jana tuyaa che hivyo hivyo, lakini iwe fundisho kwa watu wengine pia. (*Makofî*)

**SPIKA:** Safi kabisa, ndio!

**MHE. ISAAC M. CHEYO - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA  
YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa maoni kuhusu Mkataba wa Kuanzishwa Tume ya Nishati ya Afrika (*African Energy Commission*)

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa nchi zote ambazo ziliamua kushirikiana na nchi jirani au kwa ushirikiano wa kijumuiya, nchi hizo zilitoa nafasi kubwa kukua kiuchumi na maendeleo. Pia tunaamini kuwa nchi zote ambazo ziliamua kutoshirikiana na wenzao, uchumi wao na maendeleo yao yalidumaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia mkataba huu, inatoa nafasi kwa nchi kushirikiana na nchi nyingine katika kuendeleza nguvu nishati kwa lengo la kuharakisha maendeleo na hatimaye kukuza uchumi wa nchi washirika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni yaliyotajwa katika Azimio hili yanaenda sambamba na ukweli kwamba ili tuweze kuendeleza rasilimali tulizonazo hatuna budi kushirikiana na wenzetu Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina rasilimali nyingi ambazo zinaweza kuendelezwa na hatimaye kuharakisha maendeleo ya nishati vijijini na mijini lakini hatuwezi kufanya hivyo kwa ukosefu wa fedha, taaluma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuendeleza miradi ya nishati umeme kwa kushirikiana na wenzetu kupitia Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya nishati ya umeme kama vile maporomoko ya *Stigler's Gorge* na Kamati wameeleza, vimeshindwa kuendelezwa kwa sababu hatuna uwezo wa kifedha. Kwa ushirikiano, inaweza kuwa ni njia ya uhakika ya kuendeleza miradi kama hiyo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nchi kama Tanzania imejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya nishati umeme kama vile umeme kupitia makaa ya mawe, gasi na maporomoko ya maji. Vyote hivi kwa pamoja tukiviendeleza nchi itapata umeme wa kutosha kwa matumizi yake na majirani zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia *African Energy Commission*, nishati iliyoko kwa nchi jirani pia inaweza kuendelezwa na kutumika hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, umeme ni nyenzo muhimu kwa uzalishaji na kwa kuzingatia *geo-position* ya nchi yetu imezungukwa na nchi jirani ambazo umeme wake ni wa bei ya chini ukilinganishwa na umeme wa kwetu hapa nchini Tanzania.

Hivyo ni jambo la busara kutumia fursa hii ya uanachama wa *African Energy Commission* kupata umeme wa bei ya chini kutoka kwa majirani zetu kwa uzalishaji viwandani. Umeme kama *component* ya uzalishaji, bei yake ikiwa chini hata *final products* nayo inakuwa chini hivyo inaweza pia ikaingizwa katika ushindani wa soko.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi tulionao ni kwamba dhana ya uanzishwaji wa Tume ni nzuri na inaleta matumaini kwa wananchi na wanachama lakini utekelezaji wake unatupa mashaka hasa katika nyanja zifuatazo ambapo tunaomba Serikali ituhakikishie imejipanga namna gani kwa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika misingi ya mkataba huu kuna kipengele kinachosema, “kuhakikisha kila mwanachama anachangia gharama za uzalishaji, uendeshaji wa Tume ya Nishati ya Afrika kwa misingi ya utawala bora na uwazi”.

Mheshimiwa Spika, msingi huu muhimu unaleta mashaka mengi kwa sababu mikataba yote ya Serikali haiko wazi kwa wananchi na hata taasisi zinazowakilisha wananchi. Uwazi haupo na sio mara moja Waheshimiwa Wabunge kuitaka Serikali iwave mikataba inayohusu nchi na nchi au nchi na makampuni, mikataba hii Serikali imekuwa na msimamo kwamba hiyo ni siri ya Serikali na wahusika, mifano iko mingi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge walitaka kupata Mikataba kama vile ya *IPTL, TANESCO* na Serikali. Wabunge mpaka sasa hawajapata. Uwazi haupo!

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa *Net Group Solution* na Serikali haujawa wazi kwa Wabunge na wananchi kwa ujumla wake. Pia na Mikataba mingine mingi tu kama vile Ukedishaji wa Uwanja wa *KIA* kwa dola 1000 kwa mwaka, Mikataba ya Madini *TTCL* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, msingi huu unawataka nchi wananchama wawe wazi, lakini kwa jadi hii ya usiri tunataka Serikali itueleze itajinasuaje ili iendane na matakwa ya Mkataba wenye. Tunataka Serikali itamke kwamba Mikataba hii itakuwa wazi kwa Wawakilishi wa wananchi au wadau wote.

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine kinahusu uchangiaji. Nchi yetu ni maskini, bado tegemezi kwa Wafadhili. Sio mara ya kwanza kupata maeleo kwamba tumeshindwa kutekeleza miradi yetu kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Pia, sababu nyingine ni kwamba wafadhili hawajatoa ahadi zao kikamilifu. Kwa hali hii ya ufinyu wa bajeti, Serikali itawezaje kutoa mchango wake kwenye *Commission* hii?

Mheshimiwa Spika, kutochangia kama inavyotakiwa ni sharti mojawapo la nchi mwanachama kutopata faida zitokanazo na Mkataba huu kama vile *Research, Technical Assistance* na kadhalika. Tunataka kuhakikishiwa na Serikali kwamba nchi yetu itakuwa mshirika hai anaye-honour michango yake kwenye *Commission* hii.

Mheshimiwa Spika, wanachama wa *Commission* hii ni karibu nchi zote za Afrika. Nchi hizi haziko sawa katika nyanja mbalimbali kisiasa, kiuchumi, kimaendeleo na kadhalika. Kutokana na kutokuwa sawa katika nyanja hizo, kunafanya utekelezaji wa uundaji wa *Commission* uwe mgumu. Kwa mfano, ni lini nchi wanachama wataaminiana katika kujenga mazingira ya ushirikiano kama hakuna siasa za kuvumilian?

Kwa mfano Uganda na *DRC*, *they are in conflict*. Msuguano pia katika nchi zile ambazo ni wanachama, misuguano ya ndani bado ipo na tunasema hapo ni *internal conflicts* kama *in the Sudan, Somalia, Ivory Coast* na nchi nyingine. Hivyo, inatoa nafasi ya hizo nchi kutokuwa na *concentration* katika suala la maendeleo.

Vilevile, kutoaminiana katika nyanja za kibiashara zinazotokana na utofauti wa kiuchumi; nchi wanachama kama vile Tanzania na *South Africa* hatuko sawa kiuchumi wala kimaendeleo. Watanzania tunaona tunanyonywa na *Republic of South Africa*. Je, kutoaminiana kwa namna hii kweli kutaweza kurahisisha kujenga hiyo *commission* kama inavyotakiwa?

Mheshimiwa Spika, pia kuna matatizo mengi tu ambayo ni ya kijamii. Hivyo basi, tunasema *diversities* kama hizi zinahitaji *a higher study* ya namna gani Afrika inaweza kuyaweka mambo yake sawa ili isiharibu nia njema ya kuanzishwa *African Energy Commission*. Hili siyo suala la kurukia tu. Tungependa tulifanyie *study* ya kutosha na kuweza kuliweka sawa liweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuonyesha kuwa kuna kutokuaminiana katika nyanja hizi, nchi nyingi za Afrika bado hazijatia saini Azimio hili. Mheshimiwa Waziri amesema ni nchi saba tu mpaka sasa, lakini Azimio lenyewe ni kwa ajili ya nchi zote za Afrika. Hii inaonyesha kuwa Afrika haijawa pamoja katika nyanja za *Ideological and Economic Differences and the like*.

Mheshimiwa Spika, Afrika tungependa iwe na maeneo mengi ya ushirikiano katika nyanja mbalimbali kwa maendeleo yetu. Kutoaminiana ni jadi ya Afrika na ni kikwazo kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ushawishi. Tunaamini kabisa Mheshimiwa Msabaha na wenzake wamebobea katika mambo ya diplomasia, kwa hiyo, tungeomba wafanye ushawishi nchi za Afrika zikae kwa amani, ziaminiane na ziweze kufanya mipango yake ya kimaendeleo kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii kuchangia Azimio hili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuliunga mkono Azimio hili pamoja na kwamba nitakuwa na baadhi ya mawazo fulani ambayo nitaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla iangalie na iweze kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kwamba Julai, 2001 Umoja wa Afrika ulipitisha kwa kauli moja Azimio la Kuundwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika. Naunga mkono asilimia mia kwa mia (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa sababu tunategemea kwamba kutakuwa na mafanikio makubwa na Azimio hili litagusia maendeleo na uchumi wa nchi na watu kwa ujumla, hatuna budi kwa kweli kuiunga mkono Wizara lakini pia tuitakie kwamba ifanikishe haya ambayo imeyakusudia katika Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, nnikinukuu, kwa nini imezishawishi kuweza kuunga mkono Azimio hili? Katika *paper* hii ambayo imetoka kwa Mheshimiwa Waziri, imesema: “Makubaliano haya yana lengo la kuendeleza matumizi ya nishati ili kusaidia na kukuza uchumi na maendeleo ya jamii.” Ni masuala ya msingi kabisa. Kwa sababu lengo letu kubwa ni kukuza uchumi na maendeleo ya watu wetu, lakini vilevile naweza kusema ni kupunguza umaskini na kuongeza ubora wa maisha kwa nchi wanachama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zinapata matatizo ya kiusalama kutokana na hali duni ya uchumi na maendeleo ya wananchi wake. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba Azimio hili na Tume hii, kwa sababu inagusia nishati muhimu kwa maendeleo ya watu, basi ni matumaini yetu kwamba italeta mafanikio yale ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sio siri kwamba sasa hivi uchumi mkubwa katika dunia unaongozwa na elimu pamoja na viwanda na sasa hivi maeneo makubwa yanatumia *Thermo Electronic* sana na bila kuwa na nishati huwezi kutumia *electronic*. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba nishati kama itasambaa katika mashule na maeneo mengine Vijijini, tutakuwa na maendeleo makubwa katika nchi yetu na kwa wananchi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba Azimio hili wataalam wetu wa Serikali kwa ujumla watalifanya kazi na kuleta mabadiliko yale ambayo yalikusudiwa kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nilisema kwamba kuna maeneo tu kidogo nitajaribu kuyafanya marekebisho ili tuendane na hili Azimio.

Mheshimiwa Spika, katika makabrasha yetu tumepokea vilevile waraka wa Baraza la Mawaziri, imewekwa tu namba lakini ni wa mwaka 2002. Waraka huu unahuksu Kuridhia Mkataba wa Kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika. Ninanukuu. Waraka huo sehemu ya utangulizi inasema: “Moja kati ya majukumu ya Umoja wa nchi huru za Africa ni kuweza kuongeza ushirikiano wa Umoja wa Afrika (*OAU*) na kuinua maendeleo ya Uchumi kwa nchi wanachama.”

Mheshimiwa Spika, moja ya marekebisho katika Waraka huu wa Mawaziri, naomba warudi tena *OAU*, sasa hivi haipo tena, ipo *African Union*, kwa hiyo, ni vizuri mambo yetu yote yakawa sawasawa. Isiwe Waraka wa Mawaziri unasema hivi na Azimio linasema hivi. Kwa hiyo, kama sasa hivi Afrika tuna *African Union*, sasa katika Waraka huu kwa sababu ni wa mwaka 2002 na unaelezea kwamba ni kuongeza ushirikiano wa Umoja wa Afrika na ukaweka (*OAU*), naomba Mawaziri warudi

wakaurekebishe tena Waraka huu ili iainishwe pale iwe *AU* kwa sababu sasa hivi ndiyo Umoja wetu wa Africa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba katika Waraka huu umeelezea ushirikishwaji wa wadau na wakasema Waraka umetayarishwa kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawapongeza sana. Naamini yataondoa yale malumbano ambayo watu huwa wanatuhumu kwa yale madogo madogo wakidhani labda Zanzibar huwa haishirikishwi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa tunazungumzia suala la nishati na kwa sababu katika Azimio hili mmeshirikisha Zanzibar, mimi nataka niiombe tena Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Wizara yake ya Nishati na Wizara ya Nishati ya Zanzibar, hebu mtupe uhakika kuhusu suala la mafuta Zanzibar. Kweli yapo? Kama yapo, kwa nini hamjaewana mpaka leo? Tunazungumzia nishati na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hili kwa sababu sisi kule Pemba ni wiki sasa hatuna umeme, tunashindwa hata kusalimiana na familia zetu, simu hazina *charge* na hatuwezi kuwa na maendeleo bila kuwa na nishati. Kama itakuwa ni nishati ya mafuta, tunayo ambayo tunasikia kwamba yanatosheleza kwa matumizi ya ndani ya nchi na kuuza nje ya nchi. Nina uhakika kwamba nchi yetu itapiga hatua kubwa sana kimaendeleo kutoka tarehe hii ya leo mpaka huko mbele tunakokwenda.

Ninaomba mkae mjaribu kuondoa tofauti kwa sababu, moja katika nishati muhimu ni mafuta. Kuna tatizo gani? Tuondoeni ubinafsi tujenge umoja kuleta mafaniko kwa sababu kama tunazungumzia masuala ya gesi kama Songsongo inawezekana Zanzibar ikawepo, vyanzo vya nishati hivi ni vingi sana. Kwa hiyo, hebu kaeni mtulie mtufanyie mambo kwa faida ya watu.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika Waraka huu, unasema kwamba kwa kuzingatia kifungu Na.16(2) nchi wanachama itatakiwa kulipia michango maalum na ya kila mwaka; Je, uwezo tutakuwa nao? Hii michango itakuwa ni kiasi gani kwa mwezi na kwa mwaka? Kidogo nilitaka Wizara itusaidie katika hii na kama Msemaji wa Upinzani alipokuwa anawasilisha alisema, ni nchi saba tu. Je, hizi nyingine inawezekana hazijaridhia Azimio hili? Pengine uwezo wao kiuchumi hawana, wanakimbia hili suala la kuchangia. Tuliangalie vilevile kwa mapana na marefu ili lisije likaleta mgongano na kubeba majukumu makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama nchi hazina uwezo wa kuchangia tutazisaidia vipi ziingie katika Azimio hili? Hapa ndipo ninaposema inanitia wasiwasi kwamba hatutaweza kwenda pamoja kama nchi za Kiafrika. Kwa sababu itakuwa ni kosa kwamba nchi za kiafrika ziko nyingi lakini kwa kweli kwa nchi saba tu hatutafanikiwa yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nataka ninukuu mwisho ule waraka. Unasema, Na.9 kwamba: "Naomba mtafakari pendekezo lililotolewa katika aya ya nane ya Waraka huu na kumshauri Mheshimiwa Rais akubali agizo litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana kuwepo kwa kipengele hiki na tunamwomba Mheshimiwa Rais atekeleze Azimio hili kwa niaba ya Watanzania, lakini vilevile kuyashauri na yale Mataifa mengine ya Afrika yaweze kuingia katika Azimio hili kwa faida ya Bara letu la Afrika ili kuleta Umoja na Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu kuhusu Azimio lililoko mbele yetu linalohusu makubaliano ya kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika, yaani *African Energy Commission (AFREC)*.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla ya yote ningependa kuunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Sababu yangu ya kuunga mkono ni kwamba kwanza Azimio lenyewe limechelewa kwa sababu Bara la Afrika kama tunavyoju, kwa muda mrefu limekuwa likijulikana kama ni Bara jeusi, yaani *Dark Continent*. Pengine weusi huo ni kutokana na kutokuwa na mwanga na mwanga maana yake ni umeme au kwa sababu ya rangi za wakazi wa bara hili. Lakini kubwa zaidi ni weusi wa maendeleo. Bara hili liko nyuma kimaendeleo kwa muda mrefu sana.

Mimi kutokana na ule Mkataba wenyewe, makubaliano yenyewe nimevutiwa na ile sehemu ya utangulizi iliyokuwa inasema kwa kujuwa kwamba katika Bara la Afrika au sehemu nyingi za nchi za kiafrika kuna upungufu mkubwa wa umeme na upungufu mkubwa wa nishati na maendeleo hayawezi kupatikana kutokana na hali hiyo, basi jambo hili ni lazima litiliwe mkazo.

Kwa maana hiyo nasema kwamba, nishati maana yake ni maendeleo na bila ya nishati maendeleo hayawezi kupatikana. Hivyo, kwa kuunga mkono Azimio hili, sisi tutakuwa watu wa nane au nchi ya nane lakini kusema kweli ningeomba ikiwezekana zifanywe kila juhudhi nchi zinazotakikana zifike 15 hizo saba zilizobakia, basi zipatikane haraka iwezekanavyo kwa sababu panapokuwa na Tume hii, Tume hii itafanya kazi ya kuoanisha sasa na siyo kuoanisha peke yake, bali ku-*coordinate* mipango ya nchi zote katika vyanzo vinavyopatikana nchi zote katika Afrika ili tuweze kupata umeme au nishati.

Hii haina maana nishati ya maji tu, maporomoko ya maji tu bali nishati ya kila aina hasa ya makaa ya mawe, nishati ya gesi, nishati ya mwanga wa jua (*solar*), nishati ya *biogas* kwa kutumia vinyesi na kadhalika. Kwa hiyo, hapa maana yake ni kwamba tutakuwa na nishati mbadala nyingi katika maeneo mengi ya Afrika na kwa maana hiyo basi, tutakuwa na vyanzo vingi.

Sehemu ya pili au sababu ya pili inayonifanya mimi niunge mkono Azimio hili ni katika sehemu ile ya pili iliyokuwa inazungumza juu *convention*, kwamba hii itakuwa ni kama, naomba nisome pale *reckoning the various resolutions and declarations where in it had been stipulated that the integrated economic development of the African Continent is an assential condition for the achievement of the objectives of the Organization of African Unity (au African Union).*" Maana yake ni kwamba, hapa kutakuwa na kuunganishwa pamoja mipango ya nchi zote za kiafrika katika masuala ya nishati na kutakuwa na maana hiyo na mpango wa pamoja wa Maendeleo ya Uchumi.

Kusema kweli katika Bara la Afrika sasa tunataka maendeleo ya uchumi. Maendeleo ya kisiasa tumeshayapata kwa sababu nchi zote za Afrika ziko huru, tatizo letu kubwa ni maendeleo ya uchumi na kama nilivyosema pale mwanzo, bila ya nishati maendeleo ya uchumi ni ndoto.

Wakati fulani nilipatwa na mawazo nilipokuwa *Nairobi University* kuandika *research* kuhusu Bara la Afrika kuwa Bara la Viwanda katika mwaka 2018. Watu wengi sana walicheka lakini kwa kuangalia vyanzo vya nishati pamoja na uwezo tulionao katika Afrika, tunaweza kulifanya Bara hili kuwa ni Bara la viwanda au Bara la Maendeleo ya Viwanda. Lakini kwa sababu tumedharau na kutokuwa na umuhimu wa kuvitumia vyanzo vya nishati katika Afrika, ndiyo maana tuko nyuma. Siyo katika kilimo tu ambacho nchi nyingi za Afrika zinategemea maendeleo yake ya uchumi katika kilimo, bali hata katika viwanda.

Hii ilinipeleka mbali sana kuangalia jinsi Japan pamoja na wenzetu India walivyoweza kuendelea kwa muda mfupi wa miaka 20, miaka 25 tu waliweza kuendelea kwa haraka sana kwa sababu ya nishati. Waliweza kuyageuza maeneo yao yale ya kilimo kuwa ni maeneo ya viwanda, maeneo yote ya Kobe, sehemu zile za Okinawa sasa hivi ni viwanda. Lakini yalikuwa ni mashamba ya mpunga yale kama tulivyokuwa nayo sisi kule Rufiji. Lakini tungeweza kuyageuza yale kwa muda mfupi tu yakawa viwanda. Kwa hiyo, mimi nadhani kwamba tuna haja sasa ya kuimarisha suala la hii Tume ya Nishati Afrika kuoanisha ili kuwa na mpango wa pamoja wa kukabili suala hili la maendeleo katika Afrika. Hii sehemu ya kwanza. (*Makofî*)

Lakini sehemu ambayo inanifanya nishawishike zaidi kuunga mkono Azimio hili, ni katika makusudi makubwa ya kuanzisha Tume hii na aliyewasilisha wazo hili ni Dr. Msabaha. Amewasilisha kwa ufundi mkubwa. Katika vipengele vile muhimu vya Mkataba nimevutiwa sana na sehemu inayosema hivi: "Katika makusudio kuhakikisha nishati inayotolewa kwa nchi wanachama inatosheleza mahitaji, ni ya kuaminika, salama na bei nafuu." Tanzania bei ya nishati ni kubwa sana. Ndiyo maana sasa hivi hali inakuwa ngumu katika misitu yetu, watu lazima watumie kuni sana, watumie mkaa na kadhalika kwa sababu bei ya umeme ni kubwa. Sasa Tume hii pengine itafanya kazi ya kuoanisha sasa ya ku-coordinate kuona bei ya Tanzania ambayo ni kubwa ya nishati ilingane na ya Kenya, Uganda na kwingineko ili pia huyu mkazi anayekaa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania aweze kumudu bei hasa huko Vijijini.

Tukikumbuka katika Kikao hiki hiki cha Bunge, pale mwanzo tu wa Bunge hili, tulipitisha Muswada kuhusu Taasisi ya Umeme na Mfuko wa Umeme Vijijini. Sasa huu umeme Vijijini tunakusudia nini kama si ndoto tu? Ni lazima bei ya umeme ishuke ili mwanakijiji aweze kumudu huko Kijijini, vinginevyo itakuwa ni kazi bure. Kwa Muswada huu au Sheria hii au Mfuko huu kuweza kusaidia Vijiji viweze kuwa na umeme wakati ambapo bei ni kubwa, hakuna mwanakijiji atakayeweza kumudu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja kwa sababu hizi tatu ambazo nimezitoa na kwamba sasa tutoke katika hali ile ambayo wenzetu katika mabara mengine waliokuwa wametuona kwamba ni Bara jeusi (*dark continent*) tuje sasa katika hali hii ya maendeleo makubwa yanayopatikana ulimwenguni.

Hali ya utandawazi (*globalization*), hali ya maendeleo makubwa na kwamba tayari tumepiga hatua katika maendeleo makubwa katika ubinadamu katika Afrika, nchi zote zimekuwa huru na sasa hivi tunaelekea katika Umoja wa Afrika, Muungano wa Afrika na siku moja tutapata *United States of Africa*. Hiyo naamini kabisa na kwa maana hiyo, tuandae mazingira haya ya kwenda pamoja kinguvu, kinishati, kimaendeleo, kiuchumi na kadhalika na siku moja tutakuwa na Bara moja kubwa zaidi kuliko *United Stated of America* au *European Union* na Mungu Ibariki Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. REYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwa hoja hii iliyopo mbele yetu. Lakini pamoja na hayo, nataka kuishukuru sana Wizara ya Nishati na Madini kwa kuleta Azimio hili ambalo limepita muda mrefu sana. Limepita toka lilipobuniwa na kwa bahati mbaya changamoto hii haijaungwa mkono sana na nchi nyingi za kiafrika.

Mheshimiwa Spika, panapokuja suala la ushirikiano baina ya nchi na nchi, baina ya Mkoa na Mkoa, Wilaya na Wilaya, mimi ni mmojawapo ambaye ninaunga mkono sana hatua za namna hiyo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba toka mwanzo naliunga mkono Azimio hili kwa asilimia mia kwa mia. Lakini nataka kusema kwamba naliona ni changamoto kubwa na *challenge* kwa Wizara yetu ili kuijandaa vizuri kuhakikisha kwamba Tanzania inanufaika vizuri katika Tume hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu Tanzania ina vyanzo vingi sana sana nya nishati hii ya umeme tukianza na *Stigler's Gorge*, uende Mchuchuma, gesi ya Songosongo na kadhalika. Hivi vyote ni vyanzo alivyotupa Mwenyezi Mungu, lakini kwa bahati mbaya tunavitumia kwa asilimia ndogo sana.

Sasa mimi ningiomba Wizara ijitutumue hasa kama ilikuwa imelala kidogo, basi iamke zaidi kwa kujua kwamba tunaweza kufanya mambo makubwa katika nchi hii yatakayonufaisha si nchi yetu tu peke yake, lakini Bara lote la Afrika. Kwa mfano tukiurudia mpango wetu ule wa *Stigler's Gorge* ambao una uhakika wa kutoa nishati ya kutosha kwa nchi nzima, mimi nafikiri jambo hili linaweza kuungwa mkono na nchi

nyingi si za Afrika tu peke yake, lakini hata dunia nzima. Kwa hiyo, sielewi kwa nini mpaka leo mpango huo uko kwenye madeski.

Halafu hili la Songosongo, Songosongo iligunduliwa toka mwaka 1974, hivi leo ndiyo tunaona matunda yake, wote tunafurahia lakini tumepoteza muda mrefu sana ambapo tungekuwa tumefaidika na nishati hii. Hivyo hivyo nikija kwenye gesi yenye chanzo pale *Mnazi Bay* Mtwara, hivi sasa gesi ya *Mnazi Bay* ina lengo la kuhakikisha kwamba kule Kusini kote wananchi wanapata umeme au nishati ya kutosha lakini lazima niseme huwa ninafuatilia sana mimi ratiba wanayoitoa Wizara na kwa mujibu wa ratiba yao inaonyesha kwamba gesi ya *Mnazi Bay* itaweza kuanza kutoa umeme ifikapo mwezi Septemba. Ni jambo zuri. Lakini katika maandalizi yetu mimi nakuwa na wasiwasi, ukifika Mtwara hata huwezi kujuu kwamba kweli gesi hii wameshaanza kuichimba.

Mheshimiwa Spika, kutoka Mtwara mpango unasema kwamba umeme huu utapelekwa Masasi, ili Masasi isambaze katika maeneo mbalimbali kama ya Newala, Tandahimba, Nachingwea, Ruangwa na kadhalika. Lakini mpaka leo hata nguzo moja ya umeme haijasimikwa. Sasa naona Septemba yenyewe haiko mbali, kweli tutawahi kuweka *transmission lines* toka Mtwara mpaka Masasi katika kipindi hiki? Wizara huko siyo kulala kidogo?! Naomba tafadhali tuchangamkie jambo hili kesho na keshokutwa tuone nguzo zimesimikwa kati ya Mtwara na Mingoyo, Mingoyo na Masasi hata wananchi wapate imani kwamba kweli umeme wa kutosha unafika. Miezi mitano siyo mingi, tunavyojitahidi katika shughuli za namna hii ndiyo tunajihakikisha kwamba tutakuwa wanachama wazuri katika Tume hii ya Afrika ambayo nia yake kubwa ni kuhakikisha kwamba umeme unapatikana.

Mheshimiwa Spika, mimi katika kuridhia Azimio hili, nataka kuiomba sana Wizara yetu ifanye kila jitihada ili kuhakikisha kwamba nguvu za umeme zinapatikana kwanza kule Kusini. Nimetiwa moyo sana na majadiliano yetu ya hivi majuzi wakati tunajadili juu ya Mfuko wa Nishati Vijijini. Nina uhakika hii ndio njia moja kubwa itakayotufanya tufanye mapinduzi makubwa katika nchi za Kiafrika. Afrika inaitwa ni Bara la giza, lakini kwa namna nyingine unaweza kutafsiri kwamba giza hili linatokana na kutokuwa na nishati ya umeme. Nia yetu ni kuhakikisha Vijiji vyetu vyote vinapata umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wakati huu nchi yetu itumie kila njia kuhakikisha kwamba tunasambaza huu umeme Vijijini. Mimi nimeona katika sehemu zile za Jimbo langu ambako umeme umepatikana maendeleo yake yamekuwa makubwa. Viwanda vidogo vidogo vimezuka vingi. Sasa katika kuzuka viwanda vidogo vidogo ndio mambo yote ya ajira na kadhalika yanapatikana. Kwa hiyo, hatutakuwa na shida yoyote ya watu kukimbia kutoka Vijijini kwenda Mijini. Hili Azimio la Bunge kwa kweli ni Azimio linalotaka kutupeleka katika upande ulio sawasawa kabisa. Mimi nafikiri kwa sisi Watanzania *target* yetu kubwa iwe kuhakikisha kwamba tunapeleka zaidi umeme Vijijini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine, nilitaka kukumbusha tu kwamba Mchuchuma mpaka leo mambo yanasuasua na kadri ninavyoona wenzetu Wizara ya Nishati wapo tayari

kuingiza nishati kutoka Zambia. Wenzetu wana *Kariba Falls* ambapo gharama za kuingiza umeme huu wa Zambia kuja Tanzania fedha hizi zingeweza kutumiwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunachimba mkaa wa mawe wa Mchuchuma na kuuchoma ili uzalishe umeme.

Napenda sana kushirikiana na wenzetu wa Zambia, lakini ni lazima na sisi tukimbie ili tuwe na chanzo kikubwa kwa sababu tukianza kuutegemea umeme kutoka Zambia maana yake ni kwamba sisi hapa tutakuwa Posta kwa ajili ya kupeleka huu umeme Kenya, sasa tutakuwa tunapata faida gani? Umeme unatoka Zambia unapita humu moja kwa moja mpaka Kenya, badala ya sisi wenyewe kuhakikisha kwamba tunauchukua toka Mchuchuma pale na kuwauzia watu wa Kenya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema katika kushirikiana, tushirikiane kwa njia za usawa katika Afrika. Wenzetu Zambia wana umeme wa ziada safi na sisi hapa Tanzania tutumie vyanzo vyetu tuwe na umeme wa kutosha wa ziada ili nasi tuweze kuuza sehemu mbalimbali. Sasa uhusiano wa namna hiyo ndio mzuri.

Juzi tulikuwa tunazungumzia hapa juu ya Shirikisho la Afrika Mashariki, tukaona kwamba Tanzania hatuko tayari kuingia kwa sababu tutakapoingia sasa hivi sisi tutakuwa maboi, wenzetu ni walimu wanakuja kutufundisha hapa. Sasa kwa nini sisi tupeleke maboi kwa wenzetu wa Kenya. Kwa hiyo, ni lazima sasa Wizara ihakikishe kwamba Mchuchuma inazalisha umeme ili uweze kuenea nchini na kuweza pia kupeleka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nchi za Kiafrika na Tume hii iangalie jinsi ya kutumia juu (*solar*) kwa sababu nchi zote za Kiafrika zina juu la kutosha sana, lakini hatuna mipango mikubwa ya kuweza kusambaza hiyo *solar* katika sehemu zetu za Vijiji. Mimi nafikiri Tume hii ikiwepo na Sekretarieti yake iangalie pia uwezekano wa kutumia *solar* hasa katika Vijiji vyetu kwa ajili ya kupata nishati ya kutosha na ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, napenda kurudia tena kwamba, naunga mkono Azimio hili la Bunge na kwamba liridhiwe na Tanzania pamoja na Mataifa mengine ya Afrika. (*Makofî*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie mjadala huu uliopo mbele yetu. Kwanza natangulia kusema kabisa kwamba naunga mkono Mkataba huu wa kuundwa kwa Tume ya Nishati Afrika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi sichelewi kabisa kukubaliana na hili kwa sababu Jimbo langu lipo Vijijini. Kwa hiyo, hatuna umeme kabisa na kwa hiyo hili ni muhimu sana kwetu. Kwa hiyo, hapa ningependa kusema kwamba makubaliano haya tunayakubali na ni muhimu sana kwetu kushirikiana, kuungana na wenzetu ili tuangalie kama tutapata nishati iliyoko katika nchi yetu na hata ikiwezekana tupate katika maeneo ya nchi za jirani. Lakini ningependa kusema kwamba, kuna uwezekano wa kupata nishati iliyo karibu kabla ya kupata iliyo mbali. Kwa mfano, *biogas* ni gesi ambayo inaweza

kupatikana na kuwasaidia wananchi kabla hawajapata umeme mkubwa au *solar* kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Mrope. Inawezekana kabisa katika maeneo yetu ambayo hatuna umeme tukasaidiwa tukapata *solar*, mpaka wakati ambapo tutapata umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanahitaji maendeleo na bila kupata nishati kwa kweli hakuna maendeleo. Katika mpango wa kupunguza umaskini, nishati inasaidia sana. Maendeleo yanayohitajika ni tofauti sana na miaka ya sitini, miaka ya sitini na mwaka huu ni tofauti kabisa. Kwa wakati ule matumizi ya nishati hayaku julikana, ilikuwa inatumika Mijini tu. Lakini mpaka sasa hakuna Kijiji ambacho hakihitaji nishati. Nina hakika kwamba tungekuwa na umeme pale Namanga, kwa kweli umaskini ungepungua sana katika Mji wa Namanga na Longido. Tumelia muda mrefu sana tukihitaji tupate umeme, lakini mpaka sasa bado hatujapata.

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba haya makubaliano pamoja na mchango wa kila nchi kuchangia, isije ikawa tunachangia bure, tusione faida, itakuwa ni hasara tena kubwa sana kwetu. Tunakubali kabisa kuingia kwenye Mkataba huu na ningeomba Serikali pamoja na Wizara inayohusika tuichangie kabisa Tume hii. Lakini tunapochangia tuifaidi. Itakuwa ni hasara wengine wakaenda kutumia mchango wetu na sisi tukashindwa kuutumia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri ni kwamba, hebu tuangalie tunapopata Mikataba kama hii, wananchi wanasubiri sana kwa hamu waone matokeo ya Mikataba hii. Sio kwamba tunajipitishia iwe kwenye makabrasha, lakini tunapitisha ili baadaye iwasakiwananchi na hasa wananchi walioko Vijijini. Kompyuta sasa zinafundishwa mashulen, lakini wanafunzi wanaojifunza kompyuta ni wanafunzi ambao wapo katika eneo ambalo umeme unafika.

Kule kwetu tuna kompyuta lakini kutumia ni kwa muda mchache sana kwa sababu hatuna umeme. Sasa wanafunzi walio katika Shule zilizo Vijijini wanapata hasara sana mpaka wafike sijui Chuo Kikuu ndio waanze kufundishwa kompyuta, ni tatizo! Kwa hiyo, ndio maana elimu inakuwa tofauti. Ningeomba umeme Vijijini ukazaniwe zaidi kwa sababu wananchi wengi walioko Vijijini hawana umeme.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako ningependa kuwaambia ndugu zangu Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wa Wizara hii kwamba, sijui Jimbo la Longido lina nini? Tuna bahati mbaya sana. Umeme unaishia Sanya Juu pale kwa Mwanri, ukiingia kwenye Jimbo langu tu hakuna tena umeme. Umeme mwengine unazunguka Rombo, unaishia Rombo. Inakuwa sisi tunaangalia umeme Hai, Rombo na umeme ulioko Kenya, sisi tupo kwenye giza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa kusema kwamba, kama kuna lile *continent* la giza na sisi bado tupo kwenye Jimbo la giza. Umeme unaishia kwa hawa ndugu zangu, mimi sina umeme kabisa, hata lami nayo inaishia kwao. Kwa hiyo, naomba Wizara hii iangalie tena kwa makini umeme Vijijini katika maeneo haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii na waliosikiliza pia katika Bunge lako Tukufu. Kulikuwa na wachangiaji kwa hotuba sita na ningeomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Salome Mbatia - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Isaac Cheyo - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi - Mndengereko aliyeendelea, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Lekule Laizer. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa pia na mchangiaji mmoja ambaye amechangia kwa njia ya maandishi, naye ni Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge takriban karibu wote kwa kuunga mkono Azimio hili na kuliomba Bunge lako Tukufu liridhie Mkataba huu wa kuanzishwa kwa Kamisheni ya Nishati ya Afrika (*AFREC*). Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kujibu maeneo machache tu na si kujibu kwa kweli, ni kutoa ufanuzi kwa maeneo machache tu yale ambayo kwa hakika yanahitaji kupatiwa maelezo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakubaliana na sababu zote ambazo Kamati ilizitoa na kukubaliana na Azimio hili.

Pili, nikija kwa Mheshimiwa Isaac Cheyo hapa kuna mchango ambao aliutoa, anazungumzia juu ya maeneo mbalimbali kwa mfano, gharama za uendeshaji, Mikataba kwamba inafichwa na kwamba uchangiaji huu Tanzania ni maskini na kadhalika. Hapa naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mfumo wa uendeshaji wa nchi, vyombo vitatu vinavyoendesa nchi ni Bunge, Serikali na Mahakama. Hivi ni vyombo ambavyo kila kimoja kina kazi yake. Nataka niseme tu kwa ufupi kwamba shughuli ya kuandika Mikataba ni shughuli halali ya Serikali katika mgawanyo wa madaraka na kwa kweli Serikali hakuna inachoficha, kwamba labda kuna jambo la ajabu ajabu linafichwa. Lakini lazima pawe na mgawanyo wa kazi na katika mgawanyo wa kazi, Serikali, moja ya kazi zake ni kushughulikia suala la Mikataba, makubaliano baina ya nchi na nchi na kadhalika.

Kwa hiyo, ningependa niseme tu kwa kifupi kwamba suala la Mikataba ambayo Mheshimiwa Mbunge Cheyo anatoa picha, kama vile Serikali inafichaficha na kwa hiyo, basi wananchi hawaielewi. Si kweli! Mfano mzuri ni kwamba, huu Mkataba tunaouzungumzia sasa hivi upo mbele ya Bunge lako Tukufu na vipengele vyote vipo mbele ya Bunge hili Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili, amezungumzia juu ya wasiwasi wake juu ya tofauti baina ya nchi na nchi na kwamba hizi zitasababisha Tume hii kutoweza kufanya kazi. Sasa hoja kama hii haiwezi kuwa hoja kwa ajili ya Tume hii ya *AFREC* peke yake. Itakuwa ni hoja kwa ajili ya Jumuiya nzima ya Afrika, yaani kwa kila kitu unachojaribu kukifanya, basi kitakuwa hakiwezekani. Lakini ukweli na ushahidi uliopo ni tofauti kabisa na kwa hakika hata tunapozungumzia masuala ya migogoro kadri nchi zinavyokuwa katika wigo mpana zaidi, zinavyoungana, ndivyo inavyopatikana fursa ya kuondoa migogoro kwa sababu mnakuwa mnategemeana zaidi.

Mheshimiwa Spika, wataalam wa masuala ya migogoro wanazungumzia wanasema kwamba una-widen area of interdependence, yaani kwa kuwa mnashirikiana sana, mnatengeneza mfumo wa maingiliano mengi na maingiliano yale ndiyo yanawafanya muache kufanya vitu vidogo vidogo vya chokochoko na kugombana kwa sababu hasara itakayopatikana katika kugombana kwenu ni kubwa zaidi kuliko ushirikiano mnaokuwa nao. Kwa hiyo, umoja ni nguvu kama ambavyo imesemwa na umoja au ushirikiano huu ni njia sahihi kabisa ya kuhakikisha kwamba tunasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, la tatu, amezungumzia suala la nchi zilizotia saini, amesema ni saba. Nasema kwamba, nchi ambazo zinategemewa kutia saini ni nchi hamsini na tatu na nchi ambazo tayari zimetia saini ni nchi thelathini na mbili na nchi zilizoridhia ni nchi saba na kama leo Bunge lako Tukufu litakubali kuridhia Mkataba huu maana yake ni kwamba nchi ambazo zitaridhia zitakuwa nane na mimi nakubaliana na hoja ya Waheshimiwa Wabunge kwamba nchi yetu ikishirikiana na nchi nyingine, basi ishawishi nchi nyingine ziweze kuridhia kwa haraka zaidi ili Kamisheni hii ya Nishati ya Afrika iweze kufanya kazi mapema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwa Mheshimiwa Mjaka Ali, labda niseme moja tu kuhusu suala la mafuta. Aliuliza, mafuta Zanzibar yapo? Nataka niseme hivi, hadi sasa hatujaweza kupata mafuta katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano na tumeshawahi kusema hapa Bungeni kwamba endapo yatapatikana, basi Serikali haitasita kutangaza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, juu ya mawasiliano baina ya Serikali zetu mbili kuhusu masuala ya utafiti wa mafuta, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mjaka Ali na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea kujadiliana, kushirikiana, kuhakikisha kwamba suala la mafuta linaendelezwa au utafiti wa mafuta unaendelea kwa manufaa ya nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya umeme ambayo imetajwa na Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi na Waheshimiwa Wabunge wengine, nadhani tumesema mara nyingi hapa Bungeni kwamba, inafahamika kwamba ni lengo na ni Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba tunapata nishati yenye bei nafuu katika kipindi kijacho na tumekuwa tukitoa sababu mbalimbali kwa nini hali ipo kama ilivyo hivi sasa, ingawa lazima niseme pia kwamba hatua kubwa zimechukuliwa katika kupunguza bei kubwa na hasa kwa upande wa uzalishaji kwa upande wa viwanda, tofauti na ilivyokuwa hapo zamani.

Lakini niseme kwamba, hili ni lengo na ni Sera ya Serikali, lakini kadri tunavyoungana na wengine na kadri tunavyoweza kuanzisha miradi mingine ya uanzishaji umeme wenye bei nafuu, ndivyo inavyotupa uwezo au fursa ya kuhakikisha kwamba hapo baadaye tunaweza kuwa na nishati yenyе bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maelezo ya Mheshimiwa Mrope, nataka nimtoe wasiiasi ndugu yangu Mrope kwamba Wizara hii haijalala na haikulala na ndio maana basi tupo katika kiwango hiki cha hali ya juu kabisa ya utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ikiwemo ya *Mnazi Bay*. Sasa hivi *Mnazi Bay* leo tu asubuhi tulikuwa tunapewa taarifa kwamba tayari wameshaanza kuchoma gesi ya majaribio na wamefurahishwa sana na matokeo ya uchomaji huu wa gesi na inatarajiwa kwamba gesi iliyopo itatosheleza katika kipindi chote kilichokadirwa cha uzalishaji wa gesi ile.

Kwa hiyo, napenda nimtoe wasiiasi ndugu yangu na ndugu wananchi wa maeneo ya Mtwara na Lindi na nchi nzima kwa ujumla kwamba mradi ule kwa jinsi mambo yanavyokwenda hivi sasa tuna matumaini makubwa kwamba utaleta tija kubwa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimtoe wasiiasi Mheshimiwa Mrope juu ya suala la umeme unaunganishwa na Zambia kama ilivyo katika Mkataba huu. Suala la kuunganisha umeme baina ya nchi na nchi lina sura mbili. Kwanza, ni suala la usalama wa upatikanaji umeme, yaani kupata nishati endelevu. Tunafahamu kwamba nchi zetu nyingi zinafanana katika vyanzo vyake vya kuzalisha umeme vingi vinategemea uzalishaji umeme kupitia maporomoko ya maji na kadhalika. Pia tunafahamu kwamba hali ya hewa wakati mwingine huwa inasababisha upungufu wa maji. Kwa hiyo mnapokuwa mmeunganisha *Grid* zenu inawezekana kuhakikisha kwamba umeme katika nchi moja unapopungua inawezekana kupata umeme kutoka nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, hili linatuleta kwenye suala la pili ambalo ni suala la biashara. Kwa hiyo, kuna suala la usalama wa kupata umeme au kuondokana na umaskini wa nishati au kuondokana na *energy poverty* na unakuja kwenye suala pia la biashara kwamba tunapounaganisha hizi *Grid* inawezekana kufanya biashara baina ya nchi na nchi, baina ya sehemu na sehemu au baina ya ukanda na ukanda.

Suala hili la kuunganisha njia za umeme kutoka Zambia, Kenya na sisi hapa si suala tu la kuwauzia umeme, sio njia tu ya kuwauzia umeme Kenya, hapana. Sisi wenyewe tutakapokuwa na umeme wa kutosha wa kuweza kuuza, tunaweza pia kutumia njia hizi hizi kuwauzia umeme wenzetu. Zaidi basi ni kwamba, njia hii inatuunganisha nchi za Afrika Mashariki na nchi za Kusini mwa Afrika, yaani *Southern African Power Pool* inaunganishwa na *East African Power Pool*. Kwa sababu hiyo, kama nilivyosema awali, inaleta biashara ya umeme lakini pia inatuhakikisha kwamba tutakuwa na usalama wa kupata umeme hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer kwa wale waliochangia kwa mdomo. Napenda nimhakikishie ndugu yangu kwamba Longido hawakukosa lolote lile, kwamba wao sasa hivi hawana umeme.

Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote zinapata umeme, Makao Makuu ya Majimbo yanapata umeme na maeneo mengine muhimu yote yanapata umeme. Ndio maana basi, kwa ushahidi wenu ninyi wenyewe mmepitisha hapa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Umeme Vijiji na Wakala wa Umeme Vijiji na hatua hizi nyingine ambazo tunachukua siku hadi siku kuhakikisha kwamba nchi yetu, maeneo yote muhimu na Vijiji vyote vinapata umeme ili tuweze kuleta mapinduzi ya kimaendeleo hapa nchini. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie tu Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba hakuna wananchi walichokosa.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nichukue fursa hii labda pengine tuwaambie wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Michael Lekule kwamba kwa kweli kama ni suala la kufikisha Serikalini maombi ya umeme, Mheshimiwa Michael Lekule amekuwa akifanya kazi kubwa sana na wasichukue ukosefu wa umeme kutaka kumhukumu wakati wa uchaguzi. Ni suala linalotokana na uwezo mdogo wa Serikali wa kufikisha umeme kila mahali. Yeye kama Mbunge amejitahidi sana na kwa kweli pengine inakuwa bora zaidi wakiendelea naye maana anajua hata historia yenye nafasi hii kwa kweli niseme kwamba, sisi Wizarani tunafahamu jitihada kubwa ambazo amekuwa akizifanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, niseme kwamba, nakubaliana na zile njia mbadala ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge juu ya kutafuta njia za umeme nyingine kama za *solar* hasa mashulen ambapo njia kuu za umeme hazipo ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapata elimu ya kompyuta na mafunzo mengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Ruth Msafiri. Nakubaliana naye juu ya wazo la kuhakikisha kwamba tunashughulikia suala zima la bei nafuu ya umeme kama ambavyo wamesema Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya niliyoyaeleza, napenda niseme tena, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kutoa hoja na kuliomba Bunge lako Tukufu sasa likubali kuridhia Mkataba huu wa Tume ya Nishati ya Afrika yaani (*African Energy Commission (AFREC)*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Azimio la Kuridhia Makubaliano ya Kuanzishwa kwa Tume ya Nishati ya Afrika (The African Energy Commission (AFREC) liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge kama nilivyoeleza asubuhi kwamba majadiliano ya jumla yatakwisha saa saba mchana wa leo na sasa imebaki saa moja tu. Ni dhahiri kwamba hatutaweza kufanya shughuli zote zilizopo kwenye *Order Paper* ya leo. Nadhani kinachowezekana ni kuchukua hoja inayofuata tu ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, halafu wengine waliojiandaa kujadili hoja zinazoonekana kwenye *Order Paper* ya leo nafikiri wahifadhi michango yao mpaka hapo tutakapowatafutia nafasi nyingine. Tunaendelea na *Order Paper*, Katibu.

## **TAARIFA ZA KAMATI**

### **Mapendekezo Yaliyomo Katika Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa mwaka 2003 na 2004**

**MHE. JOB Y. NDUGAI (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA (MHE. ANNE S. MAKINDA)):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa kipindi cha mwaka 2003 na 2004. Nawasilisha taarifa hii ya Kamati kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Anne Makinda.

Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa Kanuni Na.101(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira katika kipindi cha miaka hiyo miwili ilitekeleza kazi zake kwa kuzingatia majukumu iliyopewa. Majukumu hayo ni:-

- (a) Kusimamia shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo hushughulikia mazingira, mambo ya Muungano na kuondoa umaskini.
- (b) Kusimamia shughuli za Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo hushughulikia Sekta za Maliasili, Utalii na Mambo ya Kale.
- (c) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii.
- (d) Kufuutilia utekelezaji unaofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii, nitajielekeza katika maeneo matatu. Kwanza, kazi zilizotekelawa na Kamati; pili, mpango wa baadaye wa Kamati na

mwisho, maoni ya Kamati. Kwa kuwa ripoti ya Kamati iligawiwa tangu juzi na sababu ya muda, nitasoma taarifa hii kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, katika kazi zilizoteklezwa na Kamati, Kamati ilichambua Miswada ya Sheria ikiwa ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Mazingira (*The Environmental Management Act*) ya mwaka 2004, Muswada uliowasilishwa kwenye Kamati na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ilikuwa ni kuridhia Maazimio ya Mikataba ya Ushirikiano wa Kimataifa na Mkataba mmoja ambao uliletwa hapa mwaka 2004 ni Mkataba wa Kuridhia Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika (*The Convention on Sustainable Management of Lake Tanganyika*) na Azimio hili lilipitishwa na Bunge lako Tukufu.

Maazimio yanayohusu Hifadhi ya Mazingira ndani ya nchi yetu yalikuwa ni manne. Azimio la Kuridhia Kuanzishwa kwa Hifadhi Mpya ya Taifa Saadani; Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Arusha; Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Kilimanjaro na Azimio la Kuridhia Kuanzishwa kwa Hifadhi Mpya ya Taifa Kitulo. Maazimio yote haya yalipitishwa.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba Azimio la Kuridhia Upanuzi wa Hifadhi ya Ziwa Manyara liliowasilishwa mbele ya Kamati yetu, lakini halikufanyiwa uamuzi, likarudia huko huko kwa sababu lipo tatizo la mipaka. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa viongozi na wananchi wa eneo husika wanashiriki kwa ukamilifu katika kuamua na kumaliza suala la mipaka ya Hifadhi hiyo ili liweze kuletwta Bungeni na kupitisha Azimio kuhusu Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilishiriki katika Mikutano mbalimbali katika nyakati tofauti kwa lengo kuongeza upeo wa Wajumbe wa Kamati katika maeneo yanayohusu Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Mikutano iliyofanyika ni pamoja na Mkutano ambao ulifanywa kati ya baadhi ya Wajumbe wa Kamati yetu na Wajumbe wa Kamati ya Mazingira na Ulinzi wa Maliasili (*Environment and Resource Protection Committee*) ya Bunge kutoka Bunge la Jamhuri ya Watu wa China.

Mkutano wa pili ulikuwa ni kati ya Wajumbe wa Kamati na Ujumbe wa Shirikisho la wenyewe Viwanda Tanzania kuhusu Uharibifu wa Mazingira Unaosababishwa na Kuzagaa ovyo kwa Mifuko ya Plastiki Nchini; Kamati iliagiza Serikali itayariske utaratibu wa kudhibiti uzagaaji wa mifuko hiyo nchini.

Mkutano wa tatu ulikuwa kati ya Kamati na wauzaji au wasafirishaji wa mazao ya maliasili na hasa magogo ndani na nje ya nchi. Kamati iliwaagiza wafanyakishara wazalendo wa magogo kuunda ushirika wao ili waweze kuwa na sauti ya pamoja.

Mkutano wa nne ulikuwa wa kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za Mashirika ya Umma pamoja na taarifa za ukaguzi wa hesabu kwa miaka husika. Mashirika yaliyohusika ni Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*), Bodi ya

Utalii Tanzania (*TTB*), Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*), Shirika la Makumbusho ya Taifa (*National Museums*), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (*TAFIRI*) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (*TAFORI*).

Pia Kamati ilipata fursa ya kupokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2004/2005 kwa Ofisi ya Makamu wa Ofisi na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara za kukagua shughuli za Kamati. Katika kipindi hicho, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara ndani na nje ya nchi kukagua utekelezaji wa mipango/miradi mbalimbali. Miradi iliyo tembelewa ilihusu usimamizi wa hifadhi ya mazingira, miradi ya Muungano, miradi ya kuondoa umaskini na Matumizi endelevu ya maliasili.

Ziara ya kwanza ilikuwa katika Mikoa ya Tanga, Arusha na Manyara ambayo ilifanyika kati ya tarehe 28 Machi na tarehe 07 Aprili, 2004. Katika Mkoa wa Tanga Kamati ilikwenda kuona pamoja na mambo mengine, tatizo la uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji unaofanya na wachimbaji wa madini wadogo wadogo na wakubwa waliovamia hifadhi ya Msitu wa Asili wa Amani. Kamati ilitoa mapendekezo kwa kuishauri Serikali kupiga marufuku mara moja uchimbaji haramu wa madini katika hifadhi ya msitu wa Amani.

Kamati ilipokuwa katika Hifadhi ya Taifa Ngorongoro ilijifunza mambo mengi kuhusu mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro. Wakati Hifadhi hii inaan zishwa, kulikuwa na wakazi wachache sana wa asili ndani ya hifadhi hiyo mwaka 1959. Hivyo, ilitarajiwu kuwa kadri muda unavyopita wananchi hawa wangekuwa wanapungua kwa wao kuhamia kwenye Miji/Vijiji nje ya hifadhi. Ukweli ni kuwa, hifadhi hiyo sasa imevamiwa na makundi makubwa ya wananchi na mifugo yao na wengine wanalima ndani ya hifadhi. Kamati inashauri kuwa huo Mkataba ulioanzisha hifadhi hii ni vizuri ukaangaliwa upya kwa lengo la kuona ni mabadiliko gani yanaendelea kutokea na nini kifanyike kuinusuru hifadhi hii ambayo ni urithi si wa Tanzania tu, bali wa dunia nzima.

Pia, Kamati ilikuwa katika Mkoa wa Manyara kwenye Migodi ya Tanzanite kwenye Tarafa ya Mererani. Kamati ilibaini kuwa maeneo mengi yana uchafu wa aina mbalimbali uliozagaa, hususan mifuko ya chupa za plasikiti. Katika machimbo ya Mererani maeneo mengi yapo wazi kutokana na miti mingi kukatwa ovyo. Kufuatana na sheria mpya ya mazingira wamiliki wa migodi wanatakiwa kuzingatia usafi na uhifadhi wa mazingira.

Pia, watoto wadogo wenye umri kwa kwenda Shule wameajiriwa kwenye machimbo hayo. Kamati iliwasaka wamiliki wa migodi, kutowaajiri kabisa watoto hao na badala yake kuwarudisha makwao ili wazazi au walezi watakiwe kuwapeleka Shule.

Hata hivyo, Kamati iliwasaa wachimbaji wote wa madini katika maeneo ya Mererani kujikinga na janga kubwa la *UKIMWI*.

Ziara nyingine ilifanyika Zanzibar ambapo Kamati ilitembelea miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inahusu Muungano, masuala ya mazingira, kuondoa umaskini na Hifadhi ya Maliasili. Kamati iliona maandalizi ya ujenzi wa Ofisi ndogo ya Bunge Zanzibar katika kiwanja cha maeneo ya Tunguu. Pia, iliweza kuona uendeshaji wa soko jipya la Mwanakwerekwe na hifadhi ya msitu wa jirani na maeneleo mengine.

Ziara ya tatu, ilikuwa katika Mikoa ya Pwani, Wilaya za Bagamoyo na Kisarawe. Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Wilaya ya Bagamoyo katika Kituo cha Mambo ya Kale. Hapa ni mahali ambapo watumwa kutoka Bara walikuwa wanasafirishwa pale kwanza kabla ya kwenda Zanzibar na baadaye sehemu nyingine za dunia. Pia, Kituo cha Kaole kwenye magofu ya himaya ya Kiarabu na makaburi yao. Himaya hiyo ilijengwa mnamo karne ya 13 na 14. Pia, Kamati iliona Makumbusho ya Kanisa la *Roman Catholic* ambalo lilijengwa mnamo mwaka 1868 pale Mjini Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, ziara ya nne, ilikuwa katika Mikoa ya Tabora na Rukwa. Katika Mkoa wa Tabora, hususan katika Wilaya ya Tabora Mjini, Urambo na Sikonge, wananchi katika maeneo hayo wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na uvunaji wa rasilimali za maliasili ambazo hufanywa bila kuzingatia uhifadhi wa mazingara. Hivyo, upo uharibifu wa mazingira kwa ukataji miti ovyo na kilimo cha kuhamahama na uchomaji wa misitu.

Matokeo ya vitendo hivyo ni kuwa, baadhi ya vyanzo vya maji vimekauka, mabwawa ya maji na mito yamejaa matope na mchanga, upepo mkali wenye kung’oa mapaa ya nyumba sasa ni zoezi la kawaida, mifugo inasababisha mmomonyoko mkubwa sana wa udongo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo ya uharibifu wa mazingira, Kamati iliwasa Viongozi wa Mkao wa Tabora, Wilaya na Vijiji vilivyotembelewa kuweka mikakati madhubuti kumaliza kabisa matatizo hayo sugu katika maeneo yao. Wananchi wapewe elimu kuhusu hifadhi ya mazingira. Wadau mbalimbali washirikishwe katika shughuli za uhifadhi wa mazingira kuanzia ngazi ya vijiji, Wilaya hadi Mkao.

Mheshimiwa Spika, tukiwa Tabora wananchi walimlalamikia Afisa Wanyamapor ambaye alikuwa Meneja wa Mradi wa Pori la Ungara kuhusiana na kuharibu mahusiano mema kati ya hifadhi na wananchi. Tunafurahi kusema kuwa, Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Maliasili na Utalii wamekwishachukua hatua ya kumwondo Afisa huyo.

Mheshimiwa Spika, katika Mkao wa Rukwa, Kamati ilitembelea Wilaya ya Mpanda ili kuona pamoja na mambo mengine, Hifadhi za Misitu na Hifadhi za Wanyamapor, yaani *Game Controlled Areas*. Maeneo haya yako katika Tarafa/Vijiji vya Katumba, Nsanda, Kambuzi, Uruira na Hifadhi ya Katavi. Aidha, uharibifu wa mazingira katika maeneo hayo ya Wilaya ya Mpanda hautofautiani na wa kule Tabora na mapendekezo yake yanafanana.

Ziara ya tano na ya mwisho ilifanywa katika nchi za Kenya na Uganda. Ziara hiyo ilikuwa ni ya kuzunguka Ziwa Victoria . Aidha, ilikuwa na lengo la kujionea hali halisi ya utekelezaji wa Mradi wa Kusimamia Uhifadhi wa Mazingira ya Ziwa Victoria, yaani *the Lake Victoria Environmental Management Project*.

Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia na sasa unaelekea katika awamu ya pili kwa ufadhili wa Benki ya Dunia hiyo hiyo. Mradi huu umegawanyika katika vitengo mbalimbali, vikiwemo:- upandaji miti katika vyanzo vya maji, matumizi bora ya ardhi, udhibiti wa uchafu utakao majumbani na viwandani unaoingia Ziwan, usimamizi wa maeneo chepechepe, ufuatiliaji wa ubora wa maji; kuondoa magugu maji, kuzuia uvuvi haramu, kusaidia miradi midogo midogo ya jamii na kujenga uwezo wa Watendaji, yaani *capacity building*.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kushirikiana na Uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Maliasili na Utalii, wamekubaliana kwamba katika suala la Kuondoa Umaskini, Muungano, Maliasili na Utalii na Mambo ya Kale kutekeleza kazi zifuatazo, katika kipindi kinachokuja.

Kutembelea Mkoa wa Morogoro ili kujionea hali halisi ya uharibifu wa mazingira kutokana na Viwanda Mjini Morogoro na hali ya Misitu ya Uluguru na Udzungwa; Kutembelea migodi ya Mwadui, Nzega na Tunduru; Kutembelea Mradi wa Ushirikishwaji Wananchi katika Usimamizi wa Mazingira unaoitwa *PERM*; Kutembelea eneo la Mradi wa Umeme wa Kihansi kuona hali ya vyanzo ya Kihansi; Kutembelea Dar es Salaam ili kuona “*Oxidation Ponds*”; Kutembelea Mji wa Kigoma ili kuona jinsi maji machafu yanavyoingia Ziwa Tanganyika; Kuchambua mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2005/2006 yatakayowasilishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Pia, Kuchambua taarifa za ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii na kutembelea Hifadhi mbalimbali za Mbuga za Wanyamapori ili kuona utekelezaji wa shughuli za utalii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya kina kuhusu shughuli zilizofanywa na Kamati katika kipindi husika, sasa naomba kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, kuweka bayana mambo ambayo Kamati ingependa kuona utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uhifadhi wa Mazingira, tunaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais kutekeleza kwa dhati mikakati ya kudhibiti uchafu unatokana na mifuko ya plastiki, kwani madhara yake ni makubwa sana kwa binadamu, mifugo, mimea, wadudu na ardhi. Pia kuandaa utekelezaji wa Sheria Mama ya Mazingira kwa kuanza na elimu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Maliasili na Utalii, bado tunasisitiza na kuishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kudhibiti tatizo la ukataji ovyo wa

magogo, ikiwa ni pamoja na usafirishaji wake nchi za nje; la sivyo misitu ya nchi yetu itakwisha na hivyo kutuathiri kimazingira kijamii na kiuchumi. Ikiwezekana badala ya kusafirisha magogo, tuweke mkazo mkubwa kusafirisha mazao yaliyotengenezwa hapa ili kuongeza thamani na ajira kwa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tunapendekeza mikakati mahsusili iliyowekwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu uendelezaji wa Utalii nchini izingatiwe. Kamati inashauri Wizara hii na Taasisi zinazojishughulisha na Sekta hii kuhakikisha inaendelea kuboresha zaidi vivutio vyote vya utalii vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la Uhifadhi wa Mambo ya Kale, bado halijawekewa mikakati madhubuti. Maeneo mengi nchini yaliyo na kumbukumbu za Mambo ya Kale hayatunzwi vizuri wala kuandikwa historia zake. Pale ambapo panatunzwa, watumishi wake ni wachache, hawana vitendea kazi na wala huduma za kijamii za kutosha. Kwa hiyo, tunaishauri Wizara ya Maliasili na Utalii kutoa kipaumbele katika Sekta hii ya Mambo ya Kale, kwani ufanisi wake unatoa tija kwa upande wa utalii na pia kwa upande wa kutoa elimu ya historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine linahusu masuala ya kuondoa umaskini. Kamati inasisitiza kuwa, nafasi ya Waheshimiwa Wabunge katika kusimamia mkakati huu wa kuondoa umaskini uwekwe bayana, kwani wao ndio wanaohusika na uwakilishi wa wananchi maskini wakati wote. Kupitisha Bajeti Bungeni na kushiriki kwenye Vikao vya Halmashauri kama Madiwani ni muhimu. Lakini wakati umefika wa kutambua nafasi ya Mbunge katika mkakati mzima wa kuondoa umaskini kwa kuwa na majukumu yaliyo wazi hasa katika kutoa elimu kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la mwisho ni kuhusu masuala ya Muungano. Kamati inasisitiza utekelezaji wa Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa William Shellukindo, ipewe nyenzo, Ofisi na ianze kufanya kazi yake kama ambavyo Katiba inawataka. Ushirikiano baina ya Wizara za Muungano na zile za Serikali ya Mapinduzi yaendelezwe ili kuondoa kero mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Kamati hii katika kutekeleza shughuli zake yametokana na ushirikiano wa karibu sana na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hizo, Mashirika ya Kimataifa kama vile Benki ya Dunia, *Africare*, *Canadian Parliamentary Centre* na kadhalika. Hawa walitusaidia sana kuandaa mpango wa miaka mitano wa shughuli za Kamati ambao sasa umefikia mwaka wa tano katika taarifa hii kama tulivyoainisha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wetu wote kwa ushirikiano mkubwa ambao Kamati yangu iliupata. Bila ushirikano huu, naamini tungkuwa na muda mgumu wa kufanya shughuli za Kamati. Shukrani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Mawaziri, Arcado Ntagazwa - Mbunge, Mheshimiwa Maokola Majogo - Mbunge, Mheshimiwa Zakia Meghji - Mbunge na Makatibu Wakuu, Bwana Mollel na Bibi Mary Mushi na Bwana Odunga, ambao wote walishiriki kwenye ziara zetu zote pamoja na wataalamu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani kubwa kwa ushirikiano tulioupara kutoka kwenye Ofisi yako. Tunapenda pia kumshukuru kwa namna ya pekee Katibu wa Kamati, Ndugu Sam Manamba ambaye sasa amestaafu, kwa kazi nzuri ambayo aliifanya kipindi chote alichokuwa bado mtumishi wa Ofisi ya Bunge. Tunapenda kumtakia maisha mazuri na yenye kheri baada ya kustaaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote 24 wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kwa kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwenye Kamati, hali ambayo imewezesha kutekeleza na kufanikisha kazi nyingi za Kamati yetu.

Aidha, naomba niwataje Wajumbe wa Kamati wafuatao:- Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Hassan Khatib, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa Aziza Ali, Mheshimiwa Shaibu Ameir, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Ali Juma, Mheshimiwa Sharifa Khamis, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Mathew Ole-Timam, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Mohamed Soud, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Issa Suleiman na Mheshimiwa Martha Wejja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumshukuru Mheshimiwa Anne Makinda kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya Kamati hii kwa niaba yake. (*Makofi*)

Mwisho, kabisa naomba kuwasilisha rasmi mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira katika kipindi cha mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia machache katika hoja hii ambayo imewasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia lile ambalo nimekusudia, kwanza, uniruhusu nichukue nafasi hii fupi nikupongeze wewe mwenyewe kwa ujasiri mkubwa na busara nyingi ambazo ulizitumia katika kuliruhusu lile suala la jana kuingia Bungeni na kuliweka hadharani. Kwa maana hiyo, badala ya kuonekana kwamba Bunge lako limepata aibu kubwa na nchi, mimi naamini kwa kuliweka wazi suala lile Bunge lako

linaheshimika sasa zaidi kuliko kama jambo lile lingefanywa kisirisiri. Nakushukuru sana na ninakupongeza Mheshimiwa Spika. (*Makofî*)

Hii inatoa fundisho kwa wale ambao wanateua viongozi wao kwa kuwaokota. Nakipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa utaratibu wake mzuri wa kuwachunja viongozi wake. Lazima viongozi wapite kwenye chekecheke wajulikane wanatoka wapi, wanafanya nini, wamefikia wapi mpaka wafike hapa tulipo. Siyo kumchukua kila mtu tu kumpeleka kwa wananchi na kumuingiza katika Bunge lako Tukufu, matokeo yake ni haya tuliyoyaona wote. Ninaamini kwamba huko tunakokwenda Vyama vingine vyâ Siasa vitaiga mfano wa Chama cha Mapinduzi kwa kutuondolea hii aibu ambayo kweli inasikitisha. Nakushukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lile ambalo nataka kuchangia ni suala maalum kidogo kwa Jimbo langu. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii analifahamu, tumezungumza naye, lakini naomba nilizungumze hapa ili niweze kupata majibu ya wazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu na Wilaya yetu ya Lushoto tunalima miti inayoitwa miwati. Miwati ni miti ambayo mazao yake ni magome yake, ndiyo yanayouzwa na kuualetea faida wakulima wale wanaolima zao hilo la miti.

Mheshimiwa Spika, pale Mjini Lushoto tuna kiwanda cha maganda. Kiwanda kile kimebinafishwa kwa Mtanzania mmoja ndugu yetu. Huyo Mtanzania mwenye kiwanda kile pia ana mashamba yake ya miti ya miwati. Muda wote amekuwa akitoa bei ndogo sana kwa wakulima wale wa maganda ya miwati. Bei yake kwa kilo moja ya maganda ya miwati yaliyokauka, yeze anachukua yaliyokauka ni Sh.30/= mpaka Sh.35/= kwa kilo moja.

Amekuja mfanyabiashara mmoja kutoka nchi jirani ya Kenya amepita Wizarani amepata vibali vyote na barua zote za kumruhusu kununua maganda na kuyasafirisha kwenda kuyauza kule *Athi River Kenya*. Huyu mfanyabiashara wa Kenya anawalipa wakulima wa Jimbo la Mlalo na Lushoto kilo moja kwa Sh.50/= tena kwa maganda mabichi na anayasafirisha kutoka Lushoto kwenda Kenya. Maganda mabichi yana uzito mkubwa zaidi kuliko yaliyokauka. Huyu bwana anatoa Sh.50/= kwa kilo moja. Lakini huyu mwekezaji ndugu yetu anayeyaokota maganda hapo nje na kuyaingiza kiwandani anawalipa wakulima wale Sh.30/= mpaka Sh.35=/. Kwa bahati mbaya sana nitategemea jibu kutoka kwa Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Spika, majuzi mfanyabiashara huyo amepewa barua ya kusimamishwa kufanya kazi yake ile. Kisingizio ni kwamba, kiwanda kile cha mwekezaji binafsi hakina malighafi ya kutosha. Kwa hiyo, malighafi inayotoka kwenye mashamba binafsi ya wakulima ndiyo ipelekwe kwenye kiwanda kile hata kama bei ile wanayolipwa ni ya kunyonywa.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa kwenye Bunge lako Tukufu tumepewa Semina nyingi sana kuhusu kupambana na umaskini. Kupambana na umaskini kusema kweli ni wakulima wetu kule Vijiji. Hawa wakulima wamepata soko nzuri la zao la maganda

na wakati mfanyabiashara huyu anapobinafsishiwa kiwanda hiki, hakuingia Mkataba na watu hawa wala Serikali haikukubaliana na wakulima binafsi hawa kwamba lazima wauze pale kwenye kiwanda chake. Lakini kwa mtazamo tu wa kupambana na umaskini; Je, inakuwaje huyo mfanyiabashara binafsi mwenye kiwanda chake pale alindwe na wananchi wale wanyonywe? Sasa haya tunayozungumza ya kuondoa umaskini tutayafikisha wapi?

Mheshimiwa Spika, Semina zilizotolewa hapa ni nyingi, tumejua juu ya kitu kinaitwa *MKURABITA*, tumejua juu ya kitu kinaitwa *MKUKUTA* na hiyo yote ni mikakati ya kulenga kupunguza umaskini kwa wananchi wetu. Sasa nitaomba majibu, haya mashamba binafsi ya wakulima wanalazimikaje kupeleka maganda kwa kunyonywa kwenye kiwanda binafsi cha mtu huyo aliyeewekeza? Ninaomba Serikali ifikirie tena. Sababu ninaambiwa maganda haya yanatakiwa yapate thamani kwa kupita kwenye kiwanda. Lakini hata hiyo mali itakayozalishwa yenyе thamani kupertia kiwandani wakulima hawa watafaidika namna gani? Ninaiomba Serikali na Wizara inayohusika kama ni lazima wakulima hawa wauze zao lao kwenye kiwanda cha mzalendo huyo aliyenunua, basi kwa nini asikubali kulipa bei ile ambayo yule mfanyabiashara wa Kenya anawalipa hao wakulima. Kwa nini asikubali hilo? Kama hakubali, hawa wakulima wana lazima gani ya kupeleka kuuza mali yao kwenye kiwanda hiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hilo jambo naomba Serikali ilifikirie na itoe uamuzi, maana kule nyumbani wakulima wa miti hii ya miwati wamegoma kuuza maganda yao, wameanza kuandamana kwa Serikali na wanakataa kabisa tabia hii ya kunyonywa. Kama mfanyabiashara yule anataka maganda yao, basi aruhusiwe anunue yakiwa mabichi na kwa bei hiyo ambayo ananunua mfanyabiashara yule kutoka Kenya.

Pili, huyo mfanyabiashara kama anataka maganda ya watu hawa, basi aendelee kuzungumza nao kila wakati kwa kubadilishana mawazo kwa maana ya kuboresha bei ya zao hili la maganda.

Mheshimiwa Spika, mimi nilisimama dhahiri kusema hilo moja tu nikijua kwamba jambo hili linawakera Wapigakura wangu na wengi wamebadilika kabisa, wamekuwa wakali sana na hasa sasa tunavyoolekeea kwenye uchaguzi, hawaelewii maana ya Serikali kufanya jambo hili ni nini. Ninaomba majibu mazuri ya Serikali ili wananchi wale wa Jimbo la Mlalo na Wilaya ya Lushoto wawe huru kuuza mazao yao waliyolima wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi kule nyumbani sasa naanza kulima matunda yanayoitwa *apple*. Nimelima kiasi fulani na ninaendelea. Kesho kutwa mitunda yangu imekamilika inatoa mazao, nimepata biashara nzuri Mombasa, Nairobi au Kampala, halafu amekuja mtu ameanzisha kiwanda chake pale, hivi ninalazimika kwa sheria gani nimpelekee huyo mali yangu iliyotoka shambani kwangu badala ya kuuza kule ambapo ninaamini kwamba kuna bei nzuri zaidi kuliko hii? Hili ni soko huria sasa na kama ni soko huria watu wanashindana! Watu hawatumii vyombo vyaya dola kuwakandamiza watu wadogo ili waendelee kunyonywa! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ni hoja nzuri na imefanyiwa kazi vizuri. Lakini jambo hili tafadhali naomba nijibiwe.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Baadaye nitampa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili aweze kujibu.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika taarifa hii ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ya kuchangia katika taarifa ya Kamati hii. Kwanza, niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa jinsi ambavyo wametupatia taarifa ambayo imeonyesha umakini wa hali ya juu sana katika kazi waliyoifanya kwa kipindi chote hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunalo Ziwa moja kubwa linaitwa Ziwa Victoria ambalo tunalimiliki nchi tatu; Uganda, Tanzania na Kenya. Katika Ziwa hili, eneo la Tanzania mimi ni mmoja ambaye nikiwa Mbunge, basi ni Mbunge katika Visiwa vinane vinavyokaliwa na watu na viko 19 kwa ujumla katika lile Ziwa ambavyo ndani yake nina Kata mbili.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa na matatizo ya muda mrefu sana ndani ya lile Ziwa kuhusu usalama wa wavuvi katika Visiwa vyangu kwa kipindi kirefu. Kwanza, kuna watu wanaotokea nchi jirani kwa imani kwamba wanatokea nchi jirani kuja kupora samaki katika eneo la Tanzania. Kuna Kisiwa kimoja kinachoitwa Goziba ambacho ndicho chenye samaki wengi sana na Kisiwa cha Kerebe katika eneo langu. Kwa hiyo, mara nyingi kumekuwa kunatokea waporaji wanatoka nchi jirani na Kisiwa cha Goziba kiko karibu na mpaka wa Uganda. Kwa hiyo, kumekuwa na matatizo makubwa sana pale ya kuporwa kwa samaki na hali inayohatarisha hata maisha ya wavuvi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, inaonyesha kwamba upande wa Tanzania Ziwa letu halina ulinzi. Ni wavuvi wenyewe ambao wanajitegemea katika kujilinda wao wenyewe na kwa zana zao wenyewe na kwa nguvu zao wenyewe. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Wizara husika ione uwezekano wa kuweka meli ya ulinzi ili kuweza kulinda kwanza maliasili yetu. Lakini vilevile kuyalinda maisha ya wavuvi wetu na vyombo vyao katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, kuna lingine pia ambalo limekuwa likijitokeza katika maisha ya wakazi wa kule, nami napenda niliwasilishe ili na lenyewe lifanyiwe kazi na kupatiwa ufumbuzi. Ziwa Victoria sasa hivi wapo wavuvi wakubwa kwa maana kwamba wapo wavuvi wenye uwezo mkubwa waliopewa leseni za kuvua ndani ya lile Ziwa. Lakini vilevile kuna wavuvi wadogo waliokuwepo miaka mingi katika Visiwa hivyo hivyo. Lakini hali kwa ujumla siyo hali yenye amani, kunakuwa na ugomvi wa mara kwa mara kati ya wavuvi wakubwa na wavuvi wadogo na kwa kweli inatishia hata hali ya maisha na usalama wa maisha ya hawa hasa wavuvi wadogo wadogo. Wengi wamekufa tayari,

taarifa zinatolewa, lakini mtu akishakuwa amezamishwa anapopatikana mara nyingi ushahidi unapotea na wengine wanakimbia. Hali hii haileti amani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, kwa kweli isimamie hali ya kuweza kuona kwamba hali ya amani inakuwepo kati ya wavuvi wakubwa na wavuvi wadogo na kile tulichokikusudia basi, cha kuwaondolea umaskini Watanzania kwa kuongeza kipato, waweze kufaidika hata wale wavuvi wadogo wadogo katika Visiwa hivi vya Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Goziba na Kerebe kila wakati wana kilio. Hata nilipokuwa kule Jimboni nilipokea malalamiko ambayo niliomba Afisa Uvuvi aende akayashughulikie. Nashukuru sana kwamba aliweza kuyashughulikia vizuri na nikapata taarifa nzuri. Lakini ufumbuzi huo umekuwa ni wa muda tu, tukikaa tena kwa kipindi fulani pia kutatokea matatizo, hali ambayo kwa kweli inatuletea hali ya kutokuwa na amani.

Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ione uwezekano wa kutusaidia. Sisi tuko tayari kushirikiana nao tuweze kuwahamasisha wavuvi wadogo wadogo ikiwezekana na wenyewe wakubali wajunge pamoja ili waweze kupata nguvu ya kuweza kupigania haki zao. Lakini pia wapate nguvu ya kuweza kukabiliana na hao wavuvi wakubwa ili kufaidika na kazi wanayoifanya kule wasiwe vibarua ila nao wawe ni wafanyabiashara wadogo wenye kuvua na kuwauzia wale wavuvi wakubwa na kwa faida yao wao wenyewe.

*(Hapa umeme ulikatika kwa muda)*

**SPIKA:** Haya endelea.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, hilo naliwasilisha kama ombi kwamba ninaomba Wizara husika iweke ulinzi katika Ziwa Victoria kusudi kuweza kuweka hali ya amani kwa Watanzania na vilevile hali ya amani na hali ya kuweza kuhakikisha kwamba samaki hawaporwi ambavyo si kihalali. Lakini vilevile, kuhakikisha kwamba wavuvi wakubwa na wavuvi wadogo wanaishi kwa amani bila kuwa na ugomvi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ninalotaka nilizungumzie na lenyewe kwa ufupi ni kutokana na hali hiyo hiyo. Kwa sababu tayari sasa hivi Ziwa Victoria linatumika zaidi kibiashara na kwa kuwa wapo wavuvi wakubwa waliopewa vibali, basi unakuta wananchi wa kawaida kwa sasa hivi hawawezi kupata kitoweo ipasavyo, kwa sababu samaki wakubwa wanapovuliwa, kwanza wananchi wanawakimbilia wale wavuvi wadogo kuwauza ili waweze kupata faida. Kwa hiyo, unakuta hali ya kitoweo kwa wananchi wengine waliobaki ambao walizoea kupata kitoweo katika Ziwa inaendelea kuwa ni ya matatizo. Lakini wananchi hawakuzoea sasa kutumia samaki wa mabwawani na mabwawa yenyewe hayapo.

Kwa hiyo, naiomba Serikali katika kipindi kinachokuja, ielekeze tena nguvu zake upya katika kuhamasisha wananchi ili kuweza kuanza nikiite kilimo cha samaki kwa maana ya kwamba kuweza kuona wananchi wanaelekeza mawazo mapya katika hali ya maisha mapya. Kuwe na mabwawa ambayo wananchi wapatiwe utaalamu wa namna ya kuchimba, kufuga samaki ili kuweza kuhakikisha kwamba ile hali halisi haishuki. Lakini vile vile kuweza kuhakikisha kwamba mabwawa hayo yatawasaidia katika kupata samaki wengi wa kutosha wanaowamiliki wenyewe, wawasaidie katika biashara, waweze kuongeza kipato chao na hata waweze kutangaza maeneo kwa sababu ukishakuwa na biashara inayojulikana, lile eneo linajulikana kwa sababu ya ule wingi wa watu wanaokuja kufuata ile biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ambayo nimeyachangia, ninaomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kusema machache. Kwa kuzingatia muda, nijielekeze kwenye hoja moja tu. Hoja hii nimekuwa nikiipokea kwenye Jimbo langu lote kuanzia Misenyi hadi Kiziba. Hoja hii mara nyingi inatolewa na akinamama. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri anayehusika na Maliasili ni mama, kwa hiyo, atailewa kwa uzito unaostahili na baadaye matarajio yangu atayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja yenyewe ni kwamba wanyama waharibifu kwa siku za hivi karibuni wameongezeka kwa wingi. Wanyama hawa hasa hasa tumbili na wengineo wa jamii hiyo wana tabia moja kubwa kwamba wakishaona mazao yamelimwa na sasa yako katika hali nzuri wanajitahidi kwa kutumia nguvu kadri wanavyoweza kuvamia mashamba na kuharibu mazao hayo. Kwa hiyo, kero hii imekuwa kubwa na uwezo wa akinamama hao kupambana na wanyama hao ni mdogo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilitazame hilo. Kwa mfanu katika Halmashauri ya Bukoba tuna Afisa Wanyamaporinno na Afisa mmoja kwa Kata nne, ni dhahiri kwamba hawesi kupambana na wanyama hao amba ni wengi na wameongezeka zaidi kwa sera yetu nzuri ya kulinda mazingira na kulinda hao viumbe.

Mheshimiwa Spika, vile vile, kuna tatizo kubwa la upungufu wa risasi. Hata ukimpata huyu Afisa Wanyamaporinno, bado risasi ya kufanya kazi hiyo zinakuwa hazipo. Sasa naomba nitoe mapendekezo matatu ambayo naomba Mheshimiwa Waziri ayafanyie kazi. Kwanza, ni vizuri ukawepo utaratibu wa Afisa Wanyamaporinno kushirikiana na wanavijiji katika kupambana na wanyama hao.

Lakini la pili ni vizuri kuwaajiri Maafisa Wanyamaporinno wengi zaidi, kwa sababu kwa Halmashauri ya Bukoba na ukubwa wake kuwa na Afisa Wanyamaporinno mmoja, maana yake ni kwamba kazi hiyo inakuwa ngumu na wanyama hao wataendelea kuharibu mazao. Tatu, ni vizuri jitihada zikafanywa za makusudi kuongeza upatikanaji wa risasi. Kwa hayo, machache naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Mawaziri wawili watatoa maoni ya Serikali. Naanza na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, atafuatiwa Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Waziri wa Nchi mwenye dhamana ya Mazingira.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kujibu baadhi ya hoja zilizoletwa mbele yetu.

Kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, Mama Anne Makinda pamoja na Kamati nzima ya Maliasili na Mazingira kwa jinsi ambavyo kwa kweli tumefanya kazi. Tumefanya kazi vizuri sana kwa ukaribu sana na mawazo yao mengi tumeyachukua na kuyafanyia kazi. Ndiyo maana utaona yale ya mwaka 2003 mengi kwa kweli yameanza kutekelezwa na hata yale ya mwaka 2004 pia nayo yameweza kutekelezwa. Kwa mfano Afisa yule wa Ughala ambaye kama alivyoeleza Mtoa Hoja ameondoshwa katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia suala hili la uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji ambao unawafanya wachimbaji wa madini wadogo wadogo na wakubwa waliovamia Hifadhi ya Misitu wa Asili wa Amani. Kamati hii ilitoa mapendekezo yao nasi tukafanya kazi pamoja na kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini na Uongozi wa Mkoa na Wilaya.

Tunashukuru kwamba Waziri wa Nishati na Madini ameshatoa tangazo na kupiga marufuku uchimbaji wa madini katika *Amani Natural Reserve*. Kwa hiyo, hilo limetekelvezwa. Tunajua kwamba kuna wavuvi wadogo wadogo wachache ambao wamebakia na tunashirikiana na Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Uongozi wa Mkoa na Wilaya ili waweze kuondolewa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala hili la Ngorongoro ambapo wananchi wengi walioko katika maeneo hayo wanaharibu mazingira kwa kulima na kadhalika. Nalo hilo tumelichukua pamoja na mawazo ambayo yaliyotolewa na Kamati hii ya Maliasili na Mazingira. Lakini pia nielezee kwamba kuna baadhi ya wananchi ambao walikuwa Ngorongoro, hivi sasa wangependelea kulima. Pale tunasema kwamba inaruhusiwa vishamba vidogo vidogo. Kwa hiyo, Ngorongoro imeamua kununua eneo kubwa la shamba ili wale ambao wangependelea kulima, basi waweze kwenda katika maeneo hayo. Kwa hiyo, hilo nalo nasema tunalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, suala la kudhibiti tatizo la ukataji ovyo wa magogo na usafirishaji wa nje, nalo tumeshikiriana na Kamati hii ya Maliasili na Mazingira. Hata wazo lao la kwamba wafanyakishi wa magogo waunde Chama chao, napenda kutoa taarifa kwamba wafanyakazi wa magogo hao wameunda Chama chao na tumekuwa na ushirikiano mkubwa kati yao na Wizara yetu ya Maliasili na Utalii.

Lakini pia niseme kwamba, Wizara imepokea mapendekezo ya Kamati na tokea tarehe 01 Julai, 2004 kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na.14 ya mwaka 2002 Wizara imesimamisha usafirishaji wa magogo ya misitu kwenda nchi za nje na pia imesitisha

ukataji wa miti ya asili tokea tarehe 01 Oktoba, 2004 hadi tarehe 30 Juni, 2005 ili kuweza kufanya tathmini, yaani *inventory* na pia kujua mahitaji halisi ya uwezo wa matumizi ya viwanda vya mbao hapa nchini ili kuoanisha na matumizi ya uvunaji endelevu. Suala la vivutio vya utalii nalo pia tunazidi kulishughulikia na tunapenda kushukuru kwa mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na masuala haya ambayo yalitokana na uchangaiji wa Waheshimiwa Wabunge. La kwanza ni juu ya mchang'o uliotolewa na Mheshimiwa Charles Kagonji kuhusu miwati. Labda nielezee kwamba Mheshimiwa Kagonji wiki iliyopita alizungumza na mimi na leo asubuhi aliniandikia *ki-memo* na kama desturi yangu nilimjibu *memo* yake. Sasa nafikiri ameipata.

Aliniuliza; Je, umelishughulikiaje? Nikasema nimeshughulikia kikamilifu wakati nikiwa Dar es Salaam na tumekubaliana na mawazo yake. Kwa hiyo, labda alitaka nilizungumze wazi wazi hili hapa ili liweze kusikika. Lakini niseme kwamba hapa hapa tumezungumzia juu ya kuongeza thamani. Kamati ya Maliasili na Mazingira imezungumzia kwamba ni budi tuongeze thamani ya Maliasili yetu. Kwa hiyo, hata suala lile la magogo nalo tunalozungumza ni suala zima la kuongeza thamani. Ndiyo maana sheria ile ya mwaka 2004 inasema tusisafirishe magogo, lakini tusafirishe kitu ambacho kimethaminiwa zaidi. Kwa sababu unapata fedha zaidi, lakini pia unaleta ajira kwa wananchi waliokuwa hapa.

Suala hili ni kweli lilijitokeza hapo Lushoto na pale ni kweli kuna kiwanda ambacho Mtanzania amenunua na kwa kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza thamani hapa nchini ilionekana kwamba, basi miwati au kwa maana ya majani haya yasiweze kusafirishwa nchi za nje. Lakini baadaye tukapata hiyo taarifa kwamba majani haya ambayo huyu Mkenya amenunua yametokana na shamba la wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tulipata matatizo huko nyuma na hata vyombo vya habari viliandika kwamba kuna baadhi ya watu mbaao wanakata majani, haya ya miwati hata katika maeneo ya Hifadhi za Taifa kwa mfano Manyara na kadhalika. Kwa maana hiyo, kwa kweli ilibidi na sisi pia tuchukue hatua. Lakini baada ya kupata taarifa hiyo na baada ya kupata taarifa kwamba huyu mwenye Kiwanda hivi sasa anawapa fedha za chini, yaani anawapa Sh.20/= kwa kilo moja badala ya Sh. 50/= kwa kilo moja tukaamua kwamba, basi huyu Mkenya aweze kusafirisha majani haya ambayo aliyانunu na tulitaka kujua ni kiasi gani, lakini mpaka hivi sasa Mkenya huyu hakutuarifu ni kiasi gani, kilo ngapi ambacho alikuwa anataka kusafirisha. Lakini tumesharuhusu hilo na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kagonji kwamba hilo tumelishughulikia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Ruth Msafiri, amezungumzia suala la ulinzi katika Ziwa Victoria. Napenda kumhakikishia kwamba bajeti yetu itaongeza maboti ambayo yatakuwa yanazunguka *Lake Victoria* upande wa Tanzania. *Lake Victoria* ni kubwa sana ukifananisha hata na Kenya na Uganda, lakini hilo tutalifanya. Lakini pamoja na hayo, tunatarajia tutumie hata ndege za kuweza kuruka juu na kuangalia masuala haya ya uhalifu.

Suala la kitoweo kwa maana ya mabwawa ya samaki nieleze kwamba hata katika sera yetu na Sheria ya Uvuvi imetilia mkazo mkubwa juu ya mabwawa ya samaki. Natumaini Waheshimiwa Wabunge pia watatusaidia katika kuhamasisha wananchi katika jambo hili. (*Makofi*)

Lingine la mwisho, ni la Mheshimiwa Kamala. Nasema tutalishughulikia kama vile tunavyosughulikia siku zote. Lakini ningependa kusema kwamba na Halmashauri ambazo zina jukumu la kuajiri Afisa Wanyamapori hawa basi watusaidie nao pia. Kwa sababu wakati mwingine unakuta katika Halmashauri hizi hakuna Maafisa Wanyamapori, kwa hiyo, inakuwa vigumu sana. Kwa hiyo, tushirikiane kwa pamoja na sera yetu inazungumzia juu ya ushirikiano na wananchi wote kwa pamoja. Nafikiri tutaweza kufanikiwa tukifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niunge mkono Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira inayosema Bunge likubali kupokea na kutekeleza mapendekezo yaliyomo.

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi kwa kuwa ndio mara ya kwanza kusimama hapa katika Mkutano huu, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole na rambirambi kwa ndugu, jamaa na marafiki wa Marehemu Balozi Ahmed Hassan Diria na Mzee wetu Balozi Paul Bomani. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, la pili napenda niishukuru Kamati ya Maliasili na Mazingira. Kamati wameishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano lakini sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tunawashukuru zaidi kwa sababu katika kutimiza wajibu wao wa kikatiba wa kushauri, kusimamia shughuli za Serikali wametuwezesha kufanya mambo mengi kwa pamoja na sisi katika nchi yetu ndio mfumo wa uongozi wa pamoja. Kwa hiyo, kwa kweli tunafarijika na ni kweli kabisa kuwa tumetiwa moyo na hamasa kwa jinsi ambavyo Kamati hii imeshirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kutimiza wajibu wetu katika kuwatumikia Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, napenda pia nao wapokee shukrani za Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia mimi niliyesimama hapa. (*Makofi*)

Lakini pia, napenda nimpongeze kwa kweli Mheshimwia Job Ndugai kwa jinsi alivyowasilisha Taarifa ya Kamati hii kwa namna ambayo inapendeza na lazima nikiri kwamba ni uwasilishaji mahiri na makini sana. Napenda kumshukuru na kumpongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina mambo mengi ya kusema, kwa sababu wewe binafsi unatuambia taarifa zinapofikishwa Mezani, kwa kweli Serikali inazifanyia kazi.

Ningependa kutoa mfano kwamba, katika taarifa hii Kamati ilipotembelea ule Msitu wa Hifadhi wa Amani kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii yalitolewa mapendekezo mahsusini na kuthibitisha kile unachokisema kwamba Serikali inaanza kufanya kazi mapendekezo ya Kamati niliyonayo hapa. Ni taarifa ya wataalamu wa Wizara zetu hizi, wakisema nini kifanyike kutokana na mapendekezo na ushauri wa Kamati. Kwa hiyo, kwa kweli kama nilivyosema, tunawashukuru, tumeshaanza kufanya kazi na nina hakika hata lile tangazo lililotoka kwenye Wizara ya Nishati na Madini, ilikuwa ni utekelezaji wa Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapenda kukushukuru wewe binafsi kwa kutukumbusha kwamba taarifa zinazofikishwa hapa ni kwamba Serikali inazifanya kazi na ushahidi ni taarifa niliyonayo hapa mkononi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ushahidi wa pili, Kamati hii ilipotembelea kule Hifadhi ya Ngorongoro, ni kweli waliona kwamba kilimo kimeanza kufanyika katika eneo lile tofauti na bustani na ni kweli kwamba pale mwanzoni nakumbuka wakati nikiwa Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwanza ilikuwa hairuhuswi kulima hata kidogo kwa sababu ilitarajiwa wakazi wa kule wawe wanapelekewa chakula. Lakini baadaye, ikaonekana jambo hili haliwezekani. Sasa maagizo yaliyotolewa na Kamati yamefanyiwa kazi vile vile na hii ni barua ya Mhifadhi Mkuu wa *Ngorongoro Conservation Area Authority* ambayo inaeleza ni hatua gani zilichukuliwa baada ya mapendekezo ya Kamati. Lakini kule ambako ilikuwa imepatikana ardhi mbadala kwa ajili ya wananchi ambao wangependa kwenda kulima, mambo ya binadamu wanasema mbuzi wa maskini hazai. Ilipokuwa ardhi imepatikana, yakatokea mapigano baina nadhani ya makabila fulani kwa eneo lile. Sasa wale waliokuwa wametoa ardhi wakasema aah, ardhi yetu hatutoi mnaweza mkatuletea ugomvi hapa. Sasa tumerudi pale pale. Lakini hatua za kutekeleza agizo, ushahidi ni huu kwamba zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka niseme haya machache. Labda katika taarifa yenyewe nigosie ukurasa wa 27 anapozungumzia mapato ya Makampuni yanayosindika minofu ya samaki na kila wanachokipata wananchi wetu kwa maana ya mtazamo ule wa kupambana na umaskini.

Nilikuwa nasoma kitabu kimoja kinachozungumzia juu ya Makampuni haya makubwa yanapokuwa na uwezo mkubwa wa kipato ukilinganisha na wananchi wa karibu. Lakini wakati mwingine kuna kitu wanatia *cooperative responsibility* kwamba Mashirika yale nayo yana wajibu. Kama mnafanya shughuli zenu na wananchi wanaoishi maeneo yale jirani mnapofanyia shughuli hawaridhiki dhahiri, kwanza hamtapata nguvukazi, lakini ya pili, hamtakuwa na raha ya kuendesha shughuli zenu.

Kwa hiyo, hili nalo la wananchi kutambua kwamba Makampuni yale yana wajibu kwao na Makampuni yenyewe kutambua kuwa yanawajibika kufanya shughuli zinazowanufaisha wananchi yanatupa nafasi kupitia wananchi wetu kusisitiza haki zao za msingi. Nilitaka niseme kwamba hata pendekozo lao walipolitaja hapa, ni kweli si peke

yao Kamati hii, lakini ni wazo ambalo linazungumzwa sasa hivi hata katika ngazi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie katika mambo machache niliyoyasema. Nimalizie hili lililotokea hapa Bungeni jana wakati tukijadili Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Baadhi yetu sisi wengine tulivyokuwa tunalelewa ilivyokuwa inatolewa taarifa hapa Bungeni unajiona kama mnyonge kwa mambo kama haya. Lakini jambo la kujivunia ni kwamba kwa utaratibu wa nchi yetu linapotokea jambo la ovyo hatusiti kulikemea, kulaani na hatusiti kuchukua hatua ambazo ziko ndani ya uwezo wetu. Kwangu binafsi ambaye nina bahatika katika kulitumikia Taifa langu, kusafiri nchi za nje mara nyingi katika Mikutano hii ya Mazingira, mambo ya namna hii yanatia kichefuchefu, yanakutia unyonge kwamba sasa utaonekana kama mionganoni mwa hawa watu wasiopendeza katika jamii ya Watanzania.

Lakini lililotokea jana kwa kulikemea, kulilaani na kulitolea adhabu kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, mimi nina hakika hata jamii ya Kimataifa ambayo pengine kabla ya jana walifikiri sisi ni wababaishaji, nadhani limetujengea heshima kubwa na nadhani nchi yetu inaaminika zaidi kwa hilo na kwa kweli tumwombe Mwenyezi Mungu mambo kama haya wale wenye mwelekeo wa namna hiyo atuepushe wasiingie katika jengo hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Basi, mpaka hapo ndio tumeifikia mwisho wa kipindi cha asubuhi cha Kikao cha leo. Kama nilivyosema, tutakaporudi saa 11.00 jioni, ni hoja ya kuahirisha Bunge. Kwa ajili hiyo basi, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hiyo saa 11.00 jioni.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Mapendekizo yaliyomo Katika Taarifa ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kwa Mwaka 2003 na 2004 yalikubaliwa na Bunge*)

(*Saa 06.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zilizokwu zimepangwa kufanyiwa kazi na Bunge katika Mkutano wako wa 19 sasa zimemalizika.

## **KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maeleo machache niliyonayo, naomba na mimi nitumie fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge

wenzangu kutoa pole kwa familia na wananchi wa Jimbo la Rahaleo, kutokana na kifo cha aliyejekuwa Mbunge wao, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria. Kwetu sisi tuliofanya kazi naye tutamkumbuka kwa busara zake na jinsi alivyoweza kila mara kutetea umoja na mshikamano siyo wa Watanzania tu, bali wa Bara lote la Afrika. (*Makofî*)

Marehemu Balozi Diria alikuwa muumini mkubwa wa Muungano wetu na kila mara alitetea kwa hoja zenye nguvu umuhimu wetu sisi kama Taifa wa kuendelea kujenga na kuuiamarisha Muungano. Tutaendelea kumkumbuka kwa utumishi wake kwa Taifa letu na tutaendelea kuimarisha Muungano na umoja wetu ili kumuenzi Mheshimiwa Marehemu Diria.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki vilevile, tumepatwa na msiba mwingine wa kumpoteza Mzee wetu, Balozi Paul Bomani. Marehemu Balozi Bomani alikuwa mmoja wa Wazee mashuhuri wa Taifa letu. Busara hekima na uongozi wake umempambanua kama kiongozi mahiri aliyeweza wakati wote kutekeleza majukumu aliyokabidhiwa kwa upeo wa hali ya juu. Balozi Bomani aliweza kutumia nguvu kubwa ya ushawishi aliyokuwa nayo kujenga uongozi wa pamoja uliowezesha Taasisi alizokabidhiwa kuongoza na kutekeleza majukumu yake. Kwetu wana CCM tumempoteza mdhamini wa Chama chetu aliyejekuwa nguzo katika kusimamia na kutetea misingi ya Chama. Tutamkumbuka kwa utumishi uliotukuka kwa Taifa letu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote hao wawili mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Serikali imejibu maswali 128 ya Waheshimiwa Wabunge na mengine mengi ya nyongeza. Aidha, jumla ya Miswada mitano imepitishwa pamoja na kuridhiwa kwa Maazimio manne. Bunge lako vile vile limepokea, kujadili na kuitisha taarifa nne za Kamati za kudumu za Bunge. Moja ya Muswada uliopitishwa na Bunge lako Tukufu ni Muswada wa Sheria ya Kutumia Stakabadhi za Mazao yaliyowekwa kwenye maghala wa mwaka 2005. Lengo la Muswada huu ni kuwawezesha wakulima, Vyama vyta Wakulima na Wafanyabiashara wa mazao, kuweka mazao yao katika maghala hayo na kupewa Stakabadhi ambazo wataweza kuzitumia kama dhamana kupatia mikopo kutoka kwenye vyombo vyta fedha.

Ili utaratibu huu utoe manufaa yanayotarajiwa, kuna changamoto zinazotukabili. Nazo ni kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe utaratibu huu unavyofanya kazi na kuwahamasisha wautumie. Pili, kuhakikisha kuwa tunayo maghala muafaka ambayo yanaweza kutumiwa kuhifadhi mazao chini ya utaratibu huu. Tatu, ni suala la uaminifu. Hifadhi ya mazao ya wakulima ni suala linalohitaji uaminifu ili kuwajengea wakulima imani kuwa mazao yao hayatapotea. Wakulima wasipokuwa na imani na mfumo huu hawatatoa ushirikiano unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada mwingine uliopitishwa na Bunge lako Tukufu ni Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini wa Mwaka 2005. Madhumuni ya Muswada huu ni kutuwezesha kuweka utaratibu endelevu utakaotuwezesha kuendeleza huduma ya Nishati Vijijini ili kuwawezesha wananchi kupambana na umaskini. Upatikanaji wa Nishati Vijijini ni moja ya hatua muhimu zenye

lengo la kuboresha maisha ya wananchi na ukuaji wa uchumi endelevu Vijijini. Wakala wa Nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini, vitakuwa vyombo vyakutuwezesha kufikia malengo hayo. Hata hivyo ni vyema tutambue na kukubali kuwa nishati mbadala inayo nafasi muhimu sana katika harakati zetu za kuwafikishia wananchi wetu wengi nishati kwa matumizi yao.

Hivi sasa tunalo tatizo kubwa la matumizi yanayoongezeka ya kuni na mkaa kama chanzo cha nishati. Ongezeko hilo lina athari kubwa sana kwa mazingira. Pamoja na ukweli kuwa ongezeko la matumizi ya mkaa linatoa ajira kwa baadhi ya vijana Vijijini na hata Mijini, ni wazi kuwa ongezeko hilo linaashiria maafa kwetu. Ukataji wa miti ovyo unaongezeka tena kwa kasi kubwa. Sisi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi jinsi biashara ya mkaa inavyoshamiri kandokando mwa barabara zetu hasa zinazoingia Mijini. Matumaini yetu ni kuwa, wakala huu utasaidia sana kupunguza tatizo hili kubwa la ucharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa kupanua Elimu ya juu ili kutuwezesha kama Taifa kukidhi mahitaji mbalimbali ya wataalam yanayotuwezesha kukabiliana na changamoto zinazoletwa na utandawazi na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia. Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wa mwaka 2005, Muswada wa Sheria ya Uendeshaji wa Vyuo Vikuu wa mwaka 2005, pamoja na Azimio la Kuridhia Chuo cha Ufundii Mbeya kuwa Taasisi ya Sayansi na teknolojia inayojitegemea inatupa fursa za kupanua wigo wa Elimu ya juu kwa vijana wetu.

Hivi sasa tunalo ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza na kufaulu Kidato cha Sita. Takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2004 kulikuwepo na watahiniwa wa Shule 13,944 waliofanya mtihani wa Kidato cha Sita. Kati yao waliofaulu na kupata Daraja la I hadi la III walikuwa asilimia 91.33. Miaka 10 iliyopita, yaani mwaka 1995, watahiniwa wa Shule walikuwa 6,021. Kati yao waliofaulu kwa viwango cha Daraja la I hadi III walikuwa asilimia 65.5 tu.

Ni wazi basi kuwa, kama Taifa tunayo changamoto kubwa ya kuwawezesha vijana wetu wote wanaofaulu Elimu yao ya Sekondari kupata fursa ya kuijendeleza kitaaluma katika Vyuo vya Elimu ya juu. Ongezeko la Vyuo vya Elimu ya Juu na mabadiliko mbalimbali yanayofanywa ili Vyuo hivyo viweze kukidhi mahitaji ya sasa, yatatusaidia kwa sehemu kubwa kukabiliana na changamoto inayoletwala na juhudii zetu za kuboresha Elimu yetu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuhudhuria Semina mbili zilizokuwa zinalenga kuwapa fursa ya kutoa mawazo yao ili kuisaidia Serikali katika utekelezaji wa sera na mikakati ya kupambana na umaskini. Mkakati wa kupunguza umaskini na kukuza uchumi, yaani *MKUKUTA* pamoja na mifuko iliyoanzishwa kwa ajili hiyo, yaani Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund - TASAF*) na Mfuko wa Kutoa Mikopo Midogo Midogo (*Small Entrepreneurs Loan Facility - SELF*) imebuniwa na Serikali ili tuweze kuwa na

mfumo na taratibu zitakazokuwa zinatuongoza tuweze kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Bunge linao wajibu wa kuendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli katika Sekta mbalimbali ili kuhakikisha kuwa maamuzi yanayotolewa kuhusu vita dhidi ya umaskini yanatekelezwa na kwamba Bajeti ya Serikali inajielekeza katika suala hilo. Kwa vile vita dhidi ya umaskini vinawagusa wananchi huko walipo, tunao wajibu vile vile wa kuhakikisha kuwa tunawahamasisha, kuwaelimisha na kuwashirikisha katika kubuni na kutekeleza miradi yao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge vile vile wamepata fursa ya kujadili na kutoa maoni kuhusu uharakishaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Tumeweza kusikiliza taarifa iliyotolewa na Wajumbe wa Kamati iliyoundwa kuangalia jinsi mwenendo mzima wa utekelezaji wa Mkataba wa Afrika Mashariki unavyowezwa kuharakishwa.

Naomba nami niungane na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walioeleza kuwa hatuwezi kukwepa ushirikiano baina ya nchi zetu. Mabadiliko ya kiteknolojia hivi sasa ni ya kasi sana na hivyo kufanya suala la utandawazi kuwa sehemu ya maisha ya nchi zote duniani. Hata hivyo napenda nisisitize kama Taifa kwamba tunakabiliwa na changamoto ya kuhakikisha kuwa tunatumia utandawazi huo kwa manufaa na maslahi ya Taifa letu. (*Makofî*)

Ni wajibu wetu kutambua kuwa hatuwezi kubaki wenyewe katika mazingira ya kibashara na uwekezaji duniani kwani kwa vyovoyote vile hatuwezi kufunga soko letu kwa bidhaa kutoka nje iwe za nchi za Afrika Mashariki au za kanda na Mabara mengine. Kwa msingi huo, ni vyema Watanzania tukaanza kuchangamkia fursa zinazojitokeza na mazingira mazuri ya kibashara katika ukanda wetu. Wito wangu kwa Watanzania ni kuwa, tuache kulalamika na tuanze sasa kuchukua hatua za dhati za kutumia fursa na mazingira yanayojengwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, kufanya biashara na kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limehitimisha shughuli zote zilizopangwa katika Mkutano huu wa 19. Maisha ya Bunge hili, yanafikia ukingoni na tumbakiwa na Mkutano mmoja tu, nao ni ule wa Bajeti ya mwaka 2005/2006. (*Makofî*)

Bunge hili limefanya kazi kubwa na nyingi katika kusimamia na kuishauri Serikali. Hivyo, Bunge hili ni sehemu ya mafanikio tunayoyaona nchini, yawe ya uchumi, ustawi wa jamii, uboreshaji wa demokrasia na utawala bora na mengineyo mengi. Tunapokaribia kuhitimisha kipindi chetu cha miaka mitano, tunao wajibu wa kuwaeleza Watanzania wenzetu jinsi tulivyotoa mchango mkubwa katika uongozi na ustawi wa nchi yetu na watu wake wote. Maelezo hayo bila shaka yatatusaidia sana katika harakati zetu za kuomba nafasi za Uwakilishi tena katika Majimbo yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi nakushukuru kwa fursa ambazo umekuwa ukinipa za kutoa hoja za kuahirisha Bunge. Kwa kawaida Kiongozi wa Shughuli za

Serikali Bungeni hutoa hoja za kuahirisha Bunge katika Mikutano yake yote isipokuwa ule wa mwisho ambapo Bunge halahirishwi na badala yake, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huja kulivunja. (*Makofii/Kicheko*)

Kwa mantiki hiyo, huu ni Mkutano wangu wa mwisho kutoa hoja ya kuahirisha Bunge nikiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa Bunge la mwaka 2000 - 2005. Nimebahatika kupewa dhamana ya kuwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa kipindi chote cha karibu miaka 10 ya Uongozi wa Awamu ya Tatu, yaani uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa. Hivyo, kuahirisha kwangu leo Mkutano huu, pia ni hoja yangu ya mwisho kwa awamu hii ya tatu ya Uongozi wa Rais Mkapa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali imefanya mengi katika kutekeleza Ilani ya Chama Tawala, yaani Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, mengi bado yanahitajika kutekelezwa na Serikali itakayofuata, yaani Serikali ya Awamu ya Nne. Serikali ya Awamu ya Tatu, imepata mafanikio makubwa kwa sababu iliendeleza misingi iliyowekwa na awamu zilizotangulia.

Aidha, Viongozi waliotangulia pia wamekuwa wakitumika katika kutoa ushauri na busara zao katika masuala mbalimbali yanayohusu mustakabali wa nchi yetu. Hivyo, ni matumaini yangu na ninaamini na ya Watanzania wengi kuwa Awamu ya Nne ya Serikali, itafuata nyayo za Awamu ya Tatu ili kuendeleza kwa kasi zaidi maslahi na maendeleo ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sitarajii kuyazungumzia mafanikio na matatizo ambayo Serikali ya Awamu ya Tatu imekumbana nayo kwa sababu hayo nimekuwa nikiyatolea maelezo wakati wa kutoa hoja za kuahirisha Bunge lako Tukufu na wakati wa kutoa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Serikali. Nadhani kwa leo ni muhimu zaidi nikielezea mambo ambayo Watanzania wangependa Serikali yao ya Awamu ya Nne iwafanyie.

Kwa ujumla, Watanzania bado ni maskini. Huduma zao za kijamii hazitoshelezi mahitaji, bado wana kero nyingi zinazowakabili, wana wasiwasi na maisha na usalama wao, na kadhalika. Mambo haya yamekuwa yakishughulikiwa na awamu zilizopita na sasa Awamu ya Tatu. Misingi mizuri imekwishawekwa na linalohitajika hivi sasa ni kuiendeleza. Hivyo, Serikali ijayo ni lazima ijielekeze kwa dhati katika baadhi ya maeneo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni la uchumi. Katika ulimwengu wa sasa, jambo la msingi sana ni nchi kuwa na uchumi bora unaokidhi mahitaji muhimu ya watu wake. Uchumi mzuri ndiyo utakaoondoa tatizo la umaskini, huduma duni za jamii, kero mbalimbali, tatizo la ajira kwa wananchi wake na kadhalika. Ni lazima juhudhi ziendelezwe kwa nguvu zote katika eneo hili.

Hivi sasa uchumi wetu unakua kwa wastani wa asilimia sita kwa mwaka na mfumko wa bei umedhibitiwa vizuri ambao sasa uko kwa wastani wa asilimia 4.2 kwa

mwaka, kutoka wastani wa asilimia 27.5 miaka tisa iliyopita. Ili kuwa na uchumi unaokidhi mahitaji muhimu ya Watanzania, utahitajika ukuaji wa asilimia nane na zaidi kwa mwaka. Ili kufikia ukuaji huo, kuna maeneo muhimu ambayo lazima yazingatiwe. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni kilimo. Kilimo ndicho kinachobeba uchumi wetu kwa sehemu kubwa, kwa karibu asilimia 45 ya Pato la Taifa. Kwa umuhimu na uzito huo, kilimo kisipobadilika, kazi ya kukuza uchumi itakuwa ngumu sana. Kazi ya kwanza katika kilimo ni kuhakikisha kuwa kinakuwa cha tija na cha kutegemewa. (*Makofi*)

Lazima jitihada zifanywe ili kilimo cha umwagiliaji kianze kuchukua nafasi pale mazingira ya umwagiliaji yanapoweza kutekelezeka. Aidha, ni lazima kuelekea kwenye kilimo cha kati ambapo tija kubwa hupatikana kwa gharama nafuu. Tija iliyoko hivi sasa kwa mazao mengi haiwezi kubadili hali ya umaskini wa Mtanzania wala hali ya uchumi wetu. Hivyo, ni muhimu sana tukaanza kulima kibiashara badala ya kuendelea tu na kilimo cha kujikimu.

Suala muhimu ni kuweka vivutio maalum na kuwatafuta wawekezaji katika eneo la kilimo na usindikaji wa mazao. Aidha, kwa wakulima wadogo tija nayo iongezeke kwa kutumia njia za kilimo cha kisasa. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, eneo la pili katika uchumi ni uwekezaji na uwezeshaji. Hili ni eneo muhimu sana katika kukuza uchumi. Lazima Serikali iendelee kuboresha vivutio kwa wawekezaji wa nje na ndani. Mazingira ya sasa ni ya ushindani mkubwa na wenye fedha na mitaji yao watakwenda kule ambapo kuna vivutio vizuri zaidi. Hata Watanzania watakwenda kuwekeza kwingineko kama watashawishika kuwa mazingira ya uwekezaji ni mazuri zaidi huko kuliko nyumbani. Tuelewe kuwa yejote anayewekeza anatafuta faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili Tukufu, mwaka jana lilipitisha Sheria ya kuwawezesha Watanzania ili washiriki zaidi katika uchumi wa nchi yao na Kitengo kinachosimamia shughuli hii kimekwishaundwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Utekelezaji wa dhati katika eneo hili ni lazima usimamiwe na uonekane dhahiri katika awamu ijayo. Tanzania tunayo nafasi nzuri ya kuongeza uwekezaji kama tutapanga vipaumbele vyetu vyema. Wasiwasi wa kuwa tuko nyuma kwa maendeleo ya viwanda, hivyo hatuwezi kushindana na wenzetu, hayana sababu ya kuwa tishio. Sisi tunazo sekta nydingi ambazo tuna raslimali nydingi kuliko wenzetu hasa majirani zetu.

Kwa mfano, tuna ardhi nzuri na kubwa kwa ajili ya kilimo, tuna vivutio vingi vya utalii, tuna madini mengi, tuna bahari, maziwa na mito mingi kuliko jirani yejote, isipokuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa baadhi ya raslimali. Tukiweza kutumia raslimali hizi kwa ufanisi na kwa hakika, tutaongeza sana utajiri nchini mwetu. Serikali ya Awamu ya Nne, inalo jukumu kubwa la kuwawezesha eneo hili muhimu kuchangia katika ukuzaji wa uchumi wetu. (*Makofi*)

(c) Mheshimiwa Spika, eneo la pili, katika kukuza uchumi ni kuongeza mauzo nje. Nchi yetu inayo nafasi nzuri ya kuongeza mauzo nje, hasa mazao ya kilimo kama matunda, maua, mbogamboga, viungo, na kadhalika. Aidha, bidhaa nyingine za kilimo kama kahawa, pamba, korosho, katani, tumbaku, chai, na kadhalika, zinaweza kutuletea fedha nyingi kama uzalishaji na ubora utaongezeka ili kupunguza gharama za uzalishaji na wakulima wetu kupata faida kutokana na kilimo chao.

Aidha, tunalo tatizo kubwa la kuuza bidhaa za kilimo zikiwa ghafi. Ni lazima suala la usindikaji lipewe kipaumbele sana ili kuuza baada ya kuongeza thamani mazao yetu. Eneo lingine muhimu ni eneo la bidhaa za viwandani. Nchi yetu inayo nafasi nzuri ya kuuza bidhaa hizo katika masoko ya nje katika kanda zinazotuzunguka na hata nje ya Bara letu. Tutumie bahati ya kuwa na bahari na kuzungukwa na nchi zisizo na bandari kwa manufaa haya. Hivyo, ni lazima vivutio vizuri viwekwe ili tupate viwanda vikubwa na maeneo maalum ya uwekezaji (*Export Processing Zones*) yatengwe na kuendelezwa. Ni kwa kuuza bidhaa nje ndipo tutafanikiwa na kujenga utajiri nchini. Serikali ya Awamu ya Nne lazima ijitahidi kuongeza mauzo yetu nje (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili muhimu ni kuongeza mapato na kusimamia matumizi ya Serikali. Eneo lingine muhimu ambalo pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana ni lazima liendelee kupewa kipaumbele, ni lile la ukusanyaji wa mapato. Makusanyo ya Serikali yameongezeka kutoka wastani wa Shilingi bilioni 27 kwa mwezi mwaka 1995 hadi wastani wa Shilingi bilioni 150 kwa mwezi hivi sasa. Mafanikio haya ndiyo yaliyoiwesha Serikali kutekeleza *program* mbalimbali za maendeleo na pia kuboresha hali ya huduma kwa wananchi wake. (*Makofî*)

Kwa hiyo, Serikali ijayo ni lazima iendeleze juhud hizi ili kuongeza mapato zaidi. Uchumi wetu unayo nafasi ya kuongeza mapato ya Serikali. Makusanyo yetu hivi sasa ni wastani wa asilimia 13 ya Pato la Taifa. Kiasi hiki kinawenza kuongezwa sana endapo watu wengi zaidi watalipa kodi. Hivi sasa Watanzania wengi bado hawajui umuhimu wa kulipa kodi. Ni vyema Serikali ijayo ikaendeleza uhamasishaji na uelimishaji wa umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

Sambamba na kuongeza mapato, Serikali lazima isimamie matumizi ya fedha za Serikali kwa kuzingatia jinsi Bunge linavyoidhinisha matumizi hayo. Hivi sasa kuna fedha nyingi sana zinazopelekwa katika Halmashauri zetu za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji. Miradi ya *MMEM* na *MMES*, Miradi ya Afya na Maji, Mfuko wa Barabara na Miradi mingine kama *TASAF* ambayo sasa itakuwa kwa nchi nzima, ni mifano tu wa miradi hiyo. Fedha hizi zikisimamiwa vizuri na zikaunganishwa na nguvu za wananchi zitaleta mabadiliko makubwa sana ya huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni huduma za kiuchumi. Ukuaji wa uchumi unahitaji mazingira na mahitaji maalum. Huduma za kiuchumi zina umuhimu kwa uchumi sawa na mishipa ya damu katika mwili wa binadamu. Ili uchumi uweze kukua, lazima huduma za kiuchumi ziimishwe. Serikali imefanya kazi kubwa katika kuboresha njia mbalimbali za mawasiliano kama vile barabara kuu, barabara za Vijijini, upatikanaji wa umeme Mijini, viwandani na Vijijini, huduma za maji viwandani, huduma za

mawasiliano na kadhalika. Uboreshaji huu umesaidia sana ujenzi wa uchumi wetu. Hivyo, ni muhimu Serikali ijayo iendelete juhudi hizi kwa kasi kubwa zaidi. Hivi sasa ipo miradi mingi inayotekelawa na inayohusu barabara kuu, upelekaji wa umeme katika Wilaya na Mikoa mbalimbali, Miradi ya Maji, upelekaji wa mawasiliano na kadhalika. (*Makofî*)

Kazi ya kwanza ya Serikali ijayo ni kuhakikisha miradi hii iliyoko katika hatua mbalimbali za utekelezaji inakamilika. Sambamba na kazi hiyo ya ukamilishaji, ni kuendelea kujenga miundombinu mipya ya kuhudumia uchumi kwa sababu jinsi uchumi unavyokuwa, ndivyo mahitaji ya huduma za uchumi yatakavyoongezeka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uboreshaji mkubwa wa huduma zetu za jamii kama vile elimu, afya, maji, barabara Vijijini na kadhalika. Uboreshaji huu umetokana na Serikali kuelekeza sehemu kubwa ya mapato yake hasa yale yaliyotokana na kusamehewa madeni katika Sekta hizi za huduma. Aidha, ushirikishwaji wa wananchi pia umekuwa sehemu muhimu sana ya mafanikio katika eneo hili. Hivi leo, elimu ya msingi imeboreka sana na sasa tunao Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari na hatimaye hadi ngazi nyingine za juu za elimu.

Kwa upande wa afya upatikanaji wa huduma katika ngazi mbalimbali, umekuwa wa uhakika zaidi. Dawa zinapatikana katika Hospitali zetu zote kuanzia Zahanati Vijijini hadi Hospitali Kuu. Huduma nyingine muhimu nazo zimeboreka. Huduma ya maji nayo imeendelea kuboreshwa Mijini na Vijini na barabara za Vijijini halikadhalika. Uimarishaji wa huduma hizi umeboresha sana maisha ya wananchi na kuwapa matumaini makubwa ya huduma bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijayo ni lazima ikubali changamoto hizi. Kwanza ni kuendelea kuboresha huduma hizi kwa vile mahitaji yake yataongezeka sana na pili ni changamoto itakayotokana na huduma kuwa nzuri, yaani matatizo yatakayotokana na mafanikio. Kwa mfano, kuboreshwa kwa Shule za Msingi, maana yake ni watoto wengi zaidi kufaulu kwenda Sekondari. Hivyo, ni lazima Shule za Sekondari zijengwe nyingi zaidi. Eneo la tano, ni utawala bora na udumishaji wa demokrasia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki cha miaka 10 ndicho kipindi ambapo nchi yetu imekuwa chini ya Mfumo wa Siasa ya Demokrasia ya Vyama Vingi. Pamoja na upya na uchanga wa Mfumo huo nchini petu, sote ni mashahidi wa jinsi demokrasia ilivyoeendelea kukua katika nchi yetu. Aidha, suala la utawala bora limesimamiwa kwa nguvu zote na Serikali na wananchi wameweza kuona matunda yake. Wananchi wa Tanzania hivi sasa wanajua haki zao zaidi kuliko ilivyokuwa na pale ambapo wanaona wanakandamizwa, kuonewa au kunyanyaswa, Watanzania wamekuwa wakipiga kelele na kulalamika. Serikali ijayo ni lazima iendelee kusimamia suala la utawala bora na kudumisha demokrasia na kuhakikisha wananchi wanapata haki zao kama inavyopasa. Utawala bora na demokrasia ya kweli katika ngazi zote ni mihimili mizuri sana ya amani na utulivu nchini.

Eneo lingine ambalo Serikali ijayo lazima iliangalie kwa makini ili utawala bora uonekane wazi, ni lile la utoaji wa haki. Mahakama zetu zina upungufu mkubwa wa Watendaji, yaani Mahakimu na Majaji na pia vitendea kazi. Uboreshaji katika eneo hili umekwishaanza, lakini lazima uendelezwe kwa kasi zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo la sita ni kero. Watanzania kama jamii nyingine yoyote wanakerwa na matendo na matukio mbalimbali. Katika jamii yetu, bado tunayo matatizo ya rushwa, matumizi ya dawa za kulevyo, ujambazi, wizi, unyanyasaji na kadha wa kadha. Serikali imejithidi sana kupambana na kero hizi na kwa sehemu kubwa mafanikio yanaonekana lakini bado kero hizi ni tatizo kwa Watanzania. Serikali ijayo inao wajibu wa kuendelea kupambana na kero hizi kwa dhati na kuhakikisha kuwa, kwa sehemu kubwa ya kero hizo zinapunguzwa kama sio kuondolewa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ulinzi na usalama, nchi yetu ni ya kupigiwa mfano kwa suala la amani na utulivu. Ndiyo maana imepewa jina la Kisiwa cha Amani. Lakini amani na utulivu huu tumekuwa nao kwa sababu vimejengwa na kusimamiwa.

Kwa upande wa usalama wa raia, Majeshi yetu ya Polisi na Magereza yanafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa katika hali ya usalama na kwamba wahalifu wanashughulikiwa ipasavyo. Sote tunakubali kwamba Jeshi letu la Polisi pamoja na juhudzi zote hizi limekuwa likifanya kazi katika mazingira magumu yanayosababishwa na hali yetu ya uchumi. Hata hivyo, kadri uchumi unavyoboreka, ndivyo Serikali ilivyojithidi kuboresha mazingira na maslahi ya Jeshi letu la Polisi. Bado hatujafikia viwango vikubwa, lakini juhudzi inaonekana na inaridhisha.

Kwa upande wa ulinzi wa nchi yetu, Jeshi letu la Ulinzi linafanya kazi nzuri sana na ni Jeshi la kupigiwa mfano. Nalo pia linafanya kazi kubwa katika mazingira magumu. Kwa kadri hali ya uchumi ilivyoimarika ndivyo Serikali ilivyojithidi kuboresha maslahi na mazingira ya kazi kwa wanajeshi wetu. Hivyo, ili tuendelee kuwa Kisiwa cha Amani, ni lazima ulinzi wa nchi yetu wa ndani na wa nje ya mipaka yetu uendelee kusimamiwa kikamilifu na kuimarishe. Serikali ijayo inao wajibu wa kuendelea kudumisha amani na utulivu wetu na kuimarishe Majeshi yetu kwa kuyapatia mahitaji muhimu ya kazi na ya maslahi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ambaa hivi sasa umetimiza miaka 41 ni wa kupigiwa mfano katika Bara la Afrika na hata duniani kote. Muungano huu ni wa Watanzania kwa maslahi ya Watanzania. Wapo ambaa wanapenda kuubeza Muungano wetu, lakini bila shaka hawaelewi ni nini kingetokea kama Muungano huu usingekuwepo. Amani na umoja tunaojivunia Watanzania, vimedumishwa katika misingi imara ya Muungano wetu. Hivyo, ni lazima tuendelee kudumisha Muungano kwa gharama yoyote. Serikali ijayo lazima ifahamu hili na iendelee kudumisha Muungano wa Watanzania kwa maslahi ya Watanzania wote wa Bara na Zanzibar. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine muhimu, eneo la kwanza ni *UKIMWI*. Ukubwa wa tatizo la ugonjwa wa *UKIMWI* halihitaji msisitizo zaidi hasa katika Bara la Afrika Kusini mwa jangwa la Sahara. Nchini petu hivi sasa watu karibu wote

wanafahamu *UKIMWI* ni nini, jinsi unavyoambukizwa na nini la kufanya ili kuepuka maambukizi. Aidha, wanafahamu kuwa ugonjwa huu hauna tiba. Pamoja na ufahamu huo, bado Watanzania wameshindwa kubadili tabia na maambukizi yameendelea kuongezeka. Ugonjwa huu zaidi ya kupoteza maisha ya Watanzania wenzetu una madhara mengi sana kwa jamii na hata uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, *UKIMWI* kwa kiwango kikubwa huua wale wenye nguvu ya kufanya kazi. Familia inayouguza mgonjwa wa *UKIMWI* mara nyingi huachwa katika hali ya umaskini mkubwa kwa vile mali zote zinakuwa zimetumika katika matibabu. Tatizo lingine kubwa kabisa ni kuachiwa yatima wengi kwa ajili ya tabia ya ugonjwa huu wenyewe ya kuua wazazi wote. Serikali ijayo lazima ipigane kufa na kupona na tatizo la *UKIMWI*, vinginevyo yote mema tunayoyapanga hayatakuwa na maana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni la madeni. Nchi yetu inakabiliwa na madeni makubwa ya ndani na ya nje. Kwa yale ya ndani, kazi kubwa ya kuyapunguza imefanywa kwa kuyalipa, ingawa bado madeni mapya yameendelea kuongezeka. Kwa upande wa yale ya nje, haya ni makubwa na kwa kweli uwerekano wa kuyalipa ni mdogo sana. Serikali kwa kusaidiana na Serikali nyingine za nchi maskini pamoja na Taasisi zenye huruma kwa watu maskini, zimekuwa zikidai nchi tajiri na Taasisi zao kufuta kabisa madeni kwa nchi maskini.

Napenda kupongeza juhudzi za Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwa kuwa mstari wa mbele katika vita hii. Serikali ijayo haina budi kuendeleza juhudzi hizi za kutafuta ufumbuzi wa tatizo la madeni ya ndani kwa kuyalipa. Aidha, Rais ajaye madarakani atambue umuhimu wa udhibiti wa madeni ya nje na aendeleze juhudzi zilizoanzishwa na Rais Benjamin William Mkapa akishirikiana na wengine katika kudai kuzishinikiza nchi tajiri na Mashirika yao kufuta kabisa madeni kwa nchi maskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu katika maeneo maalum ni maslahi ya wafanyakazi. Mishahara ya wafanyakazi wetu bado ni midogo na haitoshelezi mahitaji muhimu ya wafanyakazi na familia zao. Hata hivyo, Serikali imefanya jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba inawalipa wafanyakazi kadri inavyoonezekana na kwa kadri uchumi wetu unavyoruhusu. Hivi leo kima cha chini cha mshahara wa watumishi wa Serikali ni Shilingi 60,000/= kutoka Shilingi 17,500/= miaka tisa iliyopita. Hata hivyo, kwa kadri uchumi unavyokua, ndivyo Serikali ijayo itakavyokuwa na wajibu wa kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi ili waweze kukidhi mahitaji yao muhimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ni la ajira. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la vijana wetu kuja Mijini kutafuta ajira. Aidha, kwa jinsi ambavo idadi kubwa ya vijana wanaomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari inavyoongezeka, ndivyo idadi kubwa ya watafuta ajira nayo inavyoongezeka. Kuna aina mbili za ajira. Ajira ya mshahara na ajira ya kujitegemea. Ajira hizi zote zinategemea sana hali ya uchumi ingawa ile ya kujitegemea ina tabia ya kujitegemea kulingana na aina ya ajira yenye, kwa mfano, kujiajiri katika kilimo.

Hivyo, ili kukabiliana na tatizo hili la ajira, suluhisho endelevu na la uhakika ni kukuza uchumi ili kutuwezesha kuwa na viwanda vya kutosha na nafasi nyingi zaidi za ajira. Hata hivyo, kama nilivyoeleza, bado tunayo ardhi ya kutosha kwa wale ambao wanawenza wakajajiri katika kilimo na kukifanya kiwe kilimo cha biashara zaidi kuliko cha kujikimu. Jambo lingine ambalo ni muhimu katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo la ajira, ni kuimarisha Elimu ya Ufundu ili kuwajengea vijana wetu uwezo wa kujajiri. Serikali ijayo inao wajibu wa kuendeleza na kuboresha uchumi ili kuepukana na tatizo linalokua kwa kasi la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana, jambo ambalo ni hatari hata kwa amani ya Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika utafutaji wa madini na mafuta, katika eneo la madini, mafaniko makubwa yameonekana japo utafiti zaidi unahitajika. Eneo la mafuta bado hatujafanikiwa japo tafiti zilizopita zinaonyesha kuwa matumaini yapo. Eneo hili linatakiwa lisimamiwe na wenye uwezo wapatikane ili kama kweli mafuta yapo yachimbwe na nchi yetu na watu wake wanufaidike na rasilimali hii. Serikali ijayo itabidi iweke juhudini kubwa katika eneo hili. Rasilimali ikibaki chini ya ardhi haitusaidii.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu kama ilivyo kwa baadhi ya nchi, kiwango cha maendeleo kinapishana kutoka eneo moja hadi lingine. Hali hii imeanza kuwa dhahiri kati ya Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa, Kanda na Kanda na hata sehemu ya jamii na nyingine. Kuna maeneo ambapo kwa mfano, Shule ni chache sana, huduma za afya ni duni, wakati maeneo mengine yana unafuu sana.

Aidha, kuna tofauti zinazojitokeza sana za watu binafsi au makundi ya watu kupishana sana kwa mapato. Serikali ijayo ni lazima ione namna ya kukabiliana na changamoto hii bila ya kuwakwamisha wanaendelea kwa kasi katika maendeleo wala kuwakwamisha wenye juhudini za kutafuta fedha kwa utaratibu halali. Lengo liwe ni kuwapatia fursa zaidi wale walioko nyuma ili waongeze kasi yao ili hatimaye waende pamoa na wale walioko mbele yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, haya machache niliyoyaeleza, ni mtazamo wangu na ushauri wangu kwa manufaa ya Serikali ijayo na wananchi kwa ujumla. Haya siyo maelekezo kwa Serikali ijayo, bali ni mawazo yenye nia njema kwa nchi yetu na yenye mwelekeo wa kuongeza kasi ya maendeleo kwa manufaa yetu sote. Aidha, yapo maeneo mengine ambayo sikuyataja katika hotuba hii na wala isingewezekana kutaja yote kwa sababu ni mengi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tumebakiza miezi sita tu kabla nchi yetu hajifanya Uchaguzi wake Mkuu. Maandalizi muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu yanaendelea vyema. Zoezi la uandikishaji Wapigakura katika Daftari la Kudumu la Wapigakura limehitimishwa tarehe 18 Aprili mwaka huu kwa upande wa Tanzania Bara kwa mafanikio makubwa. Kazi nyingine muhimu za kuliandaa Daftari hilo zinaendelea.

Vyama vya Siasa navyo viro katika mchakato wa kuwapata Wagombea wao katika ngazi mbalimbali. Naomba nitumie fursa hii kikipongeza Chama Cha Wananchi

(CUF) kwa kufanya Mkutano wake Mkuu kwa amani na utulivu. Aidha, ninawapongeza Profesa Ibrahim Lipumba kwa kuteuliwa kuwa Mgombea wa Chama hicho wa Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Maalim Seif Shariff Hamad kuwa Mgombea wa Kiti cha Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Huo ndio utamaduni wa kidemokrasia ndani ya Vyama tunaotarajia kuuimarisha katika Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika muda mfupi ujao *CCM* nayo itaanza mchakato wa kuwapata Wagombea wake kwa ngazi ya Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Naomba nirudie sehemu hiyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika muda mfupi ujao, *CCM* nayo itaanza mchakato wa kuwapata Wagombea wake kwa ngazi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ule wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (*Makofî*)

Napenda kutumia fursa hii kikitakia Chama Cha Mapinduzi kila la kheri katika mchakato huo. Napenda pia kuwatakia kila jema wote wanaowania nafasi hizo. (*Makofî*)

Kushamiri kwa demokrasia ndani ya Vyama vya Siasa kutawezesha vile vile kuimarka kwa demokrasia ya Vyama Vingi na hivyo kujenga misingi imara ya Siasa za ushindani zinazojengwa chini ya misingi ya upendo, mshikamano na Umoja wa Kitaifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kadri muda unavyokaribia Uchaguzi Mkuu, ndivyo hatua nydingine muhimu zitakavyoweza kuchukuliwa ili kuwawezesha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba ya kuwachagua viongozi wao. Wito wangu kwa Watanzania wote ni kuwa, tunao wajibu kama Taifa wa kuhakikisha kuwa mchakato wa kuelekea kwenye kilele cha Uchaguzi Mkuu unakuwa wa amani na unaozingatia sheria na taratibu. Tusiruhusu jazba na hisia kali za kisiasa kuvuruga amani na utulivu wetu. Kila mara tujitahidi kutumia taratibu zilizowekwa na Sheria kutatua matatizo yanayojitekeza.

Aidha, ninao wito maalum kwa Viongozi wenzangu wa kisiasa. Kauli zetu zinaweza kuwasho moto wa vurugu ambao unaweza kusababisha kuvunjika kwa amani. Ni vyema tutumie busara zaidi katika kufikisha ujumbe wetu kwa Wanachama wetu na kwa wananchi wa ujumla. Hakipo Chama cha Siasa kitakachonufaika katika mazingira ya fujo na vurugu. Siasa ya Vyama Vingi inashamiri pale penye amani, kwani amani hutoa fursa kwa mijadala, Mikutano ya Kisiasa na midahalo ambapo hoja mbalimbali kuhusu mustakabali wa nchi yetu hutolewa na kujadiliwa na wenye hoja zenye nguvu hukubaliwa na kupewa ridhaa ya kuongoza. Huo ndio utamaduni ambao Watanzania hatuna budi kuulinda na kuutetea. (*Makofî*)

Mheshimwia Spika, hivi sasa tayari zimeanza kujitokeza dalili za badhi ya Vyama au wafuasi wao kutaka kufanya fujo. Dalili hizi mbaya ziko ndani ya Vyama vyenyewe, baina ya Vyama na hata baina ya baadhi ya Vyama na Serikali, hasa vyombo vya usalama wa raia. Viko Vyama au watu wao ambao wanatamka kuwa lazima watashinda Uchaguzi, vinginevyo hakuna suluhu. Huo sio utaratibu wa demokrasia, bali ni udikteta

na nchi hii hatutakubali kuongozwa kwa udikteta. Ni vyema tukaelewa kuwa jinsi ambavyo Chama chako au wewe mwenyewe ulivyo na hamu ya kushinda, ndivyo na mshindani au washindani wako walivyo na hamu ya kushinda hivyo hivyo. Tuwaachie wananchi waamue kwa haki na uhuru bila fujo wala vitisho. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pale ambapo itaonekana kuna watu wanaotaka kuvunja amani kwa uroho wao wa madaraka au kwa sababu yoyote ile, Serikali itatekeleza wajibu wake wa kulinda raia wema na kuwaadhibu wanaovunja sheria. Hivyo, ninapenda kuwashakikishia wananchi wote kuwa wasiwe na wasiwasi, Uchaguzi Mkuu utakuwa wa salama. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, uongozi wako makini pamoja na msaada ulioupata kutoka kwa Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge wa Tunduru; Wenyeviti, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi na Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, ndio uliotuwezesha kukamilisha kazi zote zilizokuwa zimepangwa katika Mkutano huu na pia kwa Mikutano yote 19 iliyopita. Naomba nikushukuru wewe, Naibu Spika wako na Wenyeviti kwa uongozi wenu imara. Shughuli za Bunge zinaanza kwenye Kamati za Kudumu. Napenda vile vile niwashukuru kwa dhati Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge na Wajumbe wao kwa kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa; Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Damian Foka, wametekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa sana. Kwa niaba yenu napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Damian Foka kwa kazi nzuri. Nawashukuru vile vie watumishi wote wa Serikali walioiwezesha Serikali kujibu maswali na kuwasilisha hoja mbalimbali za Serikali katika Mkutano huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Vyombo vyta Habari kama kawaida yao vimetoa habari na kuielimisha jamii kuhusu kazi zilizokuwa zinatekelezwa na Mkutano huu. Napenda niwapongeze Waandishi wa Habari na Wahariri wao kwa jinsi wanavyotoa taarifa kuhusu shughuli zinazotekelawa katika kila Kikao na kila Mkutano. Wito wangu kwa Wanahabari ni kuwa waendelee kila mara kutoa habari sahihi ili wananchi waweze kuelewa maamuzi mbalimbali yanayofanywa na chombo chao cha uwakilishi na misingi ya maamuzi hayo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kama nilivyoeleza awali, ninyi Waheshimiwa Wabunge ni sehemu muhimu sana ya mafanikio yote ya Serikali. Ninyi ndiyo mlolioishauri Serikali na kuibana pale ilipobidi. Sheria zote ambazo zinasimamia uwekezaji na uchumi kwa ujumla mmezipitisha ninyi. Ninapenda niwashukuru sana kwa niaba ya Serikali kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa niaba ya wananchi mnaowawakilisha. Ninaamini kabisa mtaendelea kushirikiana na Serikali yenu katika kuishauri na kuisimamia katika muda uliobakia. Mimi kwa niaba ya Serikali ninawahakikishia kuwa ushauri wenu utachukuliwa kwa kadri inavyowezekana hata ule mtakaoutoa katika Kikao cha mwisho cha Mkutano wa 20. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwatia moyo Waheshimiwa Wabunge. Naelewa kuwa katika kipindi hiki, wakati wao wakiendelea na Mkutano na

shughuli nyingine za Bunge, wapo Watanzania wengine wanaopitapita kwenye Majimbo yao wakijitambulisha ili nao waweze kupewa ridhaa ya uwakilishi. Wito wangu kwenu ni kuwa, wananchi ndio wanaojua kazi mlizowasaidia na jinsi mlivyoweza kuwawakilisha vyema. Bila shaka tutaweza kuhitimisha kipindi chetu salama na kuweza kupewa tena ridhaa mara muda utakapowadia. Ninawatachia safari njema ya kurudi kwenye Majimbo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 7 Juni, 2005 litakapokutana tena saa 3.00 asubuhi hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaiamua hoja hiyo. Napenda kutoa taarifa rasmi kwamba hiyo tarehe 7 Juni, 2005, yaani siku ya kwanza ya Mkutano ujao wa Bunge, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano atalihutubia Bunge hili. (*Makofi*)

Halafu nikumbushe kwamba Kamati zetu zote za Kudumu zinaanza kukutana Mjini Dar es Salaam tarehe 23 Mei, 2005. Kwa hiyo, tuna muda mfupi tu chini ya wiki tatu kati ya sasa na shughuli za Kamati zitakapoanza. Tukijipanga vizuri tutaweza. Baada ya taarifa hiyo, Bunge linaahirishwa hadi siku ya Jumanne, tarehe 7 Juni, mwaka huu 2005 saa tatu asubuhi.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Saa 11.58 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne,  
Tarehe 7 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi*)